**BUNGE LA TANZANIA**

___________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

___________

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 18 Juni, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Lediana M. Mng'ong'o) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatakia Heri ya Mfungo Mtukufu wa Ramadhani. Nawatakia Watanzania wote Heri ya Mfungo wa Ramadhani. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 219

**Ahadi ya Kumaliza Tatizo la Wakulima – Kagera Nkanda**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Mnamo mwaka 2011 na Desemba 2013, kwa nyakati tofauti, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kumaliza tatizo la Wakulima wa Kasulu wanaolima katika eneo la Kagera Nkanda wanaofukuzwa na kupigwa kila mwaka kwa agizo la Mkuu wa Wilaya ya Kasulu:-

Je, ni sababu gani zinazokwamisha kushughulikiwa kwa suala hilo kwa takribani miaka mitano sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi walioondolewa katika Kijiji cha Kagera Nkanda ni wale ambao walikuwa wanalima katika eneo ambalo Hifadhi ya Kagera Nkanda, ambapo eneo hilo kisheria haliruhusiwi kwa sababu ya kihifadhi. Aidha, ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kumaliza tatizo la Wakulima hao, kwa kuwapatia ardhi kwa ajili ya kilimo bila kuingilia mipaka ya Hifadhi.

Eneo linalozungumzwa hapa ni eneo linalotambulika kisheria kuwa ni Hifadhi ya Misitu ya Makere Kusini, ambapo baadhi ya Wananchi wa Kijiji cha Kagera Nkanda waliingia kinyume cha Sheria katika Hifadhi hiyo kwa ajili ya kilimo. Viongozi wa Wilaya ya Kasulu kwa kushirikiana

na Wakala wa Huduma za Hifadhi za Misitu ya Tanzania *(TFS),* Kanda ya Kigoma, imekuwa ikichukua hatua za kisheria kuwaondoa Wananchi wanaovamia eneo la Hifadhi hiyo, ambayo ni hazina ya Taifa lenye maliasili adimu na ambayo ni chanzo cha mapato kwa Taifa na pia ni muhimu kwa mustakabali wa hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu kwa Wananchi wa Wilaya ya Kasulu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kuhakikisha Wananchi wa Kijiji cha Kagera Nkanda wanapata ardhi kwa ajili ya kilimo, ni kutoa wito kwa Uongozi wa Kijiji kuainisha mahitaji ya ardhi kwa wananchi wa Kijiji hicho ili Halmashauri iweze kuwapatia maeneo mengine kwa ajili ya shughuli za kilimo. Mfano, kikundi cha UWT walioomba ekari 200 walipelekwa Kijiji cha Kitanga, Kikundi cha Mrubona waliomba ekari 1,500 walipelekwa Kijiji cha Titye, Kikundi cha Kilimo Kwanza kiliomba ekari 15,600 na kupelekwa Kijiji cha Kitanga, Kijiji cha Tukomboane kiliomba ekari 200 na kupelekwa Mwanga B, Kikundi cha Juhudi Tujenge Taifa kiliomba ekari 900 na kupelekwa Rungwe Mpya na Kaguruka. Maeneo mbalimbali ambayo tayari yana maeneo ya akiba ya ardhi kwa ajili ya kilimo ni pamoja na Mvugwe ekari 10,308, Kitanga ekari 132,950, Kitagata ekari 613, Kigadye ekari 32, Malalo ekari 500 na Mvinza ekari 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kutatua tatizo la Wakulima wa Wilaya ya Kasulu hususan Kijiji cha Kagera Nkanda, limetekelezwa kwa kuwatengea Wananchi ardhi kwa maeneo mengine ukiacha eneo la Hifadhi. Naomba kutoa wito kwa Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, kuhakikisha Mipaka ya Hifadhi ya Taifa inalindwa na kuheshimiwa ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nisikitike kwa majibu ya uongo na ya uzushi ambayo yanatolewa na Serikali hapa Bungeni. Nasema hivi kwa sababu nimepata kuuliza huko nyuma, moja, Serikali ilijibu hapa Bungeni kupitia Waziri wa Maliasili na Utalii. Nilieleza wananchi walipigwa na kunyang'anywa mali zao, Serikali ikaja ikatoa majibu ya uongo kwamba, hakuna Mwananchi aliyepigwa wala kunyang'anywa mali zake. Leo Serikali inaeleza kwamba, wananchi kupitia vikundi hivi wamepewa mashamba katika maeneo mbalimbali. Kwanza, naomba ifahamike pia …

**MWENYEKITI:** Uliza swali!

**MHE. MOSES J. MACHALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali ndiyo najenga hoja. Moja siyo wananchi wa kijiji hicho tu ambao wanahitaji ardhi. Maeneo hayo watu wanatoka katika vijiji mbalimbali wamekuwa wakilima huko kwa zaidi ya miaka 40.

(i) Kwa kuwa Wananchi wa Wilaya ya Kasulu ambao wanatoka kwenye vijiji mbalimbali siyo kweli ikiwemo wanaotoka Kasulu Mjini hawajapata mashamba kama ambavyo majibu haya ni ya uongo na mimi natoka huko. Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watendaji ambao wamekuletea majibu ya uongo ambayo hayana ukweli na leo unalieleza Bunge hapa Mheshimiwa Waziri?

(ii) Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kabla hatujahitimisha Bunge hili kwa niaba ya Waziri Mkuu twende ukawasikilize wananchi wenyewe wanakwambia nini uweze kuthibitisha kwamba majibu haya ni ya uongo na uzushi na hayajapata kutokea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anamfahamu Afisa Ardhi anaitwa

Richard Makupe. *I want to be concrete,* kuwa *concrete* ni kusema Moses Machali, Aggrey Mwanri, ndiyo kuwa *concrete*. Asubuhi hii saa kumi na mbili, nimezungumza nae nimemsomea majibu haya, alisema haya ndiyo majibu yetu ya Kasulu. Kwa hiyo, habari ya uzushi kwamba kuna uzushi unatoka hapa, mimi nimekaa vizuri, kuamka kwangu saa kumi na moja kwa ajili ya jambo hili linalozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kama eneo la Kagera Nkanda ni eneo ambalo watu wanaruhusiwa kwenda kulima kule, Mheshimiwa Mbunge atuambie sisi katika Bunge hili. Ninachosema hapa eneo hili ni la Hifadhi na kama nimezusha hapa eneo hili siyo la Hifadhi, Mheshimiwa yupo hapa na sisi tuko wote hapa; hakuna uzushi wowote unaozungumzwa hapa.

La tatu, maeneo haya ambayo nimeyataja yote ambayo yamesemwa yametengwa, hatukusema kwamba wamekwisha kupewa. Tumesema kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda pale akatoa maelekezo, nimesoma hapa na nililosoma mimi ndilo lililoingia kwenye *Hansard,* lilisahihisha hilo eneo. Eneo hilo unalolisoma lilikuwa limekwenda kwa kimakosa na ndiyo maana nili-*cross-check.* Nilichosema hapa nimesema maeneo haya yametengwa kwa ajili ya kutoa. Kwa hiyo, mimi hapa najua ninachosema kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, majibu ninayoyatoa ni haya yaliyoko hapa. Nataka tuelewane vizuri na Mheshimiwa Machali, wala hakuna tatizo kabisa katika jambo hili. Jambo hili siyo tu la kusema sasa jamani waruhusuni hawa watu waende pale. Kesho nitawekwa kwenye *carpet* hapa, Aggrey Mwanri, Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ameruhusu Wananchi waende katika eneo la Hifadhi kinyume cha taratibu na Sheria za nchi. Hiki ndicho ninachokichunga hapa. Habari nyingine tanayoizungumzwa hapa, wala sihitaji kwenda Kasulu wala Kigoma, nikitoka hapa nampigia Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, ambaye ni Msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali pamoja na Mkuu wa Wilaya, kuwaambia kuna tatizo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa kwa kifupi ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, unapata majibu wewe unaendelea kuzungumza. Unahitaji majibu ngoja wakupe.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema majibu ndiyo haya. Hapa sibadilishi kitu chochote. Kazi yangu hapa kuimarisha Torati wala sito kutengua Torati.

Na. 220

**Shule za Wananchi za Kata Kukosa Vifaa vya Masomo ya Sayansi**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA (K.n.y. MHE. ALIKO N. KIBONA)** aliuliza:-

Wanafunzi wengi wa Shule za Wananchi wamekuwa wakifanya vibaya katika masomo ya sayansi kwa shule hizo kukosa vifaa vya kufundisha masomo hayo na Wizara ya Afya na Ustawi na Jamii imepandisha sifa za kujiunga na mafunzo ya Kada ya Afya kwa kumtaka mhitimu kuwa na *credit* katika masomo ya sayansi:-

(a) Je, kwa kufanya hivyo Serikali haioni ni kutengeneza ufa na ubaguzi kwa wenye nacho kuendelea kuwa nacho na wasio nacho kuendelea kuwa watawaliwa?

(b) Je, Serikali haioni ipo haja ya kurejea kwenye misingi ya Azimio la Arusha ya kila mtu kupata haki sawa bila kubaguliwa kwa sababu ya kipato ili kuendelea kulinda umoja, upendo na mshikamano katika Taifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa zinazotumika kudahili wanafunzi zinazingatia hali halisi ya mahitaji kitaaluma katika kujiunga na mafunzo mbalimbali ikiwemo uuguzi. Utaratibu huu unaweka uwiano sawa kwa wanafunzi wote wenye sifa kujiunga na mafunzo ikiwemo wanafunzi wanaotoka katika Shule za Wananchi za Kata. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa katika Mitihani ya Kitaifa, unaonesha watahiniwa waliofaulu kwa Daraja I – III, ambao ndio wana sifa za kujiunga na elimu ya juu na mafunzo mbalimbali walikuwa asilimia 88.25 kwa Shule za Sekondari za Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini hii inaonesha ubora wa Shule za Wananchi kuongezeka na zinatoa wanafunzi wengi wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu na mafunzo mbalimbali kwa ushindani sawa na shule nyingine.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari nchini zimeendelea kuimarishwa ikiwemo Shule za Wananchi katika Kata ili kuhakikisha kuwa Wananchi wanapata fursa sawa za kupata elimu iliyo bora nchini. Kupitia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), pamoja na kusimamia Mpango wa Ukamilishaji wa Ujenzi wa Maabara kwa Shule zote za Sekondari, Serikali itakarabati na kukamilisha Shule za Sekondari 1,200 za Wananchi, yaani zile za Kata kwa kiwango cha kuwa na miundombinu yote muhimu ikiwemo maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Kwanza imekamilisha shule 264 ambazo zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 56.3. Awamu ya Pili itahusisha shule 528 na Awamu ya Tatu shule 408. Mwaka 2014 pamoja na utoaji wa fedha za uendeshaji, Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.1 kwa shule za sekondari 75 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara na ukarabati mdogo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani, imesambaza vitabu 2,500,000 vya masomo ya kemia, baiolojia, fizikia na hisabati na kuimarisha uwiano kufikia kitabu kimoja kwa wanafunzi wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuziimarisha shule hizi kupitia Mpango wa MMES na kushirikiana na wadau mbalimbali ili ziendelee kutoa fursa kwa Vijana wa Kitanzania kupata elimu.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu mazuri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kuna baadhi ya shule ambazo hazina *mobile lab* ambazo zinasaidia sana kuwafanya watoto wetu wanaosoma kwenye shule zisizokuwa na maabara waweze kufanya mtihani huu wa masomo ya sayansi. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha kuwa shule zote ambazo maabara hazijakamilika wanapatiwa *mobile lab* ziweze kuwasaidia kufanya masomo ya sayansi ili watoto hawa nao waweze ku-*compete* kwenye nafasi hizi za udaktari na nyingine zinazohusiana na fani ya sayansi?

(ii) Katika kudahili Wanafunzi kwenda kusomea udaktari, *TCU* kwa kiasi kikubwa sana inawachukua Wanafunzi ambao wanasoma aidha *PCM* au *PCB,* lakini wanafunzi wanaosoma masomo ya *CBG* hawawezi kuchaguliwa kwa sababu hawana somo la *mathematics* au *physics*, lakini Wanafunzi wanaosoma *CBG* somo la *mathematics* wanasoma. Sababu gani inayosababisha *TCU* isiwachague watoto wanaosoma *CBG* kwenda kusomea masomo ya udaktari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *mobile lab* niseme tu kwamba, mkazo ambao tumeuweka Serikalini hivi sasa kwa Mwongozo wa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ni kuhakikisha Shule zetu za Sekondari zote za Serikali na za Wananchi, zinakuwa na maabara kamili za kisasa na zenye vifaa vyote. Mahitaji yetu ni jumla maabara 10,085, sasa hivi tumeshakamilisha 2,628, ambazo ziko katika hatua za kukamilika ni 4,038 na zinazoendelea kujengwa ni 3,419. Si muda mrefu tutakuwa na maabara zote za fizikia, kemia na bailojia kwa kila Shule ya Kata. Kwa hiyo, biashara ya *mobile lab, science kit* na kadhalika, sasa hivi tunataka tuachane nayo.

Mheshimiwa Rais alitupa *deadline* ya mwisho wa mwezi wa sita mwaka huu. Najua hatutamudu mwishoni mwa mwezi wa sita bila shaka tutakuwa na deni hapo, lakini tunachokwenda nacho ni kwamba, *only* maabara zilizokamilika zenye vifaa kamili kwa ajili ya mafunzo halisi ya sayansi kwa wanafunzi wetu wa Shule zote za Kata na Shule Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu *combination* na kwamba wanaokwenda kwenye Udaktari wanachukua *PCB* na *Mathematics* tu lakini wa *CBG* hawachukuliwi. Mradi wa *Chemistry* na *Biology,* mategemeo yangu ni kwamba, *TCU* wanawachagua hawa, lakini mahitaji haya pia yanaratibiwa na vyuo vyenyewe vinavyofundisha fani mbalimbali pamoja na hii mahususi ya Udaktari. Nitalichukua hilo kulifanyia uchunguzi na kama kuna upungufu tutashauriana na *TCU* ili waweke mambo ambayo yatawasaidia Vijana wetu waweze kupata mafunzo ya fani hii.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri anajibu alizungumzia kuhusu kujenga maabara katika Shule zetu za Kata na za Wananchi na hiyo michango ya maabara tunajua kabisa ni agizo la Mheshimiwa Rais kwamba kila Mwananchi achangie kujenga maabara.

Kwa kuwa kumekuwa na udhaifu mkubwa wa usomaji wa mapato na matumizi kwa Watendaji wetu kuhusu hii michango ya maabara na wananchi sasa wamekuwa wakikata tamaa kuchangia:-

Je, Serikali haioni sasa kuna sababu maalum ya kuanzisha ukaguzi mahususi wa hii michango hususan ya maabara katika kwa kila Kata ili wananchi waweze kuwa na moyo wa kuchangia na kujenga maabara za kisasa kama ambavyo Serikali inataka wajenge?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Kawambwa, kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa. Nataka niweke jambo moja vizuri hapa. Hii habari ya kujenga maabara katika nchi yetu kwa kila shule za sekondari nchini imekuwa na mafanikio makubwa sana. Nataka niliweke wazi hapa, ni habari ambayo

inatuondolea matatizo yote yanayoulizwa hata hili swali ambalo limeelekezwa hapa ambalo linazungumzia habari ya *combination* na nini litaondoka, maana tutakuwa na uhakika kwamba, wanafunzi wote wanapoenda katika shule hizi watasoma kwa vitendo na siyo kwa nadharia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukalijua hili jambo kama Taifa kwamba, nchi hii isingeweza kufika hapa kama siyo kuihusisha jamii yenyewe na kuishirikisha katika mpango mzima wa kuhakikisha wanachangia maendeleo yao. Hili ni jambo ambalo tumekuwa nalo la kujitegemea, tumelifanya na tumefika hatua nzuri ambayo ni ya kujivunia.

Watu wanaweza wakapinga jambo lolote kuhusu maabara zinazojengwa katika nchi hii na shule zinazojengwa katika nchi hii, lakini hawawezi kupinga jitihada zinazofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kuhakikisha tunafika katika hatua hii tuliyofikia hapa. *That is the bottom line,* hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Christowaja analeta jambo la msingi hapa, anazungumzia taarifa ya mapato na matumizi; hii taarifa ya mapato mna matumizi inatamkwa Kisheria. Katika *level* ya Kata wanatakiwa watoe na Mwenyekiti wa Kijiji pamoja Mtendaji wa Kijiji *they have got to pin it on the board* kuonyesha hela zilizotolewa kama mchango wa wananchi kwa ajili ya maabara ni kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu hili jambo analolizungumza ni la msingi tunalichukua. Hata kama anahitaji twende tukakague pia maeneo haya kwa maana mahususi kwa ajili ya maabara, *there is no problem,* uko utaratibu ndani ya Halmashauri wa ukaguzi wa ndani waufuate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya hili analolizungumza hapa, nichukue nafasi hii kuziagiza Halmashauri zote kwamba, zihakikishe tunakuwa na taarifa maalumu kuhusu michango yote inayotokana na wananchi kwa ajili ya kufanya jambo hili. *There is no problem* na wala hatuna tatizo na hilo kabisa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa tunakwenda swali linalofuata, linaelekezwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na linaulizwa na Mheshimiwa Mchungaji Natse; kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura!

Na. 221

**_SACCOS_ Kutokukidhi Malengo Yake ya Kuwanufaisha Wananchi Wake**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA (K.n.y. MCH. ISRAEL Y. NATSE)** aliuliza:-

SACCOS ni chombo kilichoundwa kwa lengo la kuleta ukombozi wa kiuchumi kwa watu wa hali ya chini lakini inasikitisha kuona kuwa *SACCOS* hizo hazikidhi malengo yake ya kuwanufaisha Wanachama wake kwa sababu mbalimbali kama vile ubadhirifu wa fedha, vitendo vinavyofanywa na Viongozi wa *SACCOS* hizo, ilhali kuna Maafisa Ushirika wanaopaswa kudhibiti hali hiyo. Ushiriki wa Viongozi wa Siasa wanaofanya zifanye vibaya na mfano mzuri ni *SACCOS* za Halmashauri ya Karatu za Ayalabe, Mbulumbulu na Karatu *SACCOS* ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania:-

(a) Je, ni nini nafasi ya Afisa Ushirika kama jicho la Serikali katika kuhakikisha kuwa *SACCOS* zinatimiza malengo yake?

(b) Serikali inatoa kauli gani kuhusu ushiriki wa Viongozi wa Kisiasa kwenye *SACCOS* ambao umekuwa ni tatizo kubwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Jimbo la Karatu, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Afisa Ushirika katika maendeleo ya Ushirika nchini yameainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002 na Sheria Namba Sita ya Mwaka 2013 ya Vyama Vya Ushirika. Majukumu hayo ni pamoja na kukagua na kusimamia uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, kutoa elimu kuhusu umuhimu wa Vyama vya Ushirika, majukumu ya Viongozi katika Vyama vya Ushirika, kubaini migogoro na malalamiko yanayojitokeza katika Vyama vya Ushirika na kutafuta ufumbuzi pamoja na kutoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya Kisheria na Kitaalamu kuhusu uendeshaji wa Vyama vya Ushirika nchini.

Utekelezaji wa majukumu hayo umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo uwepo Maafisa Ushirika wachache ukilinganisha na wingi wa Vyama vya Ushirika, ukosefu wa vitendea kazi vya kutosha na baadhi ya Maafisa Ushirika katika ngazi ya Mamlaka za Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kutotekeleza majukumu yao ya usimamizi wa maendeleo ya Vyama vya Ushirika inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za kuimarisha na kusimamia uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na maendeleo ya Ushirika kwa ujumla, Serikali imeunda Tume ya Maendeleo ya Ushirika na kuipa Mamlaka ya kusimamia moja kwa moja majukumu ya Maafisa Ushirika kuanzia ngazi za Taifa hadi ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kukabiliana na changamoto ya ushiriki wa Wanasiasa katika Uongozi wa Vyama vya Ushirika, Serikali kupitia Sheria Namba 6 ya Mwaka 2013 ya Vyama vya Ushirika, ambayo imeanza kutumika rasmi mwezi Januari 2014, imeainisha mambo mbalimbali ikiwemo kuzuia Viongozi wa Kisiasa na Watumishi wa Umma kuwa Viongozi katika Vyama hivi vya Ushirika. Hivyo, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Viongozi wa Kisiasa wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa pamoja na Watumishi wa Umma, hawaruhusiwi kuwa Viongozi katika Vyama vya Ushirika nchini.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshmiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imekiri katika majibu yake kwamba kuna upungufu wa Watumishi wa Vyama vya Ushirika katika Halmashauri mbalimbali na Sekretarieti za Mikoa; na kwa kuwa kuna upungufu wa vitendea kazi; je, Serikali iko tayari sasa kuiwezesha Tume ya Maendeleo ya Ushirika ili iweze kuajiri Maafisa Ushirika wa kutosha katika maeneo husika na kupata vitendea kazi?

(ii) Kwa kuwa Serikali ilipitisha Sheria Namba 6 ya Mwaka 2013 ya Vyama vya Ushirika; je, Serikali sasa imeshatunga Kanuni ambazo zitasaidia Sheria hii iweze kufanya kazi vizuri? Nakushukuru.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema na kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza, ni kweli changamoto kubwa ni kuwa Maafisa Ushirika wachache katika ngazi karibu zote pamoja na vitendea kazi. Ili kuuondoa Ushirika katika hali hiyo, ndiyo sababu tumeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika ili uhusike na Ushirika moja kwa moja. Huko nyuma Ushirika ulikuwa ni Idara chini ya Wizara ya Kilimo.

Kwa kuwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, maana msingi tunaipa nguvu yenyewe na imekuwa na fungu lake yenyewe kwa maana ya *Vote*. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulipokuwa tunapitisha Bajeti ya kilimo hapa, tuliomba pia pesa kwa ajili ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kama fungu peke yake linalojitegemea.

Moja ya mikakati yake sasa ni kuhakikisha inaajiri Mafisa Ushirika wengi zaidi, pamoja na kununua vitendea kazi hasa magari na pikipiki, kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa Ushirika hawa waweze kufanya kazi vizuri hasa kwenda kwenye ukaguzi wa Vyama hivi vya Ushirika nchini. Kwa hiyo, hilo tunalifanya sana Mheshimiwa Mbunge.

Suala la Kanuni; ziko hatua za mwisho na siyo muda mrefu sana Waziri atazitunga Kanuni hizo ili ziweze kutungwa na kwa maana hiyo kuweza kushughulikia uendeshaji na usimamizi wa Sheria yenyewe Namba 6 ya Mwaka 2013.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Maafisa hao wa Ushirika hawana vitendea kazi na katika Ofisi za Halmashauri huku hawana hata magari na hawana chochote. Cha kusikitisha, Maafisa hawa wanajikuta wanapangiwa kazi na Vyama vya Ushirika au *SACCOS* ambazo huwalipa posho na kama wewe unalipwa posho au marupurupu na mtu unayemsimamia anakuwa anakunyamazisha. Kwa hiyo, unakuta Maafisa hawa wanalazimika kutokana na hali hiyo kunyamaza na kuendeleza mambo ambayo Mheshimiwa Natse ameyasema katika swali lake la msingi.

Je, Serikali inachukua hatua gani pamoja kuanzisha Tume ya Ushirika kuhakikisha Maafisa hawa wanapata nyenzo na mambo mengine ambayo yanahusu ajira yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, haturuhusu kama Wizara na kama Tume, kwa maana ya Maafisa Ushirika wanapokwenda kulipwa posho na Vyama vya Ushirika kwa maana ya *SACCOS* na *AMCOS* au vyama vya aina nyingine. Ninavyosema pamoja na hali ngumu siyo kwamba, Idara za Ushirika katika Wilaya au Sekretarieti za Mikoa siyo kwamba zinakosa mafungu. Tatizo linalojitokeza ni ucheleweshaji wa pesa wakati mwingine.

Naomba nitumie fursa hii kuwaagiza Maafisa Ushirika Nchini kote kwamba, wanapaswa kwenda kufanya kazi bila visingizio vya kwamba hawana posho na kwa maana hiyo kulazimika kuzidai *SACCOS* na *AMCOS*. Niseme pia kwamba, Maafisa Ushirika au Idara ya Ushirika katika Halmashauri iko chini ya Mkurugenzi na kwa maana hiyo, Wakurugenzi pia wanapaswa kuhakikisha wanawawezesha Maafisa Ushirika hawa kwenda kwenye shughuli za kukagua na kuona Ushirika katika nchi unaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kutokuwa na vitendea kazi kwa maana kama Idara, isiwe visingizio vya kufanya Ushirika ushindwe kufanya kazi. Cha msingi tulichosema ni kwamba, Tume sasa hivi imejipanga vizuri ili ihakikishe Tume yenyewe inawezeshwa kwa maana ya kuajiri Maafisa Ushirika wengi na kununua vifaa vingine vya kutendea kazi kama magari na pikipiki kama nilivyokwisha kusema awali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaelekea swali linalofuata ambalo limeelekezwa Wizara ya Nishati na Madini na litaulizwa na Mheshimiwa Rita Kabati; kwa niaba yake Mheshimiwa Mangungu!

Na. 222

**Rasilimali ya Madini ya Chuma – Iringa – Njombe**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. RITA E. KABATI)** aliuliza:-

Mikoa ya Iringa na Njombe inafahamika kwa kuwepo hazina kubwa ya rasilimali ya madini ya chuma hususan eneo la Liganga Wilayani Ludewa:-

Je, Serikali imefikia wapi katika kuvuna rasilimali hii ya chuma ili kuendeleza viwanda vya chuma nchini na kuleta mabadiliko ya viwanda nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES M. KITWANGA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rita Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa madini ya chuma yamegunduliwa katika eneo la Liganga, Mkoani Njombe. Aidha, madini hayo yamegunduliwa pia katika maeneo ya Milima ya Uluguru Mkoani Morogoro na eneo la Itewe Mkoani Mbeya. Hata hivyo, hadi sasa eneo la Liganga ndiyo lina hazina kubwa ya madini ya chuma.

Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imeipatia Kampuni ya Tanzania - China I*nternational Mineral Resources Limited*, leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ya chuma katika eneo la Liganga. Leseni hiyo yenye Namba SML 533/2014, ilitolewa tarehe 9 Oktoba, 2014 na itafikia ukomo wake mwaka 2029. Kampuni hii ina ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Tanzania *(NDC),* inayomiliki asilimia 20 na Kampuni ya Sichuan Hongda Group kutoka China, ambayo inamiliki hisa asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni hii inaendelea na maandalizi ya kufungua mgodi wa chuma kwenye Leseni ya Liganga, sambamba na uanzishwaji wa kiwanda cha kutengeneza chuma, yaani *steel plant* hapo Liganga na mgodi wa makaa ya mawe katika eneo la Mchuchuma. Miradi hiyo ya Mchuchuma na Liganga, inategemeana sana na inatarajiwa itakapokamilika italeta manufaa makubwa kwa Taifa, kwa kutoa ajira kwa Watanzania wapatao 3,049, kuchangia mapato yatokanayo na mrabaha na kodi mbalimbali yanayokadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 114.4 na manufaa yasiyokuwa ya moja kwa moja, yaani *indirect benefits* yanayokadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 1,034. Uhai wa Mgodi wa Liganga unakadiriwa kuwa ni miaka 50 na Mchuhuma ni miaka 100.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ningependa nimuulize maswali kadhaa ya nyongeza.

(i) Miradi hii ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Sasa ni sababu zipi zinazopelekea Serikali kusuasua kwenye utekelezaji wa Miradi hii na kuchukua muda mrefu; wananchi wamekaa na matumaini kuona Miradi hii inaanza ili iweze kunufaisha na tupunguze gharama kubwa ya ununuzi wa chuma kutoka nje?

(ii) Miradi hii ya chuma ni chuma kingi ambacho kinahitaji kusafirishwa kwenda nje; kuna jitihada gani za Serikali kuboresha Bandari ya Mtwara, Bandari ya Kilwa pamoja na ujenzi wa reli kutoka Mtwara kwenda mpaka Mbababay ambapo itakwenda sambamba na Miradi hii:-

Serikali inachukua hatua gani za haraka kuhakikisha Miradi hii inakuwa na uwiano na inatoa matokeo chanya kwa wananchi wa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Njombe ambao tumekaa kwa muda mrefu tunataka Miradi hii ianze ili wananchi wetu waweze kunufaika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwaeleze Watanzania wote kwamba, Miradi hii haisuisui. Kama nilivyojibu katika swali la msingi, Miradi hii ni mikubwa na inachukua miaka 50 mpaka miaka 100. Kwa hiyo, Serikali ni lazima ichukue tahadhari ya kutosha, ijadiliane na wawekezaji hawa kuona Miradi hii katika miaka hiyo, inaleta manufaa chanya yanayotakiwa. Kwa hiyo, siyo suala la kusuasua, bali ni umakini wa Serikali kuhakikisha Miradi hii itakapotelezwa inakuwa na manufaa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa Bandari ya Kilwa, Mtwara na reli; niwahakikishie Wananchi wa Ruvuma, Lindi na Mtwara kwamba, mpaka sasa hivi Serikali imeshaanza utaratibu wa mchakato wa kuweka *tender* kuhakikisha tunaboresha Bandari ya Kilwa, Bandari ya Mtwara na kujenga reli ambayo itawanufaisha Wananchi katika maeneo hayo yote.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nitauliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa hapa nchini tuna Programu ya *PPP,* lakini Miradi kama hii inakuwa ni mikubwa mno na inahitaji *capital* kubwa vilevile; na kwa kuwa kuna nchi zimeonyesha hamu ya kuisaidia Tanzania kwa kuwakopesha fedha katika Miradi mbalimbali:-

Je, hatuoni kwamba Serikali sasa hivi ili kuendeleza hii Mipango ya *PPP* ifanye utaratibu wa kukopa fedha hizo kuingia ubia na makampuni hayo ambayo yanakuja kuwekeza katika utengenezaji au uchimbuaji wa chuma, badala ya kuwaachia wao peke yao na hasa siyo vibaya hata wananchi wakashirikishwa kununua hisa katika baadhi ya maeneo ya kutengeneza au kuchimba vyuma hivyo kama wanavyofanya nchi zingine kama vile India na Brazil?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa tuna Sheria ya *PPP,* ambayo inatuwezesha kushirikiana na hao wabia kuweza kuwekeza katika nchi yetu.

Kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, hapa ni ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na wawekezaji binafsi waliotoka China, ambao kwa pamoja wamekubaliana kukopa katika mabenki makubwa yenye uwezo wa kutoa mitaji mikubwa na sisi kwa pamoja tukashirikiana kupitia *NDC*.

Kwa Watanzania, *NDC* kwa sasa hivi ndiyo mwakilishi wetu, lakini bado haiondoi uwezekano au nafasi ya baadaye Mradi huu utakapokuwa umekamilika kuuweka katika Soko letu la Hisa na Watanzania wakashiriki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaenda swali linalofuata, linaelekezwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, litaulizwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma; na kwa niaba yake Mheshimiwa Amina!

Na. 223

**Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. RIZIKI OMAR JUMA)** aliuliza:-

Katika Mwaka wa Fedha 2012/2014 Serikali ilitenga shilingi 2,000,000,000/= kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na katika kipindi cha Julai – Desemba 2013 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi 515,628,846/= kutoka kwa Wizara ya Fedha:-

(a) Je, Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kuwa fedha hiyo inapatikana ili kuendeleza Wanawake kiuchumi?

(b) Je, Mikoa mingapi hadi sasa imefaidika na Mfuko huo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nianze kuwatakia Waislamu wote Tanzania, Ramadhani Kareem, Mwenyezi Mungu azikubali funga zetu na swaumu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na kwamba, katika kipindi cha Julai - Desemba, 2013, Wizara ilipokea kutoka Hazina, kiasi cha sh. 515,628,846/= tu.

Hata hivyo, mkakati wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ambapo kwa mwaka ujao wa fedha 2015/2016, kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kimetengwa. Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina kuhakikisha fedha zilizotengwa na kupitishwa na Bunge zinatolewa kama ilivyokusudiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara imenufaika na fedha za Mfuko huu. Aidha, Halmashauri mbalimbali katika Mikoa ilipatiwa fedha na Wizara kwa viwango tofauti, kwa kuzingatia maombi kutoka Halmashauri husika na urejeshaji wa fedha hizo kabla ya kupatiwa zingine. Mchanganuo wa kila Mkoa upo na kama Mheshimiwa Mbunge atauhitaji tutampatia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Abdallah Amour!

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, mchanganuo nataka nipatiwe.

Katika jibu lako la msingi Mheshimiwa Waziri umekiri kuwa, umepeleka milioni mia tano na kumi na tano badala ya bilioni mbili na hizi ulipeleka 2013 Desemba na unasema mwaka unaokuja utapeleka bilioni 1.5:-

(i) Je, huoni hii ni kuwadanganya Wanawake na hamna nia njema ya kuwasaidia?

(ii) Kwa kuwa lengo la hizi fedha ni kuwakopesha Wanawake ili waweze kufanya Miradi na badala yake waweze kuzirejesha hizo pesa na waweze kujiendeleza kimaisha. Kwa utoaji huu wa fedha usiokuwa na nidhamu; je, Mheshimiwa Waziri hao Wanawake wataweza kufikia malengo waliyokusudia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, kwa kuwa Msemaji wa Wanawake, kwa sababu ni Sera ya Chama cha Mapinduzi kwamba ukiwawezesha wanawake unaiwezesha jamii na familia kwa ujumla.

Dhamira ya dhati ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Amina kama umekuwa mfuatiliaji mzuri, utaona Mfuko huu ulianzishwa kwa Azimio la Bunge mwaka 1993. Utoaji wa fedha ukakoma kwenye mwaka 1998. Kwa hiyo, sasa hivi tumeanza kuweka fedha kila mwaka kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Amina niseme nakubaliana na wewe, bilioni 1.5 ambazo zimepangwa ni fedha kidogo, lakini kama tutafuatilia Azimio la Bunge linasemaje, vyanzo vya Mfuko huu mojawapo ni mapato ya ndani ya Halmashauri husika. Sisi sote ni Madiwani katika Halmashauri zetu. Nikiichukua hiyo bilioni 1.5 nikiigawa kwa Halmashauri 168, tunapata milioni 8.9, ni kweli hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukazibane Halmashauri zetu kuhakikisha zinatenga asilimia tano kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, hapo tutaweza kupata fedha za kutosha ili kuwawezesha Wanawake kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali na shughuli mbalimbali za biashara.

Nitoe mfano; kwa mfano, Halmashauri tu ya Ilala mapato ya ndani ni zaidi ya bilioni 26. Wakisema ni 5% wana uwezo wa kutenga *one point something billion* kwa ajili ya Wanawake. Wanawake wangapi Ilala watakuwa wamepata hizo pesa? Kwa hiyo, niseme hakuna danganya toto, Serikali inayo dhamira ya dhati ya kuhakikisha tunatenga fedha kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na sisi Waheshimiwa Wabunge tuzibane Halmashauri zetu kuhakikisha zinatenga fedha.

Suala la pili, utoaji wa fedha hauridhishi. Unaridhisha ukiangalia na mtiririko wa fedha huko nyuma kama nilivyojibu awali. Muhimu sisi wote ni Wabunge na tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii mwezi huu, kwa hiyo, tuendelee kuhakikisha Serikali sasa inatoa hizo fedha 1.5 bilioni kama zilivyobajetiwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli swali la nyongeza!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami pia natumia fursa hii kuwatakia Waislamu wote Ramadhani njema na *Inshallah* kwa uwezo wa *Allah* awafanyie wepesi katika funga zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akisema kwamba, ukiangalia kwa mfano mapato ya ndani kama ya Ilala, wanaweza kutenga takribani hata bilioni moja kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni utaratibu unaotumika kutoa mikopo kwenye ule Mfuko. Unawavunja moyo hata Halmashauri kutenga, kwa sababu masharti yake yanafanya watu wapewe zile pesa kama pipi, utaratibu wake hauwabani watu katika kurudisha na nishasema katika Bunge hili mara nyingi.

Je, ni lini Serikali itabadilisha ule utaratibu ili uwatie moyo Halmashauri kuweza kutenga zile pesa kwa sababu hazirudi kutokana na mfumo wake upo hafifu; lini wataboresha ule utaratibu aua zile sheria ili pesa zirudi kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru sana wajina wangu Ummykuruthum kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi hela ambazo tumebajeti kwa mwaka ujao wa fedha wa 2015/2016, moja ya kazi itakayofanywa ni kufanya tathmini ya Mfuko. Tunakubali kwamba, ipo changamoto katika suala la ufuatiliaji wa Mfuko. Kwa hiyo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, imejipanga kufanya tathmini ya Mfuko ili kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha wanaopata hizo fedha basi wanazitumia kwa shughuli husika walizoombea, lakini pia ili waweze kurejesha.

Lengo letu tunaogopa kuweka masharti magumu sana, watu wasione tofauti ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na kwenda kufuata mkopo benki. Kwa hiyo, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba, masharti ya kupata fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake yanabaki kuwa masharti nafuu kuliko masharti mengine ambayo yanapatikana katika Mabenki na Taasisi nyingine za fedha.

Ninakuthibitishia kuwa suala lako linafanyiwa kazi, endapo fedha zitapatikana basi tathmini ya Mfuko itafanywa na kuboresha masuala ya utoaji fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam nimekuona!

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niwatakie funga njema Waislamu wenye nia safi na wasiokuwa wanafiki. Mwenyezi Mungu azitakabali funga zenu na *Inshallah* apokee saumu zenu, kwa sote amina.

Swali langu la nyongeza nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri. Nakuuliza nikiwa Mbunge makini na ninafanya upembuzi kwa kitu ambacho nauliza humu Bungeni nachambua, sikurupuki, nina akili timamu na pia nimesoma. Kwa hiyo, natambua ninachokisema, naomba nikuulize swali dogo la nyongeza. Huu ni mwezi wa toba.

Kwa kuwa Wizara hii inasimamia Watoto, Wanawake na hata Wanaume, ni ya jinsia, ndiyo maana tukasema jinsia. Kama Mifuko hii ina ma; kwa mfano, Mkoa wa Njombe pale kuna

watoto wadogo sana na akina mama wanafanya biashara ndogondogo hawaendi shule? Sasa kama akinamama wale wangekuwa wamenufaika wangepeleka wale watoto shule?

Naomba majibu ya Serikali ya uhakika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam, hilo ni swali jipya. Unataka idadi ya wanawake waliopata mkopo, atatoa wapi hizo takwimu sasa hivi! Hilo ni jipya kabisa.

Mheshimiwa Ester Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwa kuwa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Kuruthum anajibu maswali yetu hapa ameeleza kwa mwaka 2013/2014 tulipitisha bajeti ya bilioni mbili kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake lakini wakapeleka milioni mia tano. Akaenda zaidi na kusema, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ilikuwa ni bilioni moja na nusu nafikiri.

Swali langu la msingi; alisisitiza kwamba Halmashauri wanakusanya fedha nyingi kana kwamba tuwabane Halmashauri waweze kutoa fedha nyingi kwenda kwenye Mfuko wa Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, Serikali Kuu ilitakiwa iwe ni kioo cha kuona kwamba kinaweka umuhimu wa wanawake kunufaika.

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye swali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali, najenga hoja.

Serikali Kuu mlitakiwa mwonyeshe kioo kwamba kuna umuhimu wa kutenga Mfuko wa Wanawake, tumepitisha bilioni mbili mmepeleka milioni mia tano; itakuwaje Halmashauri wataweka uzito kwa wanawake kama Serikali Kuu hamjaonyesha kwamba kuna umuhimu huo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba turudi katika Azimio la Bunge lilioanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake; umeweka wazi vyanzo vya fedha za Mfuko huu ni pamoja na mapato ya Serikali Kuu, ambayo mapato ya Serikali Kuu ni kichocheo tu; yaani ni kama kwa ajili ya kuzichochea Halmashauri kuweza kubajeti kupanga. Fedha nyingi zipo katika Halmashauri zetu Mheshimiwa Esther. Tulikubali tulipanga bilioni mbili, lakini kutokana na hali ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali hatukuweza kupeleka hizo fedha kwa ajili ya Mfuko.

Nikupe mfano, kama kweli tuna nia ya dhati ya kuhakikisha Wanawake wanapata fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Halmashauri ya Tarime mapato yao ni karibu bilioni 2.1. Asilimia tano ya shilingi bilioni 2.1 ina maana wanatakiwa watenge angalau milioni mia moja. Mheshimiwa Esther kanisaidie niambie Halmashauri ya Tarime imetenga bilioni ngapi na wewe ni Mbunge makini. Kwa hiyo, haya mambo tuyarudishe katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilithibitishie Bunge lako Tukufu, nimeongea na Mheshimiwa Mwanri sasa hivi; Serikali imeamua kwamba, sasa hivi itaweka adhabu kwa kila Mkurugenzi

ambaye hatatenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, atakatwa tozo katika mshahara wake.

Mkakati wa pili wa Serikali ni kwamba, Mkurugenzi ameambiwa tangu Mfuko umeanzishwa na mapato yale ukitazama Taarifa ya *CAG,* inaonyesha Halmashauri hii makusanyo yake ya ndani ni kiasi gani. Wanatakiwa wawe na mkakati wa kurejesha kuanzia Mfuko ulipoanzishwa mpaka mwaka huu.

Kwa hiyo, naomba tusimamie suala hili ili tuhakikishe kweli wanawake wanapata fedha, kwa ajili ya kufanya shughuli za uzalishaji mali na biashara. Wote tunaamini na mimi ni muumini wa kweli wa kwamba ukimwezesha mwanamke umemwezesha baba, umemwezesha mtoto na umeiwezesha jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wabunge Wanawake ni Wajumbe kwenye hizo Kamati za Mikopo.

Mheshimiwa Kawawa!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema Halmashauri zetu ziwe zinatenga fedha hizi na kweli zinatenga, lakini Halmashauri mapato yake yanatofautiana. Ametoa mfano wa Ilala wa bilioni 27, sisi Halmashauri yetu ya Namtumbo mapato yake ni ya chini. Tunaweza tukatenga labda zikafika milioni mia moja, lakini wanawake zinaweza zisiwatoshe.

Je, Serikali inaweza kuweka utaratibu wa kwamba, Halmashauri zile zenye mapato kidogo basi zipewe fedha za kutosha katika Mfuko huu, halafu Halmashauri zenye pesa nyingi zisimamiwe mapato yake ya ndani ndiyo zitoe fedha hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba, ushauri anaoutoa Mheshimiwa Vita Kawawa ni wazo zuri, kwa sababu kama tulivyosema, fedha ambazo zinatoka Serikalini ni kati ya shilingi milioni nane mpaka milioni kumi na mbili. Sasa kama Halmashauri ya Ilala ambayo ina makusanyo ya ndani ya bilioni 26 unampelekea milioni nane, milioni kumi na mbili, inawezekana wasione *impact*. Kwa hiyo, ni wazo zuri na sisi tunakubali tutalifanyia kazi, kwa sababu Halmashauri ya Namtumbo mapato yao yanaenda kwenye milioni 645 hivi, kwa hiyo, wakiweka asilimia tano ni kama milioni 32.

Kwa hiyo, ni wazo zuri tunalichukua, tunalipokea na tutalifanyia kazi, zile Halmashauri ambazo hazina mapato makubwa, basi hizo ziangaliwe ziweze kupata fedha moja kwa moja kutoka Serikali Kuu, kutoka Wizara na zile ambazo zina fedha basi zisimamiwe kuhakikisha fedha hizo zinatoka na wanawake wanakopeshwa. Kigezo kimoja kikubwa Mheshimiwa Vita ni kwamba, jinsi ulivyochukua zile fedha na utakavyorudisha basi ndivyo utakavyoweza kupewa, lakini wazo lako ni zuri na tunalipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Sasa naomba niwatambue wageni waliopo hapa Bungeni asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wafuatao:-

Wapo wageni 77 wa Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambao ni akina mama wajasiriamali, wanaotoka kikundi kiitwacho *Daughters of* Maria Immaculata, kilichopo Jijini Dar-es-Salaam. Kikundi hicho kinaongozwa na Ma-sister watatu ambao ni Sister Teresi, Sister Liks na Sister Selvi; karibuni sana.

Naombeni na wanakikundi wote wasimame. Tunawapongeza kwa kazi nzuri mnazozifanya, karibuni sana hapa Bungeni. Tunawapongeza kwa shughuli za ujiasiriamali. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), ambao ni Mzee Abel Njalika - Mwenyekiti Mstaafu wa Kijiji cha Materereka; naomba asimame Mwenyekiti wa Kijiji Mstaafu; karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wa pili ni Timoth Ngerangera - Afisa Tawala *Capital Teachers College*; karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa - Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kutoka Iringa, wakiongozwa na Ndugu Elimo Mponzi - Mwenyekiti wa Kijiji cha Nandala Wilaya ya Mufindi; karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Albert James Mntangi kutoka Tarafa ya Amani Wilaya ya Muheza eneo la Derema, wakiongozwa na Mheshimiwa John Kiko - Diwani wa Kata ya Zirai. Mheshimiwa Diwani karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Felister Bura, ambao ni wanafunzi 40 na Walimu wawili kutoka Shule ya Tumaini *English Medium* (Nkuhungu), wakiongozwa na Mwalimu Diseko. Karibuni sana, someni kwa bidii, nafasi hizi zipo hapa kwa ajili yenu. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni Wanafunzi 70 na Walimu 4 kutoka Shule ya Msingi ya Martin Luther Dodoma. Wanafunzi na Walimu msimame; karibuni sana, someni kwa bidii na Walimu tunawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya. *(Makofi)*

Wanafunzi 15 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM);* karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi watano na Walimu wawili kutoka Shule ya Msingi Magereza Moshi. Wanafunzi hawa ni wale waliofanya vizuri katika mitihani yao ya muhula wa kwanza katika shule hiyo. Hao Wanafunzi watano na Walimu wawili kutoka Shule ya Magereza Moshi wasimame; hongereni sana. Wanafunzi hawa wamefanya vizuri tuwapigie makofi tuwapongeze. *(Makofi)*

Wanafunzi 60 ambao ni Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; hawapo nafikiri wamekosa nafasi.

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Anna Abdallah - Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuwa, leo saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo, katika Ukumbi Namba 229, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Katibu, hatua inayofuata!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria ya Masoko ya Bidhaa wa Mwaka 2015
*(The Commodity Exchanges Bill, 2015);*

*na*

Muswada wa Sheria ya Kuwalinda watoa taarifa za Uhalifu na Mashahidi wa Mwaka 2015
*(The Whistleblower and Witness Protection Bill, 2015)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa asubuhi hii mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Chiku Abwao wajiandae.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, dakika 15.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo kwenye bajeti ya Serikali ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nijikite sana kwenye suala la makusanyo na matumizi ya Serikali. Imekuwa ni kawaida kwa miaka yote kwamba makusanyo yetu yameendelea kuwa madogo kuanzia kwenye Serikali Kuu mpaka kwenye Serikali za Mitaa lakini wakati huohuo matumizi yetu yameendelea kuwa makubwa sana ukitofautisha na kile ambacho tunakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tu kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kwa mwaka 2014/2015, wamekadiria tukusanye asilimia 12.3 ya pato la Taifa kama kodi lakini ukiangalia matumizi ni zaidi ya asilimia 20 ya pato la Serikali, hayo ni matumizi ya Serikali tu. Kutegemea na vyanzo vya mapato ambavyo tunavyo na kweli nchi yetu ina neema, ina baraka, lakini bado maeneo mengi hatujaweza kukusanya, bado bajeti yetu kwa kiasi kikubwa inaendelea kutegemea fedha za ufadhili, fedha za mikopo ya riba nafuu, fedha za misaada na mambo kama hayo, kwa upande wa makusanyo bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kuna mambo yale ambayo tunayazungumzia miaka yote kuhusiana na jinsi gani ya kuweza kukusanya mapato makubwa. Kwa mfano, bahari kuu haijaguswa kabisa. Bahari kuu imekuwa ni shamba la bibi miaka yote. Tumekuwa tunasema kwamba tuanzishe bandari ya samaki, tuweze kuhakikisha kwamba samaki wanaovunwa wanalipiwa kodi, wale samaki hawalishwi chakula, hawatunzwi ni kwenda kuvua na kwenda kuuza na kuingiza kipato, Serikali miaka yote imeshindwa kusimamia. Hata bajeti ya mwaka huu hawajazungumzia chochote kuhusiana na suala la bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa tuna maeneo mengi, kwa mfano pale *TRA*, hakuna maeneo ambayo tunaibiwa kama bandarini, tunaibiwa kweli kweli. Wafanyabiashara wengi wakubwa hawalipi kodi stahiki na hili lingekuwa ni pato la taifa, ingekuwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali na miradi ya maendeleo, wengi hawalipi kodi. Nilisema tena hapa Bungeni na leo narudia, makontena mengi yanayotoka bandarini hayalipiwi kodi stahiki zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyabiashara mkiwasikiliza vizuri ni kwa sababu tu Serikali huwa haipendi kukaa na kuongea nao, hata Mwenyekiti wa Wafanyabiashara aliongea nilimsikia kwenye *media*, kontena moja la shilingi milioni arobaini, wanatoa shilingi milioni arobaini wanaandikiwa risiti ya shilingi milioni kumi, kontena moja watu wanapiga shilingi milioni 30. Kama umetoa makontena kumi kwa siku ni shilingi milioni ngapi za Serikali zimetafunwa, mbona hamfuatilii huku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoshangaza mnakwenda kuongeza kodi kwenye *diesel*, *petrol* na mafuta ya taa. Kwa taarifa ya Serikali, leo ni wiki moja tangu Mheshimiwa Waziri ametamka kuhusiana na kuongeza kodi ya mafuta, wala hatujafika kuongeza tayari maisha yameshapanda kule, vitu vimeshapanda madukani, mafuta ya vyakula yameanza kupanda, yalikuwa shilingi elfu kumi na tano leo ni shilingi elfu kumi na sita. Tayari nauli za barabarani zitaanza kupanda, unapopandisha mafuta ujue *automatic* umepandisha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie tu Watanzania kwamba bajeti hii ni ya kufunga mikanda kweli kweli. Kiukweli itawabana kwa sababu kila kitu kitapanda, kutakuwepo na kupanda kwa vyakula madukani, nauli, nguo kwa sababu *impact* kubwa anakwenda kuipata yule mlaji ambaye ni maskini Mtanzania wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kwamba kodi iliyoongezwa kwenye mafuta iende kwenye *REA*, nakubaliana, lakini mbona maeneo makubwa ya kuchukua fedha nyingi mnashindwa kusimamia, mnakwenda kubana wale wadogo kabisa ambaye anataka ajisaidie angalau kuwasha tu taa ndani anashindwa. Maeneo makubwa ambayo mngeweza kuchukua fedha yingi tena kwa mafungu mnashindwa kusimamia, lipo tatizo kubwa sana kwenye makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, nimeona bajeti ya Mheshimiwa Waziri ameweka vipengele kama sita vya kuhakikisha kwamba wanabana Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa waweze kukusanya mapato, lakini bado miaka yote ukifuatilia, wanasema kwamba tutahakikisha kwamba tunaongea na mawakala wa Serikali za Mitaa, tuweke vitabu ambavyo Serikali itafuatilia, ukija kwenye ripoti ya *CAG* vitabu vingi havikaguliwi, vingi wanaburuza wanatoa vya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, ukiangalia miaka yote kile kinachozungumziwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri siyo hicho ambacho kinatekelezwa na ndiyo maana muda wote bajeti yetu ya ndani makusanyo hayaongezeki, lipo tatizo kubwa sana. Kiukweli kwenda kuwabana Watanzania kushindwa kutumia mafuta ya taa, *diesel*, nauli, vyakula kila kitu ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ijue wanapokwenda kuongeza kodi kwenye mafuta ya taa kutakuwa na uharibifu wa mazingira. Tunajua kabisa kwamba Tanzania tuna tatizo kubwa la *climate change* na ni dunia nzima, lakini nchi yetu imekuwa na tatizo kubwa kwa sababu hatuna uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, tunakwenda kuzidi kuaharibu mazingira. Hata yule ambaye alikuwa anachemsha chai kwa kutumia mafuta ya taa lita moja hawezi tena atakwenda kwenye mkaa, tutaongeza matumizi ya mkaa, gesi haishikiki, mafuta ya taa hayashikiki, umeme kupikia hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe huwezi kupikia umeme ni gharama kubwa, matokeo yake nchi hii itakuwa jangwa. Hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni matumizi ya Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa na mimi namtaka wakati wa ku-*wind up* bajeti atusaidie, alisema atapunguza matumizi makubwa ya Serikali na ataanzia na vyombo vya usafiri kwa maana ya magari. Alitamka kwenye Bunge hili mwaka 2009, akasema magari yote ya kifahari yataondolewa kwenye Wizara mbalimbali, watumie magari madogo kama nchi za wenzetu. Mpaka leo ni miaka saba bado Mawaziri wote wanatumia *VX*, Wakurugenzi *VX*, Wakuu wa Wilaya *VX*, tunapunguzaje matumizi wakati bado vitu ni vilevile? Kwa nini hatusemi halafu tukatekeleza? Mbona tumekuwa ni watu wa maneno? Hili ni tatizo! Ukiangalia hata bajeti ya maendeleo nyingi utakuta ni kwenye vikao, semina, haziendi kule kumsaidia mlengwa. Hili ni tatizo kubwa sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la kushuka kwa shilingi ya Tanzania. Imekuwa ni shida, ni tatizo kwelikweli na inatia uchungu kwamba sisi tumeshindwa kulinda shilingi yetu inaporomoka kila siku, eti kwa sababu uchumi wa Ulaya umekuwa mkubwa, hivi ni kweli? Kwa nini Serikali inaruhusu na nasema tena, kwa nini tumeshindwa kudhibiti matumizi ya dola ndani ya nchi yetu? Kwa nini tunaruhusu dola kuwa mikononi kwa watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Kariakoo huhitaji kwenda *Bureau*, wafanyabiashara wanazo fedha unabadilishiwa mikononi, Serikali haipati kodi hata shilingi moja. Nchi za wenzetu ukibadilisha hata kama ni dola moja *you have to pay,* wanalipia kodi, sisi hatuna utaratibu huo? Kwa nini tunaruhusu mambo kama hayo? Pia nyumba za kupanga wanalipa kwa dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo zao la tumbaku wakulima wale maskini wananunuliwa kwa dola, hawajui dola. Mimi namshangaa sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, alinijibu juzi, kwa kweli nilisikitika kwamba eti inawezekana wakulima wananufaika na dola. Hivi kweli hatujui uwezo wa wananchi wetu, wanajua dola? Mimi leo hapa ukiniuliza dola kama sijaenda *bureau* ama benki sijui, kwa hiyo, hata ile *fluctuation* hatufuatilii, matokeo yake tumethamini hela ya Ulaya kuliko shilingi yetu. Fedha inaporomoka kila siku, maisha yanazidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la kuuza kidogo na kununua zaidi kutoka nje. Sioni kwenye bajeti ya Waziri ni namna gani kama Serikali tumejipanga kuweza kuuza sana nje ili tuweze kudhibiti fedha yetu ya ndani, hakuna lakini viwanda tunajua vyote karibia vimekufa. Miaka ya nyuma tulikuwa na mazao ambayo ndiyo yalikuwa yanasaidia sana kuinua uchumi, yale mazao yote leo, kahawa leo hakuna imepotea, imebaki tumbaku ambayo Serikali nayo haiiangalii, tulikuwa na *cocoa* hakuna, tulikuwa na katani hakuna, tulikuwa na pamba inazidi

kufa. Tunawezaje kuhakikisha tunauza nje wakati hata yale mazao ambayo yalikuwa yanaingiza fedha ya kigeni tumeyaacha yamekufa na hakuna utaratibu wowote wa kuyainua? Hili ni tatizo, mkulima anawezaje kunyanyuka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba Serikali ilisema hapa Bunge hili na Waziri Mkuu alisema miaka karibu mitatu au minne iliyopita kwamba tutahakikisha Serikali nzima kuanzia Serikali za Kuu mpaka Serikali za Mitaa wananunua *furniture* za maofisi kwa kutumia rasilimali ya ndani ya nchi yetu. Tunao vijana wenye uwezo, hawana ajira wapo mitaani, hawana kazi, tunazo mbao nzuri badala ya kuuza mbao magogo vijana tuwajengee uwezo watengeneze samani, ofisi zote zitumie samani za ndani ya nchi yetu lakini pia tuwe na uwezo wa ku-*export* tuuze nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Leo tunauza magogo, mbao ambayo ni nzuri, mbao ambayo ina thamani kubwa, tunapeleka mbao kwa Wachina, tunapeleka ajira kwa wenzetu, vijana wetu wapo mitaani, wanavuta bangi, wanauza unga, hawana kazi, tunashindwa kutengeneza ajira ndani tunapeleka ajira nje. Leo ni mwaka wa sita kwa nini Serikali bado inaendelea kutumia samani kutoka China, niulize swali na mtujibu hapa! Tunataka mtujibu kwa nini mnashindwa kusimamia hilo, kwa nini mbao zetu zinakwenda nje bado, kwa nini vijana wetu wanazurura hawana kazi ninyi mnanunua bidhaa huko nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, hili na lenyewe pia linachangia shilingi yetu kuendelea kuporomoka lakini pia tumechoka kuwa soko na kutengeneza ajira kwa wenzetu, haiwezekani! Sisi ni watu wa kutengenezea wenzetu tu. Hata *toothpick, it is shame*! Kijiti cha meno tuna *import* hivi tuna akili timamu kichwani jamani! Hata pamba *stick,* tunalima pamba Tanzania, pamba *stick* kwa ajili ya masikio tuna *import,* hivi hiyo ni akili? Leo nchi hii imekuwa kazi ni kuingiza kila kitu visivyofaa na vinavyofaa, sisi hatuna uwezo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli vijana wa pale Mufindi mkiwajengea uwezo tena kwa kutumia mbao ambazo hazina thamani hawatengenezi *stick*? Nadhani Serikali ina haja ya kuangalia haya mambo inasikitisha sana. Kwa mwendo huu kwa kweli shilingi yetu itaendelea kudorora sana kabisa. Ni lazima kuwepo na udhibiti wa *bureau de change*, udhibiti wa shilingi yetu, tuweze kuwa na mikakati mizuri na mipango ya kuweza kuhakikisha kwamba tuna-*export products* za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kusema hapa, leo hii tuna-*export* bidhaa za wanyama, tuna-*export* ngozi ghafi, tukasema kwa kutegemea wanafunzi wa sekondari peke yake hujagusa *primary* wala vyuo, tukatengeneza viatu vya sekondari zote Tanzania nzima, *it is a lot of money*! Leo nenda Kariakoo, tunaenda kuchukua viatu vya Kichina havina *quality*, ni bomu, siku mbili vimeisha, lakini *we are using a lot of money*. Kwa nini tunashindwa na ngozi tunazo, ng'ombe tunazo, wakulima wa mifugo wanahangaika hawana sehemu ya kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ni madogo lakini sijui kwa nini tunashindwa kuchukua hatua. Tunao wataalam ndani ya nchi hii, wamesoma kwa hela za walipa kodi, kwa nini tusiwatumie kuweza kuja na mbinu na mawazo ya kuweza kusaidia Taifa hili? Kwa kweli inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la watu kulipa kodi. Asilimia kubwa ya Watanzania hatulipi kodi hiyo ni wazi. Wanalipa wale ambao wapo kwenye nfumo maalum au mfumo rasmi, wengine wengi hawalipi kodi. Takwimu zinaonesha Tanzania tunatakiwa watu milioni kumi na tano walipe kodi, leo tunalipa watu milioni mbili na *point something* ni kidogo

sana, wengi hawalipi kodi lakini wengi wanatumia. Sasa kama Serikali ni lazima ikae chini ijiulize ni kwa nini watu wengi hawalipi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo pia tatizo la Watanzania kujengewa mfumo wa kulipa kodi kwa hiari, kuondokana na suala la watu kukwepa kulipa kodi. Watu wengi wapo radhi watoe rushwa ya shilingi elfu kumi kuliko alipe kodi ya shilingi elfu ishirini, hilo ni tatizo. Ukienda leo barabarani, tumeweka faini kule barabarani, dereva yupo radhi ampe *traffic* shilingi elfu tano kuliko alipe elfu thelathini ambayo ni kodi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hatujawajengea uwezo wa kujua kwa nini walipe kodi. Ili mtu umjengee uwezo na ufahamu ni lazima aone faida za kodi. Watu wengi hawalipi kodi kwa sababu hawaoni faida ya kodi. Leo mtu unakuta analipa kodi ukiangalia nje ya biashara kuna dimbwi la maji machafu, yupo pale miezi miwili, wafanyabiashara hawafiki pale, kwa sababu tu Serikali imeshindwa kuangalia kuna mtaro mchafu, kuna maji machafu yametitirika pale, yapo masuala madogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali ni lazima ikae chini, ifundishe na kutoa elimu, Watanzania waweze kulipa kodi kwa hiari. Mtu ajisikie ufahari aseme kwamba nikilipa kodi yangu inafanya kazi fulani. Nikiona maji ni kodi, nikiona barabara ni kodi, elimu nzuri ya mtoto ni kodi, kitu hicho hatuna! Naiomba sana Serikali, tunao wafanyabiashara na wapo tayari kulipa lakini waone faida za kodi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa sababu ya muda, tumepata bahati ya kuwa na migodi mingi ya madini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umeisha, ahsante sana. Naomba sasa nimuite Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Kombo na Mheshimiwa Chiku Abwao wajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu ni mchango wangu wa mwisho katika Bunge la Bajeti, kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunipa fursa. Pia nishukuru Chama changu kwa kunipa fursa, kwa kunijenga na naamini kabisa Watanzania ni mashahidi, Ester Bulaya wa 2011 siyo Ester Bulaya wa 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine pia niwashukuru Wabunge wote bila kujali vyama, tumeishi kama ndugu, tumeshirikiana, tumesimama pamoja katika mambo yanayohusu Taifa letu. Pia nimshukuru baba na mama yangu kwa malezi waliyonipa na kwa kuniongoza vema katika kipindi chote kigumu cha utumishi wangu wa Ubunge. Pia nimshukuru dada yangu mpenzi, Jane Kashilillah na mume wake kwa msaada mkubwa walionipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru mtoto wangu, rafiki yangu wa karibu Brighton, amekuwa akikosa mapenzi ya mama pindi ambapo nakuwa katika shughuli zangu. Najua sasa hivi anajiandaa kufanya mtihani wa kiroho kwa ajili ya kupokea *communion* ya kwanza, namtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwashukuru wanawake, vijana na wazee wa Mkoa wa Mara kwa kunilea vizuri na kunipa ushirikiano. Kipekee zaidi nawashukuru wazee na wananchi wa Bunda kwa ushirikiano wenu mkubwa, kwa maombi yenu, najua kulikuwa kuna tetesi kwamba Ester Bulaya ame-*paralyse*. Nawaambia niko mzima, nimepona, maombi yenu yanasaidia na Mungu atanijalia nitasimama kugombea Jimbo la Bunda. Nawashukuru sana, simu zilikuwa nyingi, nilikuwa naumwa lakini nimepona na kwa maombi yenu yatasaidia Mungu anasimama kwa mtu aliye mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze katika mchango wangu. Kwanza kabisa nianze na vilivyonifurahisha. Kwa siku zote tumekuwa tukizungumzia kuongeza kodi katika vinywaji; hili na mimi nampongeza Waziri kwa kuondokana na mtindo ule. Maana wengi tulisema hivi Watanzania wakiokoka hakutakuwa na shughuli zozote ambazo zinaendelea? Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Saada nakupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine nimefurahishwa na kuweka tozo kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya reli. Tuna imani kwamba tusipokuwa na reli hata shughuli nyingi za kiuzalishaji hatutaweza kuzifanya, hilo nakupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na mimi nipende kuzungumzia masuala mawili au matatu. Kwanza Mheshimiwa Saada nimesema sina tatizo na wewe ila *sometimes* nina tatizo na *commitment* ya Wizara yako. Ukija kujibu naomba uniambie ile ahadi mliyowaahidi vijana wa Tanzania ya kutafuta chanzo kwa ajili ya kuhakikisha fedha za vijana zinawekewa uzio ziko wapi? Napongeza jitihada za kuongeza kiwango cha pensheni za wazee, hawa 65% ya Taifa hili mmeji-*commit* katika Bunge hili mtawatafutia chanzo, kiko wapi? Kama mwakilishi wao na kama Mbunge yeyote makini lazima ahoji jambo ambalo wananchi wake au watu anaowawakilisha halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya vijana wa Taifa hili yamekuwa mengi, vijana wanakumbwa na dimbwi la umaskini, mbali ya kwamba umaskini unawakumba Watanzania wote, mmeahidi mtatafuta chanzo, kiko wapi? Lazima tuhoji mambo haya, hatuwezi kuja tukaunga mkono vitu wakati kuna mambo ya msingi, Watanzania walio wengi mambo yao yanaenda ndivyo sivyo! Hilo pia nitaomba unijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamezungumzia kuhusiana na matumizi ya dola kiholela. Jambo la matumizi ya dola limeanza kuzungumziwa tangu na sisi tukiwa nje tunaangalia Bunge kwenye *TV,* Bunge la Tisa. Badala ya kupungua matumizi ya dola yanaendelea kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda katika shule, kwenye hoteli, yaani sasa hivi Mtanzania anajivunia kuwa na dola kuliko kuwa na sarafu ya Tanzania, hili si jambo zuri, si ishara nzuri! Moja ya vigezo vya uzalendo ni kujivunia pesa yetu. Tunaweza tukaona ni *fashion* kuendelea na matumizi ya dola lakini si jambo zuri. Wote tunasafiri yaani hata Uganda ambao hela yetu iko juu kuliko yao wanasisitiza matumizi nya pesa yao ya ndani, siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie kupanda kwa dola. Leo hii akina mama wajane ambao wamejikongoja kwa mitaji yao, wafanyabiashara wale Kariakoo walivyokuwa wakienda China wakiwa na dola 10,000 walikuwa wanapata mzigo mkubwa, leo hii wale wamama wanataabika. Sasa hawa wafanyabiashara wetu tunawalinda vipi kwa dola kupanda namna hii? Sasa hivi *bureau* zipo kama Wamachinga tu, hakuna *control!* Unatembea hatua moja, mbili, tatu, unakuta *bureau,* mmeona wapi hii? Yaani nchi yetu sisi ni shamba la bibi

kwamba haina mwenyewe, haiwezekani! Lazima tuhakikishe tunadhibiti matumizi ya dola kupita kiasi, tuhakikishe tuna mikakati ya kufanya fedha yetu inaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati haya yanaendelea uchumi wetu umeshuka, uchumi wetu hauko *stable*. Wakati uchumi hauko *stable* tunafanya *mistake* ya kwenda kuongeza tozo ya mafuta. Jamani Waheshimiwa Wabunge, mimi ni miongoni mwa watu ambao napenda fedha ziende *REA* na ni jambo zuri sana Mheshimiwa Waziri lakini tulipoongezea sipo. Leo hii tutasema umeme ndiyo upo vijijini kwenye *centre* lakini siyo wote wanaoweza kununua hizo taa za mchina, bado kuna maeneo mengine wanatumia taa hizi za chemli zinazohitaji mafuta ya taa, hatuwezi kujidanganya, lipo! Hata mijini bado wanatumia sio kila mtu ana uwezo wa kununua gesi ambayo sasa hivi imepanda kutoka Sh.60,000 mpaka Sh.70,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni ni zuri lakini mlipoongezea sipo. Wakati uchumi haupo *stable,* dola imepanda, maisha magumu kwa Watanzania, bado tunaenda kuongeza tozo kwenye eneo ambalo litaibua mfumuko wa bei. Tumeshuhudia hata miaka iliyopita fedha inavyoongezwa wenye sheli wanagoma, nauli zinapanda, kila kitu kinapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dasa hili lazima liangaliwe wakati tunaongeza hapa bado Watanzania huko wanalalamika kwamba wanaponunua *LUKU* kuna hela inakatwa inaenda *REA*. Tunajua kama fedha zote za *REA* zingepelekwa mwaka jana, tusingekuwa na sababu ya kuongeza tozo bila sababu, hazikwenda na mimi hapa nilichangia nikazungumza hilo, kwa hiyo, tungetafuta vyanzo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaongeza tozo, kuna fedha ambazo zimetengwa za kununua mashangingi mia na zaidi. Kuna shilingi bilioni 77 za safari. Tunaposema kujifunga mkanda tungeonesha na huku kwa kupunguza haya matumizi yasiyo na lazima halafu hata tukaongeza kidogo tukawa na *justification.* Leo hii tunafanya haya kati ya shilingi trilioni 22, shilingi trilioni 16 ni pesa za matumizi ya kawaida, shilingi trilioni tatu zimeongezeka yaani hatuzungumzii *OC,* lakini kuna yale matumizi yasiyokuwa na lazima kwa nini tusiyapunguze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kuumwa nimekaa nyumbani hizo siku tatu, nimepitia bajeti zote tangu nimeingia kwenye Bunge hili, hakuna mwaka hata mmoja hata kwa fedha zetu za ndani zimetoka zote, hakuna! Ni kwamba fedha ambazo hazijatoka za ndani na za nje ni zaidi ya bajeti za Wizara nne. Kasomeni Wabunge mtaona, ni zaidi ya bajeti ya Wizara nne na kilio ni hichohicho tunatenga fedha hazitoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chako, unasema moja ya sababu ya wahisani kutotenga fedha, wanaahidi vitu ambavyo hawatekelezi na masharti, lakini tunajua na sisi tungekuwa tunashughulikia matatizo yetu yanapotokea bila kulazimishwa haya mambo yasingeendelea. Tumeona ubishani hapa wa kwenye *Escrow* yametufikisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri amezungumzia jambo lingine kwamba moja ya sababu ni *trend* ya ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi. Sasa bajeti iliyopita hakuna halmashauri ambayo imepata zaidi ya 50%. Tunajua nchi nzima miradi imesimama, je, tuna uhakika gani kwa kigezo hicho wataendelea kutupa? Umesema mwenyewe na miradi kweli haijakamilika. Katika shilingi trilioni tano za maendeleo tulizotenga shilingi trilioni mbili bado tunatarajia kutoka kwao. Hapohapo kuna miradi haijakamilika, je, watatupa? Tunaenda kuwaombaje kama miradi nchi nzima ime-*stuck* watatupa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda kuzungumzia suala la madeni. Jamani naomba nizungumzie suala la madeni kwenye *MSD,* shilingi bilioni 103. Suala hili tulianza kulizungumzia tangu tunaingia Bungeni, tangu nikiwa Kamati ya Mashirika ya Umma na *MSD* ndiye anayesambaza dawa. Leo hii tunasema watoto chini ya miaka mitano, akinamama wajawazito na wazee wapate huduma ya matibabu bure, hatupeleki dawa. Hospitali zetu na zahanati zetu huko vijijini ni choka mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi kujenga zahanati ni jambo zuri, lakini pelekeni dawa. Kama hamuwalipi hawa *MSD* watapeleka nini? Akina mama, wazee, watoto wanateseka yaani tunaweza tukacheza katika maeneo mengine lakini si afya ya Watanzania. Kama Mtanzania hana afya bora atawezaje kwenda kutafuta kipato chake cha siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kwa Mkoa wa Mara peke yake, wakandarasi wanaosambaza vyakula mashuleni wanadai shilingi bilioni mbili na zaidi. Wengine wamekopa benki, wengine wameomba tu huko mitaji, wengine mbali ya kwamba hali yetu mbaya wamejikakamua, hawajalipwa na ni nchi nzima siyo Mara peke yake. Wakandarasi wa barabara wengine mpaka walikufa kwa *pressure*. Sasa tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, haya mambo yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kuna pesa ambazo hatulipi kwenye maeneo muhimu lakini ukisoma ripoti ya *CAG* kuna shilingi trilioni nne ziko kwa mawakala. Yaani hata pesa zetu tunashindwa kuzikusanya halafu hapohapo tunakuja kumbana Mtanzania wa kawaida. Kila Mtanzania sawa anapaswa kulipa kodi lakini lazima aone ile kodi inaenda wapi? Haiwezekani fedha nyingi zikaishia kwa watu wachache. Watanzania wanapenda Taifa lao lakini lazima suala la uwajibikaji liwe kwa pande zote, wanaosimamia na wanaokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea miongoni mwa sheria ambazo tungezifanyia mabadiliko ni Sheria ya Manunuzi ndiyo kuna kichaka cha wizi mkubwa. Tenda ya shilingi bilioni mbili mtu atalipwa shilingi bilioni kumi. *Why* tunaachia mianya ya watu kuiba bila sababu. Halafu mwisho wa siku tunaenda kumbana yule Mtanzania ambaye uchumi wake bado hatujauimarisha vizuri yaani Sheria ya Manunuzi ni kichaka cha wizi. Huko kwenye halmashauri ndiko ambako wanatumia kuiba. Sasa tunaomba Mheshimiwa Saada, una uwezo, hebu haya mambo yafanyie kazi yaani tangu tumeingia tunalalamikia haya mambo mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa ndiyo usiseme, bajeti ya Uganda wao wametenga 20% kwa ajili ya kwenda kulipa deni la Taifa. Sawa kwamba tunakopa lakini pia ukiwa unakopa kila siku mwisho wa siku hutakopesheka tena.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya. Sasa namwita Mheshimiwa Kombo, hayupo, namwita Mheshimiwa Chiku Abwao.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu kuhusu bajeti na hotuba ya Mipango iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Nagu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitoe rambirambi zangu kwa familia na ndugu na Waislamu wote kwa kuondokewa na Mufti wetu, Shekhe Issa Shaaban Simba. Mwenyezi Mungu aipokee na ailaze mahali pema peponi roho yake na nasema kwamba, *inna lillahi wa inna ilaihi rajiun.* Pia, nawatakia Waislamu wenzangu wote mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu atujalie afya njema ili tuweze kufunga salama na kwa afya njema bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa wote ambao walishirikiana nami katika maandalizi ya harusi ya mwanangu, nawashukuru sana. Harusi ilifanyika, Mwenyezi Mungu asaidie familia hii ya mwanangu aweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa ni mchango wangu wa mwisho, naomba nishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo na viongozi wote kwa kuniwezesha kuwa Mbunge na wanawake wote wa Iringa na wananchi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao walionipa ili kufanya kazi zangu za Ubunge bila matatizoyoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hap, naomba niingie katika mchango wa bajeti. Ukweli ni kwamba, sikutaka kuchangia Wizara yoyote safari hii kwa sababu nimechoka kuona kwamba tunatoa michango mizuri ndani ya Bunge lakini hakuna kinachofanyika. Pia niwapongeze wasemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba zao zote mbili, wamezitoa kwa ufanisi mkubwa na wamechambua kwa umakini sana ingawa siku zote tumekuwa tukifanya kazi ya bure ambayo haizai matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipanga bajeti kwa miaka mitano sasa. Tumekuwa tukitoa ushauri kwa kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha Serikali inajaribu kusaidia kuleta maisha yaliyo bora kwa Watanzania, kuwapunguzia makali ya maisha. Cha kushangaza badala ya kuwapunguzia makali ya maisha imekuwa kama ni staili tu za mizunguko wakati wananchi maisha yakizidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie tozo ya mafuta. Tozo ya mafuta imezungumziwa karibu asilimia 85 ya Wabunge humu ndani wakilalamika na kuomba kwamba hii tozo iangaliwe upya kwa sababu italeta matatizo makubwa kwa Watanzania na hasa wa vijijini na wale wa kima cha chini cha mshahara. Kuna Wabunge ambao wamesema afadhali eti labda tungerudisha tena kuongeza bei za bia au sigara kama ilivyo desturi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa sio suala la kuongeza sigara wala pombe kwa sababu kwa kuongeza tozo ya mafuta tayari kila kitu kitapanda bei. Kwa maana hiyo, Serikali safari hii imeamua kupandisha kila kitu bei kwa Watanzania. Ni kweli, umeme tunauhitaji lakini lazima tuangalie utaratibu mwingine wa kuweza kufanikisha suala la umeme. Kuongeza tozo ya mafuta ndugu zangu tumejifunga kitanzi kwa Watanzania kuishi maisha magumu kuliko wakati wote uliokwishapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, suala la kuongeza tozo hili tulitoe, tuangalie ni namna gani tutafanikisha kupeleka umeme vijijini. Nchi yetu hii siyo maskini, tuna rasilimali nyingi sana. Tuna madini ya kutosha, tuna misitu, tuna bahari, tuna maziwa, tuna mambo mengi ambayo kama Serikali itazingatia kuleta ufanisi hakuna haja ya kuongeza tozo ya mafuta ambayo itamgusa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilipo kwanza tena nisije nikasahau, nimetumwa na wananchi mimi wa kima cha chini cha mshahara, wamesema wao wanafadhaika sana

wanashindwa kupanga bajeti ya kutumia Sh.260,000. Naomba leo Mawaziri wote wawili wa Mipango na Waziri wa Fedha wakati wanajibu hoja watupangie bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa hili na wananchi na mimi hili nitashika shilingi; wapangiwe bajeti ya kuweza kuishi kwa Sh.260,000/= kwa mwezi mzima, ikizingatiwa kwamba wamepanga nyumba watatakiwa kulipa kodi ya nyumba, watatakiwa kulipa umeme, watatakiwa kulipa maji, watatakiwa kuwa na nauli ya kwenda kazini na kurudi kila siku na watatakiwa wale milo mitatu, waanze na chai asubuhi au uji, waje wale chakula cha mchana, waje wale chakula cha jioni na hatimaye wawe na hela ya dharura ya kuwafanya wawe na amani ya kuishi mwezi mzima wakienda kazini na kurudi na wakiishi na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ombi ambalo nimeombwa kwa dhati kabisa na wananchi wamenitumia *message* ziko hapa, mkitaka kuona, wanasema kwamba, Mheshimiwa tumesikia unachangia leo, tunaomba uwaambie Mawaziri, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango watusaidie kutupendekezea bajeti ambayo itatuwezesha sisi kuishi toka tarehe moja mpaka mwisho wa mwezi kwa Sh.260,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili siyo la kupuuza hata kidogo, Watanzania wa kima cha chini wanashindwa kuishi, wanashindwa kufanya kazi, hawawi na amani katika maisha yao kwa sababu, hawana kipato cha kuwasaidia. Sasa leo na mimi nawasaidia na nitasimamia hili. Wakati wanajibu hoja Mawaziri wote wawili, Waziri wa Mipango apange mipango mahsusi kabisa ya matumizi Sh.260,000 na Waziri wa Fedha hali kadhalika naye atupe mpango wa kumfanya Mtanzania aweze kusaidiwa kupanga bajeti ili kweli aweze kuishi toka tarehe 1 mpaka tarehe 30 kwa yote haya niliyoainisha alipe maji, alipe umeme, alipe kodi ya nyumba, ale chakula milo mitatu na awe ana dharura kidogo akipatwa na shida ambayo inaweza ikamkwaza katika siku hizo ambazo anaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Wabunge wengi pia wamelizungumza hapa, wamezungumzia suala la kuporomoka kwa shilingi. Suala hili pia ni nyeti sana, Tanzania tumekuwa tunaithamini dola ya Marekani. Kwa nchi ambazo nimebahatika kwenda nimekuta kwamba ukishakwenda kule hata hiyo dola wao hawaitaki ukiacha Marekani kwenyewe. Wao wanataka ukifika uchukue hela yao ndiyo uanze kutumia sisi hivi tunapata kigugumizi gani cha kuamua mara moja kwamba hatutaruhusu dola itumike eneo lolote la biashara katika nchi yetu? Kuna maslahi gani ambayo mnayang'ang'ania hapa viongozi? Mnanufaika nini ninyi kwa kutumia sana dola katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila jambo tukilalamika hapa Wabunge na hii imekuwa kama ni ugonjwa sasa tunaambukizana wote, wanasema, ooh tutapanga, tutaangalia na hii ni lugha haswa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutaangalia hili jambo kweli linakubalika lakini tutageuza, tutapanga, tutafanya nini, halipangiki, haligeuziki, halitekelezeki, tumechoka. Hii lugha sasa inaambukiza Mawaziri wote wanakuwa na lugha hiyohiyo, hili suala zuri, Wabunge tumelisikia, tutaangalia, tutageuza, mtapanga mpaka lini? Mnashindwaje kutoa maamuzi katika mambo ya msingi kabisa ambayo yanatuletea shida katika Taifa letu hata katika suala la kulinda pesa yetu! Mnataka leo Watanzania tufikie kuikataa hela yetu ya Tanzania kwamba haina maana wala thamani yoyote tukimbilie kwenye dola na hii imeshatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Harare - Zimbabwe, kule hela yao hawaitaki kwa sababu imekuwa ni mzigo, viongozi mnataka tufike huko? Leo pesa yetu tuikatae kwa sababu tu ninyi viongozi mmeshindwa kuisimamia? Mmeshindwa kabisa kukataa dola isiwe pesa inayotumika katika nchi yetu? Kweli dola ni muhimu tutumie huko wanakoihitaji sisi tutumie pesa yetu ya Tanzania. Waheshimiwa Mawaziri, naomba iwe mwisho sasa, hii habari ya kusema

Waheshimiwa Wabunge tumewasikia, jambo hili ni nzuri tutaangalia, tutapanga, tutageuza iwe mwisho, linatuchosha linaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ningependa hata Mheshimiwa Waziri angekuwa hapa asikie, hii lugha ameizoea sana jamani. Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtaniunga mkono, anakubali sana ushauri, kwa kubali ushauri mimi naweza kusema labda ni Waziri namba mmoja, hata katika lugha nzuri ya kidiplomasia isiyo na maudhi Mheshimiwa Waziri Mkuu ana lugha nzuri sana lakini hili suala la utekelezaji kwake ni tatizo kubwa. Serikali nzima sasa mmelemewa na hili suala, wote Mawaziri mkisimama mnasema hili suala tumelikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi Naibu Waziri wa Fedha nilimuuliza kuhusu utekelezaji wa hoja ya Wabunge ya kwamba wahitimu wa vyuo watumie vyeti vyao kama mtaji wapewe mkopo, jambo ambalo lilishaitikiwa hapo siku za nyuma tukaambiwa hivyohivyo litapangwa, litageuzwa, juzi tena karudia kusema hivyohivyo. Hili suala ni zuri Mheshimiwa Mbunge tutapanga, tutaangalia, mtapanga na kuangalia mpaka lini? Hii lugha ya viongozi wangu iwe mwisho, hatutaki mambo ya kupanga, tunataka utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tatizo hilo la pesa yetu kuzidi kushuka thamani, naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Kangi Lugola, kwa jinsi alivyoainisha hapa tunashindwa kusimamia viwanda vyetu vitoe uzalishaji hata kwa vitu vidogo vidogo tu kila kitu tunategemea kutoka nje. Hii ndiyo inatufanya pesa yetu haikui, kila siku uchumi wetu unazidi kudorora ingawa ninyi mnasema uchumi unakua, sijui kukua kwa uchumi maana yake nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba hoja zote za Upinzani ambazo tumekuwa tukizisema ndani ya Bunge hili ambazo mmekuwa mkitupinga siku zote, leo hii wagombea wenu wa Urais wote wanazungumzia Sera za UKAWA. Wanasema kwamba sasa hivi mkinichagua mimi ndiyo nitafanya hivi, yote tuliyokuwa tunayasema sisi Wapinzani humu ndani ndiyo yanaenda kunadiwa sera huko ya kutaka Urais. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ya ajabu kabisa, mmeshindwa! Kumbe mngekuwa mnayachukua haya toka mwaka wa kwanza tulipoingia ndani ya Bunge hili leo hii tungekuwa mbali mnakuja kuyazungumza leo kwa kutaka kura. Watanzania nawaambia msiwasikilize hawa watu ni watu wa *propaganda*, hawafai, wameshindwa, hawana sera. Mmekuwa mkisema Wapinzani hatuna sera kumbe ninyi hamna sera mnadandia za kwetu leo mnaombea Urais, hamziwezi, hamjui siri yake wala hamtaweza kuzitekeleza na huu ndiyo mwisho wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nilivyoenda kuhamasisha watu wajiandikishe walikuwa wanasema wamepata kichinjio, wao wanaita hiki kitambulisho cha kupigia kura ni kichinjio, ni kuichinja CCM mpaka ife. Ni kuichinja CCM mpaka ife, tumechoka na umaskini, tumechoka kudanganywa, tumechoka kupuuzwa, sasa tunataka mabadiliko, hakuna kutawaliwa tena na chama ambacho kimeshindwa kutekeleza wajibu wake, Watanzania wakati wenu umefika wa kulipa kisasi. Tusingoje kukaa tunalialia tena kama kulia tumelia vya kutosha, tumeteswa vya kutosha hatuko tayari tena kuteseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania nimetumia fursa kuwaambia kudanganywa na Chama cha Mapinduzi sasa ni mwisho, mmeshuhudia wenyewe hawa sera, sera wanayoondoka nayo mitaani ni sera UKAWA.

**MBUNGE FULANI:** Ubwabwa wa asubuhi huo.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Kwa hiyo, hiyo siyo sera yao wameshindwa, hawataweza kuitekeleza ni kuondoka madarakani, mtupishe tumechoshwa na umaskini ambao mnatupa kwa makusudi…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Ubwabwa wa asubuhi huo.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** …ili tuendelee kuwa wanyonge kuwaombaomba misaada. Watanzania msindanyike kabisa. Watanzania tumechoka na umaskini. Huu ugonjwa wa umaskini mnaotaka kutupatia mbakie nao wenyewe, tunawatoa madarakani turekebishe nchi, haiwezekani hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waziri jambo moja kwamba hii bajeti imepangwa kwa lengo la kujitegemea. Kwa kweli kama tutapanga bajeti zetu kwa kujitegemea na ndipo tutaweza kuwa na changamoto ya kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba tunatekeleza malengo kuliko kukaa tunategemea wafadhili. Namshangaa unakuja kukurupuka leo kwamba unataka eti tujitegemee ulikuwa wapi. Unaweza kusema ni juzi tu umekuwa Waziri wa Fedha lakini viongozi wako na uongozi ni taasisi, chama kinaongoza...

**MBUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Hakuna aah, aah, hapa mnaambiwa ukweli mmeze shubiri tu mnasikia? Ilikuwa mpange toka mwanzo kwamba… *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiku zungumza na Kiti.

**MBUNGE FULANI:** Wanafanya fujo.

**MWENYEKITI:** Zungumza na Kiti.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza na Kiti ndiyo maana nawapuuza hawa, mimi hawa hawanipi shida kwa sababu watu walioshindwa kazi siku zote wanajua kupiga kelele tu. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii bajeti kama kweli tutaendelea kupanga kwa kujitegemea itatusaidia akili zetu kufanya kazi kuhakikisha rasilimali zetu ambazo tunazo katika nchi yetu zinapatikana na zinatumika kikamilifu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho kinatakiwa kufanyika ni kuhakikisha kwamba tunawawezesha pia vijana kufanya kazi. Narudia hoja yangu

ileile kwamba vyeti vya wanafunzi ambao wamefaulu vizuri vitumike kama mtaji, wapewe mikopo waweze kufanya kazi ili waongeze uchumi wa nchi kwa sababu ajira hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Bwanausi atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete na Mheshimiwa Amina Mwidau.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya dada yetu Waziri wa Fedha na kuhusu mipango ya nchi katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, kukushukuru wewe na Wenyeviti wenzako lakini pia kumshukuru Dkt. Kashilillah na watendaji kwa jinsi walivyoliendesha Bunge hili kwa miaka mitano kwa ufanisi mkubwa sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Lulindi ambalo wamenipa ridhaa ya kuliongoza kama Mbunge wao kwa miaka mitano, nawashukuru kwa kunipa ushirikiano mkubwa sana. Napenda kuwaahidi kupitia Bunge hili na kwa sababu huu ndiyo uchangiaji wangu wa mwisho katika vikao hivi, kuwahakikishia kwamba mipango yote ambayo tumeianza tutahakikisha tunaitekeleza katika miaka mitano ijayo kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo, nianze kuchangia kwenye suala la mapato. *TRA* wamekuwa wakijitahidi sana kukusanya fedha lakini pia halmashauri zetu. Nataka niseme, moja ya jambo ambalo Wizara ya Fedha na Serikali haikupaswa kulitazama ni kuhusu viwango vikubwa vya kodi vinavyowekwa kwa wafanyabiashara wetu. Hiyo ni chanzo kikubwa sana cha kuwafanya wafanyabiashara wakwepe kulipa kodi kwa sababu baadhi ya tozo au kodi ni kubwa mno kiasi kwamba haziwezi kulipika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri na Naibu na Serikali kwa ujumla kutazama sana kuhusu mgogoro wa wafanyabiashara unaoendelea hivi sasa. Nashukuru wameunda Kamati yao, naomba Serikali isiwapuuze, iendelee kukaa nao, nina uhakika kabisa yapo mambo ya msingi ambayo Serikali inatakiwa kukubaliana nao ili wafanyabiashara wale waweze kulipa kodi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine ni Wabunge lakini pia ni wajasiriamali, unapomtoza asilimia 18 ya mauzo ya mfanyabiashara mdogo maana yake unachukua na mtaji wake. Hukati kutoka kwenye faida yake unakata mpaka kwenye mtaji wake. Kwa hiyo, kelele zingine zinapopigwa siyo kwamba wafanyabiashara hawataki kulipia lakini wanaona kwamba hata hiyo mitaji midogo waliyonayo inaondoka. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kweli wakae pamoja na wafanyabiashara hawa wakubaliane kimsingi ni utaratibu upi mzuri utafanywa ili wananchi hawa waweze kulipa kodi vizuri na kuchangia kwenye mapato ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niikumbushe tu Wizara ya Fedha kwamba kuna wakati kulishakuwa na utaratibu wa kuwatoza wafanyabiashara hawa wadogo si kwa asilimia kama ilivyo sasa, ni kutumia mtindo ule wa *stamp duty composition agreement* ambapo kulikuwa na kiasi fulani wanakadiriwa kulipa kwenye pato lao kulingana na jinsi wanavyopata. Hebu tutazame upya, si vibaya kurudi nyuma pale ambapo tunaona kuna haja ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nalisisitiza ni kwamba kwa miaka mingi Serikali yetu imekuwa ikitegemea sana vyanzo kutoka nje. Namshukuru dada yangu Waziri wa Fedha na Naibu wangu, ndugu yangu Mheshimiwa Malima na Mheshimiwa Mwigulu, kwa jinsi ambavyo mmeona kuna haja sasa Serikali kuwa na bajeti inayojitegemea. Naamini hali hii itaondoa utegemezi mkubwa ambao Taifa letu limekuwa likitegemea sana wahisani na hivyo kupelekea mipango mingi ya Serikali kutoenda vizuri. Nisisitize kwamba kupanga ni jambo lingine na kukusanya ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni-*declare interest* kwamba mimi nimekuwa kwenye Serikali hizi kuanzia chini kabisa. Nimekuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa miaka kumi, nimekuwa Diwani miaka kumi na nimekuwa Meya wa Dar es Salaam kwa miaka mitano. Kwa hiyo, nimekuwa kwenye utaratibu huu wa Serikali kwa muda mrefu sana. Tatizo kubwa lililopo Serikalini ni kwamba baadhi ya watendaji hawako *serious* na siyo wabunifu wa kufuatilia vyanzo vya mapato, tumekuwa tukiridhika, mtu asipokusanya, akikusanya mshahara wake uko palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima wakati mwingine Wizara na Serikali itafute *incentives* za kusaidia watendaji wale wazuri na wanaojituma katika ukusanyaji wa mapato ili asiyekusanya na anayekusanya kuwe na utofauti. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ilizingatie jambo hilo ambalo ni muhimu sana katika kuhakikisha mapato yetu yanakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye matumizi, Serikali yetu imekuwa ikijitahidi kukusanya lakini tatizo lipo kwenye nidhamu ya matumizi. Mara nyingi hapa tumekuwa tukipitisha bajeti lakini bajeti zetu hazipewi umuhimu wowote. Bahati mbaya siyo hapa tu kwenye bajeti za Serikali Bungeni hata zile bajeti za halmashauri. Mara nyingi tumekuwa tukipitisha bajeti kwenye halmashauri na tukitakiwa sisi wanasiasa kwenda vijijini kuwaambia kilichopitishwa kwenye bajeti na nini kitafanywa katika mwaka huo wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kule viongozi tunaonekana waongo, kwa sababu tulichokipanga sicho kinachotekelezwa. Kumekuwa na shughuli za mlipuko zinazotoka Serikali Kuu kwamba chukueni fedha zote pelekeni kwenye jambo fulani, kwa hiyo, tunavunja kila kitu tulichokipanga. Ni jambo jema lakini kila jambo liwe kwenye mpango. Naiomba Serikali kwa kweli kwa sisi ambao wengi wetu tumekaa kwenye mazingira ya wananchi wa kawaida tunaelewa hali halisi ilivyo kule. Barabara zetu na madaraja yetu mengi hayawezi kutengenezeka kwa sababu halmashauri hazina fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niiulize Serikali, hivi tuna mpango wa kuua halmashauri? Kwa sababu enzi ya Baba wa Taifa tunakumbuka kabisa kwamba hizi halmashuari zilishawahi kuondolewa lakini Mwalimu katika hotuba zake alishawahi kusema katika jambo ambalo tulikosea ni kuziondoa Halmashauri za Wilaya na za Miji. Kwa hiyo, baada ya kurudi, nadhani bado kuna viongozi ndani ya Serikali Kuu wana *concept* ya kuona halmashauri hazitakiwi kuendelea kuwepo na ule ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwa halmashauri unaanza kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu liko tatizo la wengi wetu kudhani kwamba halmashauri zina pesa nyingi sana na kusukumiza kazi zote zikafanywe kwenye halmashauri. Ukweli ni kwamba siyo halmashauri zote zenye uwezo. Sasa hivi kama Halmashauri yangu ya Wilaya ya Masasi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu, hakuna halmashauri ina hali mbaya kama Halmashauri ya Wilaya ya Masasi hasa baada ya matukio ya kuchomewa moto ofisi zetu karibu zote ikabaki moja tu lakini pia kuchomewa magari zaidi ya kumi, halmashauri hii haijapata msaada wowote mzuri kutoka Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli majanga haya mbona yanapotokea kwenye maeneo ya wenzetu tunaona uharaka wa kupelekwa huduma, kwa nini siyo Masasi? Mheshimiwa Waziri tumekosa nini? Mezani kwenu kuna taarifa za maafa na tayari Serikali ilishatoa *commitment* ya kutoa fidia lakini mpaka leo *nobody cares,* sasa ile halmashauri unategemea itafanya kazi gani? Tunaletewa tu utaratibu hakikisheni maabara zote zinakamilika mpaka tarehe 30 Juni, hakikisheni hiki kinafanyika kwa fedha zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukusanya mapato kwa sababu hatuna magari ya kwenda kufuata ukusanyaji wa mapato, magari hamtupi. Tena kibaya zaidi Mheshimiwa Waziri naambiwa hata kwenye bajeti hii lile jengo la halmashauri ambalo lilikuwa linaendelea kujengwa hamjatoa hata senti tano kusaidia ujenzi ule, sasa hawa watumishi watakaa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka nikuombe tu Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unahitimisha hebu tueleze sisi Wanamasasi kwamba zile fidia ambazo ziko pale kwa ajili ya kusaidia taasisi maana yake hata jengo letu la CCM lote liliunguzwa moto mbali ya watu binafsi lakini pia ofisi za halmashauri pamoja na vifaa vyake, hebu tueleze kwamba nini *commitment* ya Serikali ambayo mnatarajia kuifanya kwenye Wilaya hii ya Masasi? Wakati mnapopeleka maelekezo kwenye halmashauri zote nchini basi itazame halmashauri yetu hata kwa kui-*support* kwa namna yoyote nyingine ili kutekeleza maagizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wangu amechanganyikiwa, *DT* amechanganyikiwa, wame-*paralyse* wafanye nini. Kwa hiyo, naomba kwa kweli hili Mheshimiwa Waziri hebu litilie maanani kwamba zile taasisi zilizopata maafa pamoja na halmashauri ni jinsi gani zitapata hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niende moja kwa moja kwenye lile Jimbo la Lulindi. Tatizo kubwa la Jimbo langu ni maji na katika bajeti ya 2013/2014, zilitengwa shilingi bilioni 4.8 kwa ajili ya miradi mikubwa ambayo ni agizo la Rais lakini hadi sasa ni karibu nusu tu ya fedha hizo zilizopatikana na katika bajeti hii tumetenga tena shilingi bilioni 1.9 ku-*support.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimemsikia dada yangu Mheshimiwa Waziri Mkuya akisema kwamba kuna fedha atawapa Wizara ya Maji na mimi niiombe Wizara ya Maji katika fedha hizo anazotoa dada yetu hebu pelekeni Lulindi kule katika miradi ya maji. Nilieleza pia kwamba hivi vijiji kumi vya *World Bank, World Bank* gani hiyo inayotekeleza miradi zaidi ya miaka 20? Tuondoe tutekeleze wenyewe kwa sababu inaonekana *World Bank* hawako tayari ku-*finance* miradi hii basi tui-*finance* wenyewe na tuitekeleze kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri, kuna barabara yetu ya kutoka Mtwara-Newala-Tandahimba-Masasi. Tungeomba Mheshimiwa Waziri, lile wazo ambalo limetoka kwamba tuanze mwaka huu huitengeneza kwa kiwango cha lami kwa kilomita 50, zianze na tumuombe Mheshimiwa wetu kabla hataondoka atuwekee jiwe la msingi pale, ili tuweze kutekeleza mambo yote.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa kweli nilitaka kuchangia hilo, lakini nataka kuchangia kwenye sekta ya afya. Mheshimiwa Waziri, hali ya huduma za afya vijijini ni mbaya sana na kama kuna mafungu huko Hazina na Serikalini, hebu tuelekeze ili wananchi wetu waweze kupata huduma vziuri.

Tunayo majengo ya zahanati, tunayo majengo ya vituo vya afya, lakini viko pale mara nyingi ni kama *white elephant,* hakuna huduma sahihi ambazo zinatakiwa zipatikane. Hebu

mtiririto wa kupeleka dawa, kupeleka watumishi, hebu tuongeze kasi, ili pale maeneo ambayo zahanati ambayo inahudumiwa na manesi, hebu tupate waganga, lakini pale ambapo kuna waganga na hakuna nesi, basi apelekwe nesi ili wale wananchi waweze kupata huduma.

Nina mifano mingi sana ya zahanati na vituo vya afya kwenye Jimbo langu nisingependa kuchukua muda mrefu sana kwa sababu nitachukua muda katika kuviorodhesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kilimo, sisi kilimo chetu cha biashara ni korosho. Nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi, kumpongeza sana Mheshimiwa mama Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho. Kwa jinsi anavyofanya kazi yake, ametekeleza kwa miaka mitatu na sasa Mheshimiwa Rais kutokana na utendaji wake amemteua tena kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho. *(Makofi)*

Hebu naomba Serikali sasa tumsaidie, wananchi wamehamasika sana kutumia hizi mbolea za ruzuku, hebu tuongeze kiwango cha fedha ili wakulima wetu wengi waweze kununua mfuko wa *sulfur* kwa sh. 15,000 badala ya 30,000 au 40,000 au 50,000 ambao upo sasa.

Naamini kabisa kwamba Serikali inaweza kabisa na pia inapoweza kutoa ruzuku zaidi, maana yake uzalishaji wa kotosho utaongezeka na kipato cha Serikali pia kitaongezeka. Kweli naamini kabisa hali hiyo tukiitekeleza, lakini pia katika msisitizo wa kuongeza thamani ya korosho kwa kubangua.

Serikali tuliviuza vile, tulivibinafsisha vile viwanda, hebu tuvirudishe, Serikali tuwe *committed*, kuhakikisha korosho zinabanguliwa hapa nchini. Suala la kupeleka korosho ghafi kule nje, linatuangusha sana. hebu tu-*add value* hapa, tuongeze thamani ya korosho, ili korosho zetu ziweze kupanda thamani, lakini pia tukieongeza thamani ya korosho, mana ayake tunaongeza pia kipato cha mkulima ili aweze kulima vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye suala la elimu, wote ni mashahidi kwamba walimu nadhani ndiyo kada kubwa katika ajira ya nchi hii, lakini mazingira ya walimu wengi, siyo nzuri hata kidogo. Nashauri Serikali, tusilimbikize malimbikizo ya fedha kwa muda mrefu na kujikuta inatakuwa kutoa ma-*billions* ya pesa. Tunapomaliza kulipa, tuendelee kulipa hatua kwa hatua, ili Serikali isibebe mzigo mkubwa, matokeo yake inapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, walimu hawa mazingira yao katika vijiji, siyo mazuri, wengine wanadiriki kutembea kilomita nyingi zaidi kufuata mishahara yao, hebu tuwatazame walimu. Liko wazo na ningependa Serikali la kulipa *teaching allowance*. Tulishalianza hili wakati wa awamu ya Mheshimiwa Rais Mwinyi, lilionyesha kabisa matunda mazuri kwa walimu, lakini baadaye likaondolewa. Mimi naomba sana Serikali ilitazame kwa nguvu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Abood ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ningependa kukushuku kwa kunipa nafasi hii, lakini na mimi nipate nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara yetu ya Fedha, ambayo inatupa nafasi ya kujua uelekeo wa nchi yetu katika siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kwanza kuwashukuru waajiri wangu, wananchi wa Jimbo la Chalinze, kwa kuendelea kwao kuniamini na kunipa ushirikiano mkubwa kwa sababu bila ya wao, nina hakika kabisa hata nguvu yenyewe ya kusimama hapa nisingelikuwa nayo. Wako wenzetu wengi sana ambao mambo yameshaanza kuwaharibikia huko Majimboni, sisi tunawapa pole, kwa sababu wananchi wa Jimbo la Chalinze wameendelea kunipa ushirikiano na mambo kwangu ni mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kipekee kabisa nikishukuru sana chama changu, maana tusione vinaelea, vimeundwa na waundai wenyewe kwenye siasa ya Tanzania ni CCM. *(Makofi)*

Nimeona hapa wenzangu wanajitahidi kuzungumza mambo ya siasa, dada yangu Chiku Abwao naona amezungumza zungumza, lakini naomba tu waelewe kwamba CCM ndiyo tunao-*set pace* na wengine watafuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nimshukuru sana mke wangu, maana unajua katika kipindi hiki, kipindi kigumu, muda mwingi tunakuwa tuko Majimboni na kwenye siasa hizi na wakati mwingine hata nyumba nazo zinatingishika, lakini namwomba anisamehe kama ataona kwamba simpi muda ila ni kwa sababu tunatengeneza nchi na wananchi waendelee kuona umuhimu wa mtoto mimi kuzaliwa ndani ya nchi yao. Pamoja na yeye ni washukuru pia wanangu wa uvumilivu wa kumkosa baba yao, lakini pia na ndugu zangu ambao siku zote wameendelea kunipa moyo wa kufanya kazi, lakini moyo wa uzalendo na moyo wa kuihudumia Tanzania yetu.

Pamoja na hayo, niwashukuru kidogo kwa nafasi ya kwanza marafiki zangu, ambao tumekuwa tunasaidiana nao siku zote katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kulisaidia Jimbo letu la Chalinze. Misaada yao imekuwa ni mizuri sana na misaada hiyo ndiyo ambayo inanifanya mimi leo hii nakuwa hata na nguvu ya kuwaambia wana Chalinze kwamba wasiwe na wasiwasi, ikifika Oktoba nitaendelea kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nichukue nafasi hii kwa upekee kabisa kuwapa pole Waislamu wenzangu, kwa kufiwa na Mufti wetu, Sheikh Shaban Simba. Ni msiba mzito, lakini naomba niwakumbushe tena kwamba, Mwenyezi Mungu anasema, kwamba sisi sote ni wake na kwake tutarejea. Kwa hiyo, hii ni safari ambayo imemkumba Mufti wetu, ambayo na sisi tunaobakia nyuma hatuna budi kujiandaa na safari hiyo, kwa sababu sisi wote ni wake na kwake tutarejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nitumie nafasi hii pia kabla sijaanza kuchangia, kuwatakia Waislamu wenzangu wote na dunia nzima, mfungo mwema wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, maana tumeanza leo na kipindi hiki ndicho kipindi ambacho tunatakiwa turudi kwake kwa nguvu sana. Hata hivyo, siyo leo tu siku zote tuwe hivyo ila tujitajidi sana katika kipindi hiki kuwa wakweli na hata tunapochangia bajeti hizi ee, tumwogope pia Mungu kuongopa, maana wakati mwingine unaweza kutumia ufundi wa kuongopa hapa ukatengeneza siasa, kwa Mungu haitompendeza pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia bajeti. Bajeti imezungumza vitu vizuri sana, lakini yako mambo ya msingi ambayo nataka niyazungumze siku ya leo ikiwa ni kuweka kumbukumbu sawa juu ya yale ambayo Wizara yetu, Waziri wetu bi Saada Mkuya na Naibu Waziri wake kaka yangu Adam Malima na ndugu Mwigulu, kwa jinsi walivyoweza kuonyesha uelekeo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze katika eneo la afya. Nimeona jitihada nzuri zilizofanyika katika bajeti, za kuainisha vipaumbele na mambo gani ya msingi ambayo wanataka kushughulikia kama Serikali. Hata hivyo, bado, yako mambo ambayo yanabakia kuwa katika ombwe kubwa na watu kusababisha sintofahamu ambayo mimi binafsi yangu ningependa nimwambie Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wanapotoa majibu ya hoja za Wabunge basi hili jambo nalo walizungumzie au waliweke katika mambo yao ya msingi.

Kwanza, sera nzima ya afya. Kwenye sera ya afya yetu inazungumza kwamba, msisitizo unawekwa kwa walemavu waweze kutibiwa bure, lakini, mpaka leo walemavu hao wanapokwenda mahospitalini tabu imeendelea kupatikana hasa katika uchangiaji wa mfuko wa afya. Jambo hilo mpaka sasa hivi hatuelewi, maana kule kwangu imefika sehemu walemavu wangu wale, hasa walemavu wa ngozi na wa viungo wananambia kwamba Mheshimiwa Mbunge tunakwenda hospitali, lakini tunaposema tutibiwe, tunaambiwa wakati mwingine kwamba bwana madawa yetu hayapo, wakati mwingine tunaambiwa kwamba vifaa tunavyovihitaji havipo; lakini Serikali iliweka msisitizo katika hili.

Sasa ni vema Mheshimiwa Waziri unapokuja, ukatolee majibu ya hili ili wananchi wangu wenye ulemavu pale Chalinze na Tanzania nzima wasikie juu ya jinsi gani Serikali imeji-*commit* kuhakikisha kwamba jambo hili wanalifanyia kazi na siyo jambo ambalo linabakia kwenye karatasi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Mheshimiwa Waziri, kwenye suala la afya, tuna ujenzi wa hospitali ya Chalinze.

Chalinze ni moja ya eneo ambalo kwa namna moja ama nyingine limekuwa linatoa huduma kubwa sana kwa afya za wapita njia. Watu wakipata matatizo ya afya, kwa wale wanaotokea njia ya Tanga, mara nyingi wanakimbilia Chalinze ikiwa sehemu ya kwanza, lakini pia wanapokosa Chalinze kituo chao kikubwa kinakuwa ni Tumbi.

Sasa Serikali ikaamua kuleta mpango mzuri wa kujenga hospitali ya Chalinze, sisi ndani ya halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo tumeshatengeneza bajeti, lakini bajeti ile haitowezekana kama wewe bi Saada Mkuya na wenzako hamtosema ndiyo. Sasa nataka hapo utakapokuwa unasimama utuambie juu ya yale maombi yetu ya Wilaya ya Bagamoyo kuhusiana na ujenzi wa hospitali ya Chalinze nyinyi mmejipanga nayo vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, pamoja na hilo, pia tumekuwa na changamoto kubwa sana ya miundombinu, hasa katika maeneo ya mahospitali na hata kwenye majengo yetu kuwa miundombinu siyo miundombinu rafiki. Sasa hili ni jambo la Kiserikali ambalo Waziri Mkuu, ofisi yake labda ikusaidieni kulielezea vizuri, lakini tumekuwa na tatizo kubwa sana na kwa kuwa hili ni eneo lenyewe la bajeti, basi nyinyi kama Serikali, nalo mngeweza kulitolea majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la mipango ya fedha zinazokusanywa kwenda kwenye kodi za mafuta, kupelekwa kwenye umeme vijijini. Mimi binafsi yangu kwanza nikupongezeni sana kwa kuona kwamba maeneo mengi sana ya watanzania yanatakiwa

kuwashwa umeme, lakini pili kwa kuona kwa upekee kabisa kwamba Jimbo la Chalinze, ni asilimia 24 tu ya Jimbo zima ambalo limekuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukombozi mkubwa sana, katika jambo hili, lakini Mheshimiwa Waziri, iko changamoto kubwa sana. Katika Jimbo la Chalinze na maeneo mengi sana ya Tanzania,akina na watoto wameendelea kufariki kwa kukosekana kwa huduma bora za afya.

Sasa kwangu mimi mnaponiambia kwamba fedha za kodi zinazopatikana kwenye mafuta zinakwenda kwenye umeme vijijini napata shida sana kwa sababu watu wangu wa Chalinze wataendelea kufa wakijiangalia kwenye umeme.

Sasa ningeomba sana Mheshimiwa Waziri, mtuambie katika mkakati mlionao, mmejipangaje kuhakikisha kwamba ziko fedha zinazotengwa kupelekwa kwenye maeneo ya afya. Kwa sababu tumekuwa kila siku tunalia, fedha zinazopelekwa kwenye eneo hilo zimekuwa ni chache sana na hata wakati mwingine kupata shida kubwa sana hasa tunapohitaji madawa, vifaa vya hospitali na hata pia tunapohitaji fedha kwa ajili ya kulipwa wauguzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo la ubia, kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wamelieleza katika hotuba yao ya bajeti kwamba bwana wanaendelea kutia msisitizo na msukumo mkubwa, kuhakikisha kwamba, mipango mikakati ya sekta binafsi na sekta za umma kufanya kazi kwa maendeleo ya wananchi nazo zinaendelea kuwekewa msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nakumbuka, wakati nachangia bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, nilizungumzia juu ya mahusiano yaliyopo baina ya Kampuni ya *Edosama Hardware limited* na *TIB*. Hawa kampuni hii ni kampuni ya kizalendo ambayo wameanzisha mradi wa kutengeneza madawati, ambayo madawati yake kwa bei yake linauzwa dawati moja lenye kukaa wanafunzi watatu 25,000/= na wale mabwana wakawa na mpango wa kuhakikisha kwamba wanatengeneza kiwanda hapa. Waliongea na watu wa *TIB*, lakini *TIB* mpaka leo hii hawaeleweki kwa sababu ile *go ahead* ya kutoa fedha na kuhakikisha kwamba mradi huu unafanyiwa kazi, haiendi vizuri. Hapa ndiyo narudi katika mchango wa ndugu yangu Kangi Lugola alosema jana, kwamba tumeendelea kugeuza nchi yetu kwamba ni dampo la vitu vya nje, jambo ambalo tunaweza sisi wenyewe tukajikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anguko la shilingi. Katika anguko la shilingi nimeona mipango mizuri ambayo Serikali imeendelea kuifanya, mojawapo ikiendelea kuimarisha vituo vyetu vya *EPZ* na *Special Economic Zone (SEZ),* katika kuhakikisha kwamba tunatengeneza bidhaa zetu na kuziuza nje. Pamoja na hilo, pale Bagamoyo, tunalo eneo la *EPZ*, pale Zinga, lakini niseme masikitiko yangu makubwa, eneo lile sasa limeshakuwa pori, sasa sielewi, kwamba tunapozungumzia mpango mkakati wa kuimarisha *EPZ*, huu ni mkakati ambao unaendelea kubaki kwenye makaratasi, au ni mkakati ambao utafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeamua kabisa kwa dhati, tunataka kuimarisha *EPZ* na *SEZ*, basi ni vyema sasa Serikali ikatuambia juu ya mkakati gani walionao katika kuhakikisha kwamba wanafanya uratibu mzuri kwa wale watu wanaopewa maeneo hayo, ili waweze kuhakikisha kwamba, mtu anapopewa eneo basi analifanyia kazi kama ambavyo wamekubaliana; na kama atashindwa kufanya hivyo basi Serikali ichukue hatua za kumnyang'anya na kutafuta mtu mwingine ambaye anaweza kufanya hivyo. Mfano mzuri umefanyika katika maeneo ya ardhi na naamini kabisa kwa mfano aliofanya Mheshimiwa

Lukuvi, ni wazi kabisa kwamba Serikali ikiiga hilo basi tutaendelea kuneemeka na Serikali yetu na watu wataendelea kuipenda Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, kuna eneo la maji, Jimbo la Chalinze tumepata bahati ya kupata mradi wa maji wa Wami, lakini mradi ule umekuwa ni sehemu ya masikitiko makubwa sana ya watu wa Chalinze. Eneo la Chalinze limeendelea kukosa maji, lakini tunapouliza wale wataalam wa pale kwenye Mamlaka ya Bonde la Wami, wanachotujibu, ni kwamba upungufu wa fedha. Kwa mfano, mimi nimeingia hapa nina vipindi viwili sasa, bajeti hii ya pili, lakini bajeti ya mwaka jana tulitenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji, hakuna kitu, bajeti ya mwaka huu tena tumetenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji.

Sasa nataka nisikie *commitment* ya Serikali juu ya jambo hili, kwa sababu hali ya Jimbo la Chalinze, upande wa maji imeendelea kuwa mbaya sana kiasi kwamba inatupelekea sehemu ya kuogopa, kama pakitokea magonjwa ya mlipuko, basi mnaweza mkaja sasa Serikali kuja kuokoa afya za watu katika maana ya kwamba watu watakuwa wanakufa na kupata matatizo makubwa ya kiafa kwa sababu maji hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nizungumzie pia jambo la uwekezaji mdogomdogo katika maeneo ya viwanda. Ndani ya Jimbo la Chalinze kama niliwahi kuzungumzia katika bajeti ya Wizara ya Viwanda Biashara na Wizara ya Kazi na Ajira katika Bunge lililopita, kwamba eneo la Chalinze ni eneo *strategic* kabisa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vya namna hiyo, lakini Serikali ilipokea jambo lile na ikatwambia kwamba inaendelea kulifanyia kazi na tumeona baadhi ya juhudi ambazo zinafanyika, lakini nataka niseme kwamba juhudi zile zimekuwa ziko taratibu sana, kisai kwamba zinatusumbua sisi wapenda maendeleo juu ya *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba maisha ya watu yanaendelea kuneemeka kutokana na fursa zinazojitokeza kwa mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, wananchi wa Chalinze niwashukuruni sana, mimi nitakuja tena Chalinze kuomba ruhusa yenu ili mnipe nafasi nyingine ya kuendelea kuwahudumia. Mwaka huu mmoja nimefanya kazi kubwa, ambayo naamini kabisa nimeonyesha mfano wa nini ambacho naweza nikakifanya tukipewa miaka mitano ya kuwahudumia katika Serikali yetu. Nawaomba sana watu wa Chalinze waendelee kuniamini, lakini pia wanipe nafasi niendelee kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya chama changu, niendelee kuwatoa wasiwasi wenzetu hawa wa UKAWA, msiwe na wasiwasi, Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoendesha Serikali hii, kitafanya kila kitu kinachowezekana kuhakikisha kwamba kinafikia malengo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa dada yangu Chiku Abwao, nimwambie tu kwamba kinachofanyika sasa hivi siyo wizi wa sera zenu, Serikali iliyopo inaondoka, waliopo wanaotaka kuongoza watu wanatoa matumaini mapya kwa watu na juu ya jinsi gani wanataka kutekeleza yale ambayo wanataka kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana, ahsante sana kwa kunisikiliza. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Amina Mwidau, atafuatiwa na Mheshimiwa Abood, Mheshimiwa Yahya Kassim ajiandae na Mheshimiwa Maria Hewa.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya lala salama. Awali ya yote kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake. Kwa aina ya kipekee kabisa nikishukuru sana chama changu kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuweza kuwakilisha katika Mkoa wa Tanga.

Ni imani yangu kuwa nafasi hii nimeitendea haki. Tatu, nawashukuru sana wananchi wa Tanga kwa ushirikiano wao, lakini shukrani za pekee kwa ndugu zangu wa Pangani kwa ushirikiano mkubwa sana ambao wamenipatia na wanaoendelea kunipatia mpaka sasa hivi. Niwahakikishie tu kuwa tuko pamoja na sitawaangusha. Wanajua kuwa nagombea Jimbo, watu wa Pangani wanajua kuwa mimi nimechukua *form* na chama change kimenipitisha na siendi kujaribu, ninakwenda kugombea. Kwa hiyo, nakwenda kushinda vile vitisho vya akinamama, wanawake vyote havina nafasi safari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nichukue nafasi hii ya kipekee kuwapongeza sana viongozi wangu wa chama, Mwenyekiti na Katibu Mkuu kwa kutia nia na kwenda kuchukua *form*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mwanzo tu wa UKAWA jamani, naona pale Ridhiwani alivyomalizia anasema CCM bado tunaendelea, najua kuwa mna wagombea 36 lakini na sisi wa UKAWA ni mwanzo jamani, ndiyo tumeanza kuchukua *form*, msiwe na wasi wasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wamepita wamechangia mengi mazuri, nami naomba kuongezea katika bajeti hii. Tunajua ni bajeti ya lala salama, ni bajeti ambayo ina vipaumbele vichache kwa mujibu wa Waziri alivyoeleza kwenye kitabu chake, lakini kipaumbele cha kwanza ni uchaguzi. Ni jambo muhimu kwa sababu liko mbele yetu. Najua kuwa Mheshimiwa Waziri ni dada yangu, swahiba wangu, ni mchapa kazi si kama namsifu kwa sababu ni swahiba wangu lakini ni mchapa kazi; na majemedari wake, Mheshimiwa Malima na Mwigulu. Vile vile kwa kweli kuna hali ngumu kwa bajeti yao ambayo iko mbele yetu. Kwa sababu ukiangalia ugumu wa *implementation* ya bajeti iliyopita ambayo tunaendelea nayo, tunaimalizia, kuna mengi ambayo yamejitokeza, lakini kubwa ni kiwango cha makadirio ya mapato yale tuliyoyategemea hakikufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na tatizo kubwa lililojitokeza la kashfa ya Tegeta *Escrow* lolilosababisha misaada ile ikaweza kuchelewa. Kwa hiyo, Wabunge wengi hapa tumepiga kelele sana kwa sababu pesa zile za maendeleo hazikuweza kufikiwa, ni asilimia 40 tu. Kwa hiyo hakukuwa na utekelezaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mfumo huu wa bajeti tatizo kubwa kabisa hapa na Mheshimiwa Sakaya hapa kiongozi wangu amelielezea, kwenye ukusanyaji wa mapato. Kuna tatizo kubwa sana sana sana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vitabu vyote tangu tumeingia hapa Bungeni anaelezea jinsi ambavyo kunakuwa na mirija katika ukusanyaji wa mapato. Hii ndiyo inayosababisha ukusanyaji ukawa mdogo sana. Najua *TRA* wamejipanga na wameanza mikakati, lakini bado haitoshi, tunatakiwa tujifunge mikanda hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* wameshaanza kujipanga vizuri lakini bado ukiangalia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali safari hii ameonesha kuna mizigo ya *transit* ambayo inasema inapita hapa nchini, lakini ni mizigo inayoishia hapa. Kodi yake ni bilioni mia nane na; hao ni wafanyabishara wakubwa, wakubwa kabisa. Kwa hiyo, nina imani kabisa *TRA* katika kujipanga kwao na hili wataliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha ya kodi kiholela, hili Mheshimiwa Saada katika kitabu chake hiki ameelezea mikakati iliyoyopo. Hata hivyo, ningeomba Serikali isitoe tu maelezo, iyafanyie kazi kwa sababu hapa Mheshimiwa ameelezea mapendekezo ambayo yako kwenye Miswada, kwenye wawekezaji wakubwa wa kimkakati watakaopewa misamaha hii, lakini vile vile iliyopo sasa hivi ipunguzwe. Nina imani kabisa tukiweza kukusanya vizuri hiyo mikopo ambayo tunakwenda kukopa ya masharti ya kibiashara tutaweza kuipunguza vile vile kama tulivyopunguza misaada na mikopo yenye masharti nafuu, lakini tuongeze udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa, tunajua sheria ya bajeti ipo na imepitishwa, lakini sheria peke yake haitoshi, Serikali yetu ina tatizo kubwa kabisa la usimamizi na utekelezaji wa sheria, nidhamu hiyo na utamaduni huo haupo. Naomba kabisa mjitahidi, kuwe na dhamira ya dhati kabisa katika kutekeleza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye Deni la Taifa. Ukiangalia Mheshimiwa Saada alivyoelezea hapa, amesema kuwa Deni la Taifa mpaka kufikia Machi mwaka huu wa 2015 ni trilioni thelathini na tano. Ukiangalia kwa mwaka wa jana Machi ilikuwa ni trilioni thelathini, limekua kwa asilimia 21. Kwa hiyo, hapa unaona kuwa kasi ya kukua kwa Deni la Taifa ni kubwa kuliko kasi ya kukua kwa Pato la Taifa. Hili ni tatizo na Mheshimiwa Waziri ameelezea kuwa deni letu linahimilika. Hili sikubaliani nalo sana kwa sababu sisi Tanzania tuna historia ya kuomba kufutiwa madeni, na hiyo imefanyika mwaka 2000 na imefanyika mwaka 2006. Hili ni tatizo na ndiyo maana bado tunakuwa na bajeti tegemezi. Mheshimiwa Waziri nakuomba na Bunge hili tuliomba sana; kukopa tunajua ni kwa ajili ya maendeleo, lakini maendeleo yale wananchi wanapenda wayaone. Tunaposema tunakopa, tunakopa kwa ajili ya nini? Vile vile tunakopa wapi? Hicho ni kitu muhimu sana. Bunge hili tuliomba kama ingewezekana mikopo hiyo tuweze kuletewa Bungeni ili tuweze kujua ni kitu gani hasa tunakwenda kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye mafao kwa wazee. Hapa ukiangalia *page* ya 14, ni kweli imeingizwa kwenye bajeti na inaonesha kuwa wazee wetu wameangaliwa, lakini, jinsi ambavyo hapa imeelezewa, Serikali inatarajia kuanza maandalizi ya kuwezesha kufanya hayo, maandalizi hayo ni pamoja na kutunga sheria stahiki, kuwatambua na kuweka mfumo wa kulipa. Kwa mwaka gani, 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa Mheshimiwa Hokororo alielezea pia na akatilia msisitizo sana, nakubaliana nao, nakubali sheria tumeipitisha, lakini, kuna tatizo la utekelezaji, hii inaweza ikatumika 2015/2016, peke yake; mpaka linamalizika Bunge linalokuja ndipo wazee hao wanapewa mafao hayo. Naiomba Serikali iharakishe katika hilli. Kama kweli wametia nia katika hili basi walifanyie kazi kwa kiwango cha juu sana, yale mambo ya kesho kesho kutwa si mazuri. Pia, inaonekana kuwa tunafanya mambo kisiasa zaidi kwa sababu kesho kutwa ni uchaguzi, ili kuwavuta wazee basi inawekwa tu, lakini ikifanyika, mkitembea kwenye maneno yenu itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko kwa kweli imeoneshwa hapa, ukiangalia *page* ya 12 Waziri ameelezea kwenye Hotuba yake, lakini Mheshimiwa Waziri nakuomba, unajua hali za Mifuko. Hapa umeelezea *PSPF* kwa sababu deni lao limeshaingizwa kwenye bajeti basi wataweza kulipwa, naomba kwanza waharakishiwe kulipwa, lakini pia na Mifuko mingine kwa sababu Mifuko mingine nayo, ukiacha *PSPF* inadai. Mheshimiwa waziri nakuomba uiangalie mifuko kwa nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kutoa mapendekezo yangu ili kuongeza vyanzo hivi vya mapato. Tuna tatizo kwenye vyanzo vya mapato. Wabunge waliopita hapa na mimi nakubaliana na kukusanya pesa kwa ajili ya kuongezea kwenye *REA*, umeme ndiyo maendeleo. Hata hivyo, kuongeza kwenye mafuta ya taa, kuongeza kwenye *petrol*, kwenye

*diesel* tunawaongezea mzigo mkubwa sana sana sana Watanzania. Si kama hatukubaliani na umeme, umeme tunakubaliana nao kabisa, lakini tunaomba muangalie sehemu ya kuongeza tozo hiyo, si kwenye mafuta ya taa, tunawaumiza wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kodi ya majengo. Serikali kwa kweli inapoteza pesa nyingi sana kwenye nyumba. Tuliomba na nilisoma katika mapendekezo miaka iliyopita, tangu nimeingia Bunge hili 2011/2012 mpaka leo. Tulipendekeza Serikali ianzishe *Real Estate Regulatory Authority* ili iweze kuwatambua wenye nyumba. Ukishawajua wenye nyumba tutajua wanavyopangisha, kama ni nyumba, kama ni chumba kimoja kimoja Serikali itapata mapato kwenye hilo. Tunapoteza pesa nyingi sana hapa. Kubwa ni kwa kuwa viongozi wengi wanaotunga sheria wanaofanya haya wana nyumba hizi. Ni muhimu sana tukiweza kuiga hata kwa wenzetu wa Kenya. Kenya wanafanya vizuri sana kwenye hili. Kila kitu kina changamoto zake. Niwaombe ndugu zangu mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimesikia wabunge wengine wamependekeza nami naomba kusisitiza, kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. Mheshimiwa Hamad Rashid ni mdau mkuu katika hilo na yuko kwenye Kamati ya Bajeti na Kamati ya Bajeti imependekeza hili. Tutilie maanani uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia kupendekeza, kule kwetu Tanga kuna bahari kubwa na tuliomba na nilimsikia Mheshimiwa Kitandula akaomba Bandari ya Uvuvi na eneo wanalo MOA, Halmashauri ya Wilaya imetoa eneo kwa ajili ya ujenzi huo, basi tufanyie kazi ili tuweze kuendeleza kwanza wavuvi lakini pia kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Wabunge wamezungumzia hapa na naomba kutoa msisitizo kwenye bandari bubu. Bandari bubu kweli zipo na *TRA* wanafuatilia lakini huwezi kuzihalalisha bandari bubu. Ninachoomba Serikali iangalie, ni kweli Tanga kuna bandari bubu, lakini wananchi watafanya nini kwa sababu wao wanahatarisha maisha yao. Ningeomba zile bandari bubu basi ziangaliwe ili waweze kujua watafanya nini ili waweze kuwasaidia wale wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kweli nisipoongelea Pangani nitakuwa sijawatendea haki. Pangani tuna bahari nzuri na pia ina milango ya bahari ambayo ni mizuri kwa bandari. Serikali ikiweza kuja na *idea* ya kuweka bandari ya kusafirisha wanyama hai, si twiga na tembo, mifugo, kama ng'ombe, mbuzi; tuna soko la ndani lakini tuna soko la nje vile vile na halmashauri inayo maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo. Nina imani kabisa Serikali ikiweza kuja na wazo hili na tukaweza kusafirisha, tunajua tunakataza kusafirisha wanyama hai kwenda nchi nyingine kwa sababu tunapoteza ngozi na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi za wenzetu kama nchi za Uarabuni kama Oman na kwingineko wao kuchinja ni *part* ya ibada na hawana wanyama, kwa hiyo sisi tukiweza kupeleka kule itaweza kutupatia soko na tunapeleka kwa makubaliano maalum. Tunajua Rais wetu alikwenda kule, tunajua Waziri Mkuu alikwenda kule na wao wana imani ikubwa na Tanzania na wana uwezo mkubwa wa kuwekeza nchini kwetu, hapo ndipo *PPP* inapokuja na Mheshimiwa Cheyo analitilia mkazo sana suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba muangalie hapo kwa sababu itaweza kuinua uchumi wa wananchi pale, itaweza kufungua milango ya biashara kwa sababu miundombinu itatengenezwa, vile vile *population* itaongezeka, watu watazaliana, lakini pia na watu wengine watakuja kuwekeza pale na uchumi utakua kwa sababu mzunguko wa pesa utakuwa mkubwa. Ningeomba Serikali iangalie kwenye maeneo hayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Abood, atafuatiwa na Mheshimiwa Kassim Issa na Mheshimiwa Maria Hewa.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru waajiri wangu ambao ni wananchi wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa kushirikiana nami katika kuleta maendeleo Jimbo la Morogoro Mjini kwa miaka yote mitano. Naamini wameona utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi na juhudi zangu binafsi Mbunge. Wameona mabadiliko makubwa katika Jimbo langu la Morogoro Mjini. Ahadi nyingi tumeshazitimiza kwa asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ya Fedha. Pia, niwapongeze kwa kuongeza kodi kwenye sukari, nawapongeza sana kwa kulinda viwanda na ajira ya wakulima. Hata hivyo, nataka niwaambie, viwanda vinavyotegemea malighafi ya wakulima si sukari peke yake. Kuna viwanda vya mafuta, naomba ni-*declare interest*. Kuna viwanda vya mafuta vinavyotumia malighafi ya hapa hapa Tanzania. Vinatumia mbegu za kilimo, alizeti, ufuta, lakini mafuta kutoka nje yanaingizwa bila kodi na mafuta kutoka nje si *crude*, yanayotoka nje ni *semi crude* ambayo *TBS* wameweka kiwango cha *two percent FFA* ambayo ni sawa na mafuta safi tu ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakumbuka wakati Waziri wa Fedha alipokuwa mama yetu Zakia Meghji aliweka kodi kwenye mafuta ya kutoka nje na kilimo cha alizeti mbegu za pamba, karanga zote zilikuwa zinatoa mafuta, ili-*boost* sana, lakini leo angalia kilimo cha alizeti, kimekufa kabisa. Ukienda Sumbawanga alizeti hakuna, Singida alizeti nazo ndiyo hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Dodoma kilimo cha alizeti ukitazama Gairo hakuna, kimekufa. Kwa hiyo, ningeshauri tungerudisha kodi kwenye mafuta ya nje ili wakulima wetu waweze kulima mazao haya ya biashara yakanyanyua kipato chao, lakini sasa hivi tunamnufaisha mkulima wa Malaysia ambaye anaingiza mafuta yake hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mawese, Kigoma, Kyela lakini yanakufa, hakuna soko ni kwa sababu ya mafuta kutoka nje. Morogoro pale kuna kiwanda kikubwa tu cha *MOPROCO* mpaka leo kimefungwa kutokana na mafuta kutoka nje na kinategemea malighafi ya hapa hapa Tanzania. Ajira karibu ya watu 400 mpaka leo inashindikana kupatikana kutokana na mafuta kutoka nje. Kwa hiyo, ningeshauri Wizara ya Fedha, dada yangu najua ni msikivu na manaibu wako wasikivu mliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta ya *crude* yanayotoka nje kama *TBS* wataweka kiwango cha *five percent FFA* hayataagizwa kwa sababu gharama yake ya uzalishaji itakuwa ile ile kama ya mkulima wa hapa ambaye anapeleka kiwandani. Itasagwa, itakamuliwa, itasafishwa, gharama ni kubwa. Kwa hiyo tunaweza tukawabana kwa njia hiyo. Leo mafuta yanatoka nje mepesi tu yanakwenda moja kwa moja kwa walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia nichukue nafasi hii kuhusu viwanda vilivyokuwa mashirika ya umma. Kuna wafanyakazi ambao waliachishwa kazi mpaka leo hawajalipwa, ni miaka 17 sasa, wanazidi kupungua na haki zao hawapati. Ukiangalia kiwanda cha *Politex* wafanyakazi karibu 1,000 mpaka leo hawajalipwa haki zao, ukija kuangalia kiwanda cha Morogoro *Canvas,* sijui kama Mama yangu Nagu umeshalipwa maana ulikuwa mmojawapo pale; mpaka leo hawajalipwa. Kuna Shirika la Mzinga wafanyakazi wake mpaka leo

hawajalipwa. Kwa hiyo, naomba mngeliangalia suala la kuwalipa maana wanahangaika kufuatilia mafao yao lakini mpaka leo wanazidi kupungua  wengine wanakufa haki yao bado hawajapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wafanyabiashara wenye maduka madogo. Ningeomba Wizara mliangalie hili, najua mnalifanyia kazi lakini la muhimu zaidi ni kuangalia kutokana na kuanguka kwa shilingi yetu na hasa kwenye *VAT*. Leo ukihesabu kwa shilingi yetu hata Mamantilie atastahili alipe *VAT* kwa sababu milioni 40 ni kitu kidogo sana kufika kwa mwaka.  Hata hivyo, ningeshauri, ili kuondoa vurugu *VAT* tungeweka hata milioni mia tatu ili tuweze kuwapata wale ambao ni wahusika hasa wa kuweza kulipa *VAT* maana maduka mengi utaona hayafiki milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Jimboni tena. Tuna matatizo ya afya, hospitali yetu ya Mkoa ambayo ni hospitali ya rufaa leo hii *X-ray machine* hawana. Unapovunjika leo Daktari anakupima kwa kukushika kwa mkono ili kujua mfupa wa ndani  umevunjika au haukuvunjika. Hospitali kama hii ya Mkoa leo hii haina *X-ray machine*. Naomba jamani, Morogoro mnaielewa, Hospitali ya Mkoa ipo Morogoro barabara kuu ipo Morogoro, ajali zinapotokea wagonjwa wanashindwa kupiga *X-ray*, hakuna! Leo hata sindano ya kumshonea aliyepasuka hakuna, hali ni mbaya sana. Ningeomba Mheshimiwa Waziri mliangalie hilo la mashine ya *X-ray*, ukikamuakamua huko kununua mashine ya *X-ray* hamuwezi kushindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, Hospitali ya Mkoa wodi ya wazazi ni ndogo, leo kwenye kitanda kimoja wanakaa wazazi wanne, wodi ni ndogo. Kwa hiyo, hilo nalo naomba mliangalie ili tuondoe hii kero ya wazazi maana akiwa na watoto mapacha panakuwa patashika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye sekta ya maji. Tunashukuru tumepata mradi wa maji wa *MCC* uliogharimu karibu bilioni 11 lakini  umeshaanza kazi, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kuja kutufungulia. Hata hivyo, mradi ule hautakuwa na maana iwapo hatukukarabati miundombinu ya maji, ni chakavu sana na hasa miundombinu inayokwenda Kihonda mpaka Mkundi na Lukobe, inayokwenda Nanenane yote imeoza inahitaji kubadilishwa. Kwenye bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri tuliahidiwa mtatupa milioni mia nne, mmetupa sh milioni 100 tu, tunaomba hizo milioni mia tatu tuweze kukarabati miundombinu ili wananchi wa Kihonda, Lukobe na Nanenane waendelee kupata maji, au ule mradi utakuwa wa bilioni 11, lakini hauna msaada wowote kwa wananchi Jimboni Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini dada yangu Saada na Manaibu wako tena bahati nzuri una Naibu Ustaadhi, mtalifanyia kazi hili jamani, mnipe milioni mia tatu zangu zilizobaki za miundombinu ili tuweze kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho narudia tena kuwashukuru wananchi wa Jimboni kwangu naamini wameona kazi nilizokuwa nazifanya na kazi za chama changu, nategemea nitarudi tena Dodoma, naomba wahusika jina msilitoe kwenye vibao mnavyobandika, chokochoko mchokoe pweza CCM huiwezi na Abood Morogoro humuwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abood.  Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Yahya Kassim.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuzungumza machache hii leo. Awali ya yote namshukuru Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Katibu na Watendaji wote kwa ujumla. Kazi aliyopewa siyo nyepesi lakini kwa kweli ukweli uko nje kwamba ni watendaji wanaostahili sifa zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya kuwepo chombo hiki tulichomo ndani ni kila mmoja kuweza kutoa mawazo yake na hakuzuiliwa na ndiyo maana ikiwa siku zote kuna mwenendo wa Serikali kupanga mipango na kupangua, lakini kwa kweli Wizara yetu kipindi hiki bajeti yake haina pingamizi, safi kabisa na naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze katika kitabu hiki ukurasa wa 48 namba 10, napenda kunukuu; kuongeza kiwango maalum cha ushuru wa forodha kwenye mchele kutoka dola za Marekani 200 kwa tani moja au 75 ya thamani ya bidhaa hiyo inapofika bandarini hadi dola ya Marekani 345 kwa kila tani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar chakula chetu kikuu ni wali, si harage, si mtama, si sembe. Mgeni anakuja kwako ukimpia wali kwa kweli itakuwa wewe umemtukuza hata kama yeye ni mlaji wa sembe kwa sababu ndiyo chakula ambacho tunatumia Zanzibar. Sasa hofu yangu, sisi Zanzibar tunaagiza nje chakule chetu, huo mchele wenyewe. Tani kwa tani ukija kule bila shaka utakuta chenga ndiyo chakula chetu. Sasa leo naona iko hatari kwa upande wetu, mchele huu kupanda bei na watu kushindwa kimaisha kwa sababu Mchele wa Tanzania Bara ambao unatumika si mara nyingi, tunatumia lakini si mara nyingi na mara nyingi wanatumia wenye uwezo utaona ndiyo wanatumia mchele huu lakini ule mchele uliokuwa uraufu ambao tunauagizia nje sisi ndiyo mara nyingi watu wanautumia.

Sasa napenda nipate maelezo, sijui mazungumzo yenu Waziri mlizungumzaje na Serikali ya Zanzibar na Serikali ya huku kwa utaratibu ambao wananchi wa Zanzibar hawatapata taabu au hawataathirika au hawatapata mateso kutokana na chakula hicho.

Kuna hatari kisijepanda bei ikabidi watu wanashindwa hata kimaisha na hatari inayokuwepo, ulanguzi unaweza pia kujitokeza. Kwa hiyo, lazima pawe na mawasiliano baina ya Serikali na Serikali ili wananchi wa Zanzibar waweze kunufaika. Kwa hiyo, hilo tunapenda kidogo tupate maelezo juu ya Serikali, taratibu ambazo zilizowekwa kama Waziri wa Kilimo wa huku na Waziri wa kule kwamba wamekutana wakaweza kupanga taratibu ambazo zitastahiki na kufanikisha kuhusu suala hili kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hapa watu wamelalamika sana lakini ni moja katika shughuli zetu kila mmoja namna ya kichwa chake kinapomuandisi na mawazo yake na huwezi kumlaumu inabidi umkubali kwa sababu ndiyo Serikali yenyewe ina hakika inachangia. Hata hivyo, kulikuja kipindi mimi niko Bunge hili, kuhusu suala la mafuta kuchakachuliwa na magari yetu yakaharibika na magari yetu kwenda nchi jirani yakarejeshwa kwamba mafuta kwa kweli hayastahiki. Leo nashangaa watu wanatumia kama siasa ili kuonekana wao wana mapenzi ilihali kwamba Serikali ina nia njema ya kurekebisha mipango hii ili ifanikishe, mimi nashangaa sana. La ukweli tulisemeeni.

Halafu pia leo tunaona kwamba kuna utaratibu mzuri tu hapa uliopangwa kuhusu dizeli na mafuta ya taa, lakini pia kelele zipo nyingi, lakini yeye huyu anayepiga kelele anatumia umeme wa kijijini anatumia kibatari. Leo tunapanga mipango tupeleke umeme na tumeona njia ya busara ambayo hii itakidhi na baada ya kelele nyingi kuhusu umeme baadaye kweli ndiyo una imani na watu wa vijijini? Shilingi ngapi zilizoongezwa hata ikiwa kelele kama hizo? Wakati jambo zuri na lina manufaa; lakini siku zote najua upinzani maana yake ni upinzani,

utamuonyesha vidole vinne atakwambia vitatu, kwa sababu ndio upinzani hawezi kukiri jambo hili. Pia mpinzani siku zote si aghalabu jambo zuri kuweza kuliunga mkono, si aghalabu kwa sababu anajua hili wakati zuri na litaleta mafanikio ina maana yeye hatapata la kusema.

Sasa kwa kweli utaratibu huu uliopangwa na Serikali nauunga mkono kabisa na kwa kweli huu utasaidia na wenzetu kutokana na kukosa umeme. Naamini muhimu mipango iliyopangwa iwe na msimamo iendelezwe vizuri basi nina imani kule vijijini wasiwe na wasiwasi umeme utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna jambo la kudhibiti kodi za mapato. Kwa kweli sisi Tanzania si watu maskini kabisa lakini hatujaweza kujipanga kutokana na taratibu hasa kuweza kudhibiti mapato yetu. Njia za uchochoroni zinatumika sana hata kwa shughuli za uvuvi, mifugo utaona kwamba wavuvi wanaweza kutoka Kigoma lakini wakapeleka biashara zao sehemu za Zambia, Burundi, utaona Serikali vilevile inakosa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kudhibiti kodi hizi za mapato katika bandari zetu kwa kweli wenye uwezo ndio wanaotubana na ndio katika biashara zao mapato hayapatikani vizuri kutokana na mipango sehemu zile za bandari. Sasa naiomba Serikali, suala hili lichukue kila jitihada kuhakikisha kwamba tunadhibiti mapato yetu kikamilifu, hakuna kila sababu na haya ndiyo sababu ya kusema kwamba bila shaka hivi sasa tunataka kujitegemea na misaada tunaiona, hata tukasaidiwa inakuja *too late*. Kwa hiyo kwa kweli *time* nyingine inakuwa lile lengo ambalo tunalipanga hatufanikiwi. Hata hivyo, hakuna sababu kwamba tukijizatiti na tukisema kwamba tudhibiti mapato kikamilifu kwamba hatuwezi kufanikiwa hili suala, naamini kabisa tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru sana na naunga mkono hoja na nawashukuru Watendaji wote na muhimu naomba kwao kuchukua jitihada zaidi ili kuweza kufanikisha mambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Maria Hewa atafuata Mheshimiwa Kasulumbayi na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii finyu ambayo sikuitarajia, lakini Mungu ni mwema nimeamka salama. Naomba nizungumze haya ambayo nitayazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niunge mkono hoja kwa maana ya mapendekezo ya bajeti iliyoletwa mbele yetu. Katika kusema hivyo nimpongeze tu Waziri ndani ya Wizara hii pamoja na Manaibu wake wawili, Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Mwigulu huko aliko azipate tu salama na namtakia kheri na kichwa kizuri ambacho ana uwezo wa kugawa matukio mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kuwakumbuka wanawake wa Mwanza wa Umoja wa Akinamama kuniwezesha kuishi ndani ya Bunge hili kwa awamu mbili. Mimi mwenyewe, najua wenyewe wanajua nawapenda, tena nawapenda na nitaendelea kuwapenda. Hata kama sitarudi wanajua jinsi gani nitaendelea kujichanganya nao katika mapenzi waliyonipa awamu zote mbili. Nawapenda na wenyewe wananipenda, wasingeweza kunipa awamu mbili. Kwanza nikisema sasa basi watasikitika naamini, lakini hebu mapenzi haya kwa wanawake wa Mwanza nayaleta kwao na waendelee kunipenda na yoyote yule kama atakajitokeza

niwaombe wampe upendo kama walivyonipa upendo kama walivyonipa mimi kwa awamu zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea suala la Bajeti. Wengi wamefafanua maana ya neno Bajeti lakini kwa ufupi wake ni pesa, ni pesa. Kwa mtu wa kijijini ukimfafanulia kwamba leo wanajadili bajeti, kwanza neno bajeti sijui ni la Kiingereza sijui kwenye Kiswahili lipo? Lakini kwa ufupi wake ni utafutaji wa pesa kuweza kuiendesha nchi hii na kumaliza kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna mapato ya kutosha tunapoteza muda kuzungumza chochote humu. Wizara hii inapaswa kutafuta fedha kwa udi na uvumba. Ukweli ndiyo huo. Kila awamu na nilikuwa nanong'ona na jirani yangu hapa, hivi mimi wakati naingia 2005 bajeti ilikuwa ya trilioni ngapi, nimeshasahau, lakini leo najua imeongezeka, mapato yameongezeka kabisa, lakini pamoja na kuongezeka huko kila awamu je, tumeongeza huduma kwa wananchi? Kama tumeongeza huduma ni zipi ambazo zilikuwa kero kubwa kabisa kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza humu, kwa mfano, leo tunaongelea kuongezeka kwa kipato cha wastaafu sh. 85,000, watu wameifanyia hesabu mpaka wakajua kwamba kila siku ni sh. 2,600/- kitu kama hicho, wamezungumza hapa. Ukipewa wewe Mbunge utasema mimi nina kazi nyingi mno, hivi wenyewe hawana kazi nyingi? Niombe, ombi langu kwenu Serikali, Ombi langu kabisa Mheshimiwa Waziri hebu tutoke hebu tutoke hapo kwenye 85,000/- tena afadhali ilivyokuwa ikisomeka 50,000/- inapendeza hata kuandikwa, 85,000/- haipendezi. Twendeni hata kwenye laki moja; unajua hata ile tu kutamka laki atapumua mzee huyu mstaafu kama kweli tuna nia ya kuwajali hebu tumpe mara mbili yake atajisikia vizuri mno. Atasema sasa hivi afadhali kidogo tunapewa, tena huwa hawasemi laki tu, wanaweka kalaki.

**MBUNGE FULANI:** Kisukuma, Wasukuma hao!

**MHE. MARIA I. HEWA:** Wananiambia eti tunasema kalaki kwa sababu sisi fedha kwetu si lolote tunajali ng'ombe, ndiyo! Hebu tutoke hapo, 85,000/- haipendezi mpaka akatafutiwe chenji ya 5, sitaki, apewe, zihesabiwe noti nyekundu zile kumi atajisikia vizuri. Tutoke 85, tuongeze 15 tu ziwe 100,000/-. Bado wananiambia ni ka-laki, eee, kadogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yakiwa mazuri tunafuta hata kutoa hata hizi za Walimu, tuna matatizo kwelikweli tudhibiti vyanzo vyetu vya mapato jamani. Trilioni ishirini na mbili ndizo tunazozitarajia. Je, zinaweza angalau zikapunguza matatizo haya ya Walimu? Je, zinaweza zikakidhi kupata dawa hospitali? Je, zinaweza zikakidhi angalau tukachonga madawati ya kutosha, je zinaweza kukidhi angalau Jiji la Dar es Salaam likafunguka? Ni kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku nimetoka hapa Dodoma kwa basi kwenda Dar es Salaam niliingia saa sita za usiku nilikokuwa nakwenda. Jamani tuwe tunafikiria haya, vyanzo hivi vya mapato Watanzania wanakero kama ninazozitaja jamani, kero kabisa, niliingia saa sita utadhani nimetokea Mwanza kumbe Dodoma. Jamani, je, trilioni ishirini na mbili zinaweza kuifufua Reli ya Kati ambayo sisi wa Kanda ya Ziwa huko ndiyo raha yetu kuona treni inafika bila matatizo? Je, trilioni ishirini na mbili zinafanya shughuli ipi au *priorities* zenu ni zipi jamani, Watanzania wakatuelewa tulikuwa wawakilishi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya kwa kweli kwa machungu. Mtu akisikia trilioni ishirini na mbili wanaziona ni nyingi, kwa kusikia tu ni nyingi, lakini basi haya ni kidogo kwa nchi kama Tanzania. Lakini niseme, zikidhibitiwa katika haya niliyoyataja angalau basi Wizara itasimama itasema, tulitafuta mapato tukapata na zikatumika, maana tatizo kubwa pia ni

matumizi. Ukiuliza kwenye Halmashauri mpaka baada ya robo ya mwaka hawajapata hata shilingi. Mimi nilikuwa kiongozi wa Halmashauri nalijua hili. Ukiuliza ni nini unaambiwa Hazina. *What's* Hazina? Hivi Hazina mnawaogopa nini? Huwa mnatutajiaga Hazina *link* yenu na Hazina ni mbaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema ushauri wangu ni kwamba tulishapitisha azimio la kila robo ya mwaka kwa wale watakaorudi mlilisitize hili Wizara kutuletea mapato na matumizi ili tuone *trend* ya ukusanyaji na matumizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kutatua usugu wa Hazina. Narudia muwe karibu, lenu liwe moja. Hatutaki kusikia ni Hazina halafu Halmashauri zinateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo nalisema kwa uchungu. Jamani kanda ya ziwa mmetusahau. Tumeomba viwanda angalau kimoja tu kanda ya ziwa tunaambiwa hakuna malighafi za *cement*, ikitajwa *limestone* eti iko chini sana. Hivi hatuna ubongo wa kufikiria kutoa hiyo *limestone* chini huko na sisi tukapata kiwanda? Mawazo yetu ni tuikute juu juu? Vyote hivyo viko Pwani, Dar es Salaam na Tanga tu, lazima tugawane huduma hizi muhimu. Mwanza mmetuonea mno. Tulipata kiwanja hapo wakasema eti hatuna maeneo. Tukawapa Shinyanga, hamkutaka kutupokea. Iko siku mdharau mwiba. Naendelea, angalau basi mtufuatilie viwanda hivyo ambavyo karibu vyote vimekufa kanda ya ziwa. Mwanza kila kitu, si *MWATEX* tu tulikuwa na viwanda vya kutengeneza mambo mengi tu *Voil, Glass* na nini na nini, mambo mengi tu na ngozi mmebadilisha matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa uchungu kanda ya ziwa kila tunachoomba hakuna. Mkipata mradi mnaupeleka kwingine kwa vipi? Narudia huo msemoi wangu mdharau mwiba mtakuja kutukumbuka siku moja kwamba Mama Hewa alisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hata umeme wa hapo Singida nao nilizungumza humu na sisi wa karibu tungepata hata masalia yake na wenyewe umepigwa vita. Naomba mtukumbuke kanda ya ziwa kwa miradi tunayoomba. Hata tunapoomba kikanda tunanyimwa, kwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo lakini nisisitize mapato tunayoyapata yaende kwenye matumizi ya kumaliza kero hasa hasa nimetaja sitaki nirudie, zimerekodiwa kero za wananchi ninayoyazungumza hapa, lakini mkumbuke mahitaji hata walau kikanda. Kanda ya ziwa mmeisahau mno hata barabara za lami sisi tumepata wa mwisho. Mbona sisi mnachimba dhahabu, mnachimba almasi, mnachimba nini maendeleo yanatumika nchi nzima sisi tupeni walau kiwanda cha *cement,* lakini kiwanda kimeenda Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishia hapo kwa machungu makubwa, hatujitengi lakini sisi si Chama ambacho kinazungumzia kujitenga, lakini kwa ujumla wake tukumbukeni na sisi kanda ya ziwa maana mafanikio Kitaifa yapo sijakataa, lakini inapofika wakati tunataka hitaji hatupati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishia hapo, lakini nimpongeze mwanangu kwa hili ambalo umelisimamia pamoja na vijana wako kwa maana ya kile kitakachopatikana kutokana na mafuta, kile ulichoongeza *so long as* ni umeme hata Wasukuma wanauona.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Ahsante kwa kunisikiliza.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipatia nafasi hii. Nianze kumshukuru Mungu namna alivyoniwezesha kuwa na afya inayoridhisha. Niwashukuru pia wapigakura wangu wa Jimbo la Maswa Mashariki. Niwashukuru sana kwa namna wanavyonipa ushauri, ushauri ambao unanifanya kuwa imara katika kuisimamia Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Niwashukuru pia viongozi wangu wa CHADEMA, Nashukuru Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa namna ilivyoweza kuelekeza namna bora inavyoweza kuwasaidia Watanzania kuondoka kwenye hali hii mbaya ya kuwa wanalialia kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku ya leo nitazungumza baadhi tu ya mambo ambayo yapo kwenye bajeti na nitaanza kuzungumzia suala la mafao ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imekuwa na mbinu ambazo zinawavuta wazee ili kuwaonyesha kwamba Serikali hii inawajali wazee na imeleta hoja kwamba itaingiza mafao au pensheni kwa ajili ya wazee lakini wakati huo huo inashindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Cha kushangaza Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2010 alikutana na wazee kwenye Sikukuu ya Wazee DUniani mjini Morogoro; aliwaambia kwamba Serikali yake itafanya mkakati wa haraka kuhakikisha pensheni ya wazee inapatikana; lakini baada ya mwaka huo wa 2011 wazee hao mpaka sasa hivi kwa mujibu wa bajeti inaonesha Serikali bado haijajua hata idadi yao, kwamba hawa wazee inayozungumza itawapa mafao wako wangapi. Wakati sensa ya mwaka 2012 inaonyesha kabisa kwamba tuna wazee katika nchi hii zaidi ya milioni mbili na nusu, lakini leo hii unaambiwa kwamba sasa wanaambiwa wasubiri mwaka 2016 kwa sababu Serikali inafanya mchakato wako wangapi ili iweze kuweka mafao au pensheni yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado haijasema hawa wazee inayowazungumza ni wazee wa aina gani. Je, ni wazee waliotumikia Ikulu au ni wazee waliotumikia Serikali au ni pamoja na wazee wa Ikulilo, Sangamwalugesha na maeneo mengine ambao wao hawajafanya kazi Serikalini bali wamezalisha ng'ombe, wamelima pamba, pamba ambayo imesaidia sana kujenga uchumi wa nchi hii. Je, katika hayo mafao hawa wazee wa Ikulilo na Ikungulyakoma na wao wamo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kweli Serikali ina mkakati huo basi ihakikishe wazee wa aina zote, wahunzi, wajenzi wavuvi na wengine ilimradi kwamba wameshafika kwenye sifa ya kuitwa wazee waweze na wao sasa kuishi vizuri. Kama hili hatulioni chanzo kingine kikubwa kinachosababisha watu kuhujumu uchumu wa nchi hii ni jinsi wanapokuwa ofisi wanafikiri hali za wazee zinapokuwa mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtu anaamua kuanza kujilimbikizia kabla ya uzee haujampata kwa kujua kabisa kwamba hayapo maandalizi ya kumwandaa mzee huyu atakapokuwa ameishiwa nguvu aweze kuishi vizuri kwa kujua nchi yake haina utaratibu. Kwa kuwa hatuna utaratibu ndiyo maana hujuma zinakuwa nyingi kwa sababu watu wanajiandalia mapema ili haya yasije yakawapata yanayowapata wazee wa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda ukaangalie hospitali wazee wanavyohangaika kutafuta huduma, analazimika mzee wa watu huyu kutokwenda hospitali kwa sababu ataambiwa kama ni dawa nenda kanunue kwenye duka la fulani wakati hata uwezo wa kutafuta hiyo hela hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la wafugaji. Mimi ni sehemu ya watu wanaoishi kwa kutegemea mifugo kwa hiyo, nalizungumzia sana. Tanzania ilijaliwa sana kwa

kujikuta watu wake wanakuwa ni wafugaji. Kama ningekuwa mimi ndiyo naiongoza hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ningesema hivi, wafugaji tayari ni wawekezaji wa ndani moja kwa moja kwa sababu wafugaji hawa wana mtaji, kinachopungua kwa wafugaji ni nafasi ya kupewa uelewa tu wa namna gani mifugo hii waweze kuiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama kweli ni sikivu kama inavyojiita, basi ingesikia. Wenzetu Serikali ya Ethiopia ambao wana ng'ombe wengi kuliko ng'ombe tuonafuga sisi. Sisi ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika; Ethiopia ndiyo nchi ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa sisi ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika, tunaona ng'ombe ni kero mpaka tumefika mahali tunasema ng'ombe ni chanzo cha uharibifu wa mazingira, wakati ng'ombe ndiyo wanaoleta kila kitu. Wewe unayezungumza hivyo, kiatu ulichovaa ni cha ngozi; kibegi kile cha akinamama ambacho wanaita kipimajoto, ni ngozi ya ng'ombe; lakini bado hutambui kwamba umeweka chanzo kibaya kwenye kwapa lako kinachotokana na ng'ombe unayemwita ni mbovu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Waethiopia kwasababu wanawajali wafugaji, Ethiopia wameamua kuwaita Wachina; na kwa urafiki wao wenzetu wamewajengewa kiwanda ambacho kinatengeneza viatu vya akina mama, ambacho mauzo yake ukisoma taarifa inaonyesha kuwa watapata Dola bilioni nne. Kama ingekuwa hiyo Dola bilioni nne Dola bilioni nne ni yetu Tanzania hapa, maana yake ni sawasawa na Shilingi trilioni saba za pesa ambayo ni nusu ya bajeti ya Serikali yetu hii. Wenzetu kwa kutambua ng'ombe hawampuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi kama ya kwetu na Serikali hii inayojiita makini, inamtambua ng'ombe kuwa ni chanzo cha uharibifu wa mazingira na matokeo yake inashindwa kujenga miundombinu ya mifugo kwasababu ya fikra mbovu iliyoko kwamba ng'ombe ni chanzo kibovu. Kwa hiyo, imeshindwa hata kutoa iundombinu kwa ajili ya kumwendeleza huyu ng'ombe.

Kwa mfano, taarifa ya mwaka 2014/2015 inaeleza kabisa kwamba mifugo ilitengewa bajeti ya bilioni 24 na ushee, lakini matokeo yake mpaka kuja kufika mwezi wa Nne mwaka huu, pesa zilizokuwa zimetolewa ni bilioni tatu kutoka kwenye bilioni 24. Ni aibu! Matokeo yake, haitawezekana kujenga miundombinu kwasababu ya dharau hii. Ng'ombe anatengewa bilioni 24, lakini zinazotolewa ni bilioni tatu. Hata hizo bilioni tatu zilizotolewa kabisa zikaenda kwenye Idara husika ni bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni mizaha! Utaweza kuboresha ufugaji kweli katika staili hiyo? Tutaweza kuondoka kwenye shida hii? Matokeo yake, kila mmoja ananuna anasema, ng'ombe ni chanzo cha uharibifu wa mazingira. Inawezekana vipi? Ng'ombe ambaye ni mnyama mtakatifu, hata wengine anajua! Hata Bwana Yesu alizaliwa kwenye pango la ng'ombe kwasababu ni mnyama pekee ambaye ni mwaminifu na mtakatifu! Wenzetu India wamefikia hata hatua ya kumwabudu, leo wewe unamwita ng'ombe ni chanzo cha uharibifu wa mazingira!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe ni M-Pesa, ng'ombe ni Tigo Pesa, ng'ombe ni wakati wowote unambadilisha anakuletea maisha mazuri. Wewe unakuja hapa unamdharau ng'ombe! Chezea vitu vingine, usichezee ng'ombe! Ng'ombe ndiyo rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kama Serikali kama kweli Serikali hii ina watu makini, nimemwona Naibu Waziri wa Fedha, ameitwa Ustaadhi, amsikilize basi amshauri huyu mama. Najua mama ana huruma kuliko mtu mwingine yeyote. Ndiyo maana hata ukiumia tu

unasema mamaa! Unamkumbuka mama. Sasa Mama Saada kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, japokuwa tunapowaambia mmechoka, mnachukia! Hivi ni kwa nini usikubali kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imechoka kama ina rasilimali hizi na inashindwa kuzitumia? Unashindwa hata kuiga kwa wenzako!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzako Ethiopia, urafiki na Wachina wameuingiza ili wawajengee miundombinu ya kurutubisha mazao ya mifugo. Wewe umeshindwa kujifunza hilo? Mmeshindwa na mna wataalamu! Kuna Wabunge hapa wanaposimama wanazungumza kabisa kuwa wao ni wasomi. Mimi nashindwa kuelewa usomi wa hawa Wabunge wanaokuja humu ndani wanazungumza wasomi, wanashindwaje kuishauri Serikali hii ili tuweze kuondoka kwenye nafasi hii mbaya ya kuwa masikini? Sisi siyo sehemu ya watu wa kwenda kuomba misaada. Tunajitosjelaza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro wa wafugaji pia kuhusu malisho. Mimi natoka Maswa. Huko Maswa kuna eneo linaitwa *Shishio Holding Ground*.

Eneo hili lilikuwa linatumiwa sana na Kiwanda cha *Tanganyika Parkers* kipindi kile. Lina ukubwa zaidi ya hekta 21,000 eneo hili limewekewa miundombinu mikubwa na tena lilitengenezwa na Wakoloni ambao walikuwa ni makini, wakatengeneza miundombinu, wenyeji wa pale wakaondolewa, ili liweze kutumika, ng'ombe wote wanaokusanywa waweze kunenepeshwa, waandaliwe tayari kwa kupelekwa kwenye kiwanda cha *Tanganyika Parkers* kwasababu wenzetu Wazungu wanahitaji hata wakipokea nyama wanaangalia huyu ng'ombe ametunziwa eneo gani.

Kwa hiyo, eneo lile ni fursa nzuri. Wafugaji wa Wilaya ya Maswa baada ya *Tanganyika Parkers* kufa waliamua kuliomba lile eneo ili na wao sasa waweze kuwaingiza ng'ombe wao mle wawanenepeshe ili wajiandae kuwauza ili waweze kutoka katika nafasi ya kuzurura na kutembea na baadaye wanaitwa wafugaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili pamoja na kwamba wameliomba, nami kama Mbunge nimejitahidi sana kumwona Waziri wa Mifugo, akaniahidi kwamba kweli anaweza kuwapa hao wafugaji wa Kisukuma walioko Maswa ili waliendeleze eneo lao. Cha ajabu, mpaka hivi sasa ninapoongea, eneo hilo la *Shishio Holding Ground* tayari amewekewa mtu mmoja anaitwa Mwekezaji kutoka Zanzibar. Sasa hii maana yake ni nini?

Huyu mtu ambaye kila siku unamlaumu anatembea na ng'ombe na ng'ombe wamekonda na yeye amekonda, leo amekwambia basi alitumie hili eneo ambalo ni haki yao, wewe unamweka mwekezaji! Kwa nini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inashindwa kuwaamini walioko kule na badala yake inapenda watu wengine kutoka sehemu nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Hivi kweli sasa tutamwondoa kweli huyu Msukuma kuzurura na ng'ombe wake kila siku? Anapotembea, mnasema anavuruga mazingira. Atashindwaje sasa kutembea, kwasababu asipotembea hawezi akala! Hawezi kupata riziki! Waswahili wanasema heri mtembea bure kuliko mkaa bure. Hawezi kuendelea kukaa kwenye eneo ambalo tayari anaona riziki yake anashindwa kuipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Serikali yako, ninaposema Mwenyekiti maana ni walewale ambao ndiyo hao inakuwa ni ngumu kusikia. Naomba kwa sauti hii, msikie, mkae na mjiulize, kwenye hii bajeti ambayo tunaizungumza, angalau basi ianze kuleta mabadiliko katika nchi hii. Vinginevyo Kambi ya Upinzani imefanya kazi kubwa sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimeshangaa hao ambao wanaumuka kujikuta wako kwenye nafasi ya kutafuta ugombea; kuna mgombea mmoja wa Chama cha Mapinduzi, katika kutaka kujinadi, yeye amesikia Dkt. Slaa ameenda Ulaya huko. Kwa sababu Ulaya kule kuna mahojiano, akahojiwa, akaeleza rushwa ilivyoshamiri kwenye nchi hii. Sasa huyu mgombea wa Chama cha Mapinduzi anayetafuta Urais, akaona eti hiyo sasa ampandilie Dkt. Slaa aonekane haifai. Anasema, huyu sio Mzalendo kwa sababu mambo ya ndani anaenda kuzungumza kwingine. Hivi wewe unaweza kuvumilia kuweka mkaa wa moto kwenye suti yako? Unaweza? Unaweza kwasababu eti ni mzalendo, ni heri uendelee kuwa na mkaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni msema kweli kwasababu jirani yako ukimueleza kinachokuzunguka, kinachokubana atakuongezea mbinu ya namna ya kupata utatuzi. Siyo uzalendo wa kuficha makosa! Huo siyo uzalendo; ama umasikini, siyo uzalaendo! Uzalendo haupimwi kwa kigezo cha kuvumilia migogoro. Mimi kila siku nawaambia chenye uwezo wa kuweza kuvumilia chochote kile, ni mdomo wa koroboi tu! Mdomo wa koroboi hata ukichomeka namna gani, hauwezi kujitetea kwasababu hiyo ni koroboi. Lakini binadamu anapaswa apige kelele maeneo ambayo anaona mambo hayaendi vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SYLVESTER M. KASUMBAYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda umeenda...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasulumbayi. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Margareth Mkanga na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Sabreena Sungura.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu kwasababu ndiyo inayopanga kwamba tutaendaje na tutafikaje kwa mwaka wa Fedha ujao wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameniwezesha kuwepo hapa leo vizuri, sijambo. Lakini nitoe masikitiko yangu na huzuni kuwa juzi ilikuwa ni Siku ya Watoto Duniani na Tanzania tuliadhimisha kwa malengo muhimu mazuri. Hata hivyo, siku hiyo hiyo ndiyo ukatili ulijidhihirisha kwa mtoto *Albino* ambaye alikuwa anauzwa na Mjomba wake huko Tabora lakini kwa rehema ya Mungu raia wema walitoa taarifa hiyo na yule katili, dhalimu akawekwa mikononi mwa Usalama, yaani alikamatwa. Nina tumaini hapo haki itatendeka kwa mtuhumiwa huyu kusikilizwa ni kwa nini alifanya hivyo na hatimaye apate adhabu inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba ukatili wa watoto hasa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi unazidi kuendelea nchini, tatizo sijui ni nini! Sijui wanadamu tumeshakuwa na unayama wa aina gani kiasi kwamba wenzetu hawa afadhali wacheze na simba kuliko binadamu mwenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalaani kitendo hiki na ninaomba wananchi, ulinzi kwa watu wenye *Albinism* siyo wa wazazi peke yao, tushirikiane kama wenzetu hawa wa Tabora walivyoweza kushirikiana na kumtia mtu huyu hatiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo napenda kuwashukuru. Kwanza wanawake wa Mkoa wa Morogoro na wanawake wote wa Tanzania hii kwa kuniwezesha kuwepo hapa na kuweza hasa hata kutetea, kama hili nililolisema la mwanangu huyu *Albino* ambaye kwa kweli ilikuwa almanusura aingie sasa katika midomo ya simba kuuzwa, kuuawa na kuchukuliwa

viungo vyake. Wameniwezesha kuwa ni mtetezi makini wa masuala ya watu wenye ulemavu humu Bungeni na nje ya Bunge. Naamini uamuzi wao wala sijauaibisha, wala sijautania, nimeufanyia kazi kwa jinsi Mungu alivyonielekeza pamoja na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Taasisi ya Bunge kuanzia Spika, Naibu Spika, Wakurugenzi na wote kabisa. Nimeishi kama nyumbani vile! Kwa upande wangu nimejitahidi kuishi vizuri tu na wenzangu, mpaka unasema ooh, jamani haya mambo yaendelee kuwepo tu, *inshaalah* Mungu akitujalia yataendelea kuwepo. Kwa sababu nimetunzwa, nimesaidiwa, maafande hapa mara watoe kiti, waweke, yaani mpaka unajisikia wala huna tatizo kati ya wenzako; na wamekukubali! Mungu aendelee kuwahifadhi na mioyo hiyo ili wenzenu sisi wenye ulemavu tuendelee kujisikia kwamba tuko pamoja na wala tusiwe na wasiwasi. Ulemavu siyo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mama Saada Mkuya namfahamu kwasababu Kamati yangu ambayo nilikuwa nayo ya Uchumi, Viwanda na Biashara, mbona fedha ndiyo tunaziangalia huko! Nilimwona uwezo wake ndani ya Kamati jamani! Ni Mama bado mbichi tu na Mungu amsaidie, lakini kwa kazi ni hodari. Huyu akisimamia kitu, hata mfanye nini, Mheshimiwa Saada atasimama na hilo mpaka mtakubaliana naye kwamba kweli, maana yake anajenga hoja na ikaeleweka hata ndani ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Saada Mkuya siyo peke yake, na wasaidizi wake; Mheshimiwa Malima na Mheshimiwa Mwigulu wamekuwa ni msaada kwao na Wizara ukiona inaenda vizuri, unatambua kwamba wao watatu au wanne kwa kweli mambo yao wanakubaliana wanaenda vizuri. Hawa kwa *pair* hii ambayo ipo sasa, kwa kweli mambo yao yalikuwa ni mazuri kwasababu walikuwa wanakubaliana katika mengi na hayo tuliwaona wakifanya ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, nawapongeza mmeandaa bajeti yenye mwelekeo wa kujitemea; na ni bajeti ya kimageuzi sana. Nakumbuka ndani ya Kamati tumeendelea kushauri kwamba jamani muwe na vipaumbele ndani ya vipaumbele.

Nashukuru hili Wizara mmelielewa. Safari hii mmekuwa na vipaumbele vichache ambavyo Mungu akitusaidia kweli kutimiza trilioni 22, baadhi ya mambo mengi yatakuwa yamepata utatuzi. Changamoto hizo mnazijua na ndiyo maana mkasema kwamba ni lazima mkamilishe miradi inayoendelea bila kuianza mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu kwa hela hii, kwa nchi masikini kama sisi tukamilishe kabisa miradi ile ambayo tayari tuliianza; ujenzi wa reli, viwanda vya Mchuchuma, barabara sijui kufanya nini, *flyover* za Dar es Salaam, Hospitali na nini, Maabara, Afya (Zahanati)! Kwa kweli tukamilishe kwanza hivyo, halafu mnaanza kingine. Ndiyo maendeleo, lakini tukijichanganya sana, huenda pesa hizo zisingeweza kukamilisha mambo ambayo tumeyadhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana na dhamira ya Serikali kuondoa kodi katika bidhaa muhimu; pembejeo, vifaa tiba na mengineyo yote. Nami hapa nazungumzia zaidi kwenye vifaa tiba, Naamini watu wenye ulemavu hapa tutafaidika zaidi. Kwasababu kwa muda mrefu sana nimelalamika au nimeshauri, jamani vifaa vile bandia, ni ghali mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikiondolewa malighafi zake kodi, ninaamini kuwa vifaa hivi sasa watu wengi wenye ulemavu watamudu kuvinunua kama pale *MOI* au kokote kule, na kujitahidi kuendelea maisha yao wakiwa angalau na msaada wa vifaa hivyo kama mikono ya *artificial;* miguu, haya mavyuma, tunaweza tukayamudu endapo hili litawezekana kufanyika.

Katika kupunguza kodi katika maeneo haya, ninaamini wanunuzi wa aina mbalimbali watapa ahueni kwasababu kodi zitakuwa zimepunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla, yasiwe ni maandiko lakini vitendo vionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara pia kwa kujitahidi kabisa na kuahidi kudhamiria kulipa malimbikizo ya madai ya Makandarasi, Wazabuni, Watumishi wa Serikali, Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema na ni muhimu kabisa kwasababu kwa kufanya hivi, itasaidia kimatendo maeneo haya yote watu kuweza kujiendeleza. Makandarasi ambao wana madeni; Wazabuni ambao wengine wameshafariki, wastaafu watakaopita kwa *PPF* na *PSPF* na mengine yote; kwa kweli hii ni dhamira njema, tena ninaomba kabisa hapa, kila hela itakayopatikana kwa ajili hii hapa iwe *ring fenced* na watu hawa waweze kulipwa hizi fedha haraka iwezekanavyo baada ya makusanyo yatakavyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni ya Wazee imezungumzwa mno na sisi hapa wote tunakwenda huko huko. Tusipojiandalia makao mema, tusije kulalamika kwamba ooh, mbona! Mbona! Kwa sababu sasa unajiona ni kijana lakini baada ya muda unakuwa mzee. Tuelewe kama wenzangu walivyosema, hawa ndio waliolijenga Taifa hili tukalipokea hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuandamana na hili, nasikitika sana. Wazee hawa Sera yao ilitungwa toka mwaka 2003 lakini mpaka leo hii Sheria ya kutafasiri Sera hii haijatungwa. Sasa haya mengine tunayowashauri kuhusu wazee, laiti kama Sheria ile ingekuwepo, yangekuwa yameanza kujitatua yenyewe Kisheria. Hata hivyo, mpaka hivi leo Sheria hakuna; Sera ile kutafisirika kimatendo, ndiyo hivyo, mtu anafanya apendavyo kwa sababu hakuna *Law* ambayo ina-*enforce* ukweli wa mambo yaliyoko. Hivi kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sasa Serikali ijayo hebu basi iwe *number one* kulikamilisha kusudi wazee kama wenzangu walivyozungumza kwamba ni 85, mimi nilisema hata kalaki na nusu hivi, wanaweza kujisikia sawasawa. Kwasababu katika hali ya uzee changamoto zinakuwa ni nyingi; maradhi, wanapenda chai ya sukari na nini. Sasa haya watayamudu vipi na wengine hawana hata wa kuwalea? Siyo wote wanalelewa, wengine wako kwenye makambi haya ya wazee; nayo ni matizo matupu! siyo kwamba wanakwenda kule kwa kupenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ukiwepo katika familia yako, ukaweza na wewe kujitegemea na kusaidia, unaheshimika zaidi. Kwa kweli tunapaswa kuwalea na kuwatunza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulizie jambo moja. Uendeshaji na ugharamiaji wa Baraza la Watu wenye Ulemavu nchini, ambapo suala hili liko kwenye Sheria ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2010. Baraza hili Kitaifa limeishaundwa toka Novemba, 2014, lakini halijaweza kufanya kazi mpaka leo kwasababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu, ndani ya bajeti hii, kupitia Wizara ya Afya ambapo ndiyo wanasimamia, ni kiasi gani kimetengwa ili kuendesha Mabaraza haya? Kwa sababu Mabaraza haya ndiyo yatakayokuwa yanatoa ushauri kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu na yanapaswa kuwa mpaka ngazi ya Kata. Hivi hapa tunaendaje? Naomba kabisa kwa sababu ushauri wa masuala ya watu wenye ulemavu ndipo yatakapotokea na kisheria ndiyo tumefanya hivyo? Fedha zipatikane kusudi Mabaraza haya yaanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kuhusu umuhimu wa tozo ya mafuta kwa ajili ya kugharamia Mfuko wa Umeme Vijijini. Mengi yamesemwa kuhusu mafuta ya taa kupanda. Kwa mawazo yangu nilikuwa nafikiri hivi, jamani eeh, Jeshini kuna usemi, "toa jasho jingi sana wakati wa amani, kwa kujiandaa na nini ili utoe jasho dogo wakati wa vita." Hili ndilo ninalolinganisha hapa, kwamba haya ni maamuzi. Kwetu yatakuwa magumu na machungu, kwamba inabidi tutoe tozo hizi, lakini kama Kamati husika ilivyosema, waliangalia faida na hasara, wakakuta faida ni nyingi sana.

Kwa hiyo, nawaomba wenzangu, hili kwa uchungu tuliridhie, kwa sababu wakishamalizia, *REA* wakapata kweli fedha hizi, umeme ukaenda Vijijini, wakashushwa bei, wazee wakawa na uwezo wa kutumia umeme na majiko ya umeme yakashuka bei, kila mtu akaweza kutumia fursa hii, kwani macho mekundu yatapatikana kutoka wapi? Kwani sasa wataendelea kukata miti kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maendeleo haya! Ni uamuzi mgumu lakini wenye manufaa. Tujue kwamba katika kuiendeleza nchi, mengine yatakuwa machungu, lakini baadaye ni sukari! Mimi ndiyo hili ninaloliona hapa. Kwa sababu umeme vijijini utakuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo. Kompyuta mashuleni tunataka, majokofu badala ya mafuta ya taa yatakuwa ya umeme, watoto wetu watapata chanjo sawasawa. Mashine za kusaga zitakuwepo, kuranda mbao, kuvutia maji, kila kitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yatakuwa yanarahisika jamani kwa kutumia umeme kama mzee wangu alivyosema, waa, unawasha tu, mambo yanawezekana. Hata wazee katika kujihudumia upishi, itakuwa kwao ni rahisi, lakini umeme huu ni lazima uje ushuke bei na vifaa vinavyotumia umeme ni lazima vishuke bei ndiyo iwe manufaa zaidi kwa wote wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara, imetoa agizo kwamba Taasisi za Serikali na Serikali yenyewe iweze kulipia Bima kupitia Shirika la Bima ya Afya. Hii nayo ni muhimu, na tutaongeza mapato. Kwa jinsi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti suala la Bima limekuwa ni njia mojawapo au uchochoro mmojawapo kwa kweli wa pesa za ndani kutoroshwa kwenda nje. Kwa sababu kunakuwa na mikataba ya masuala ya Bima mtawanywa, ambapo *literally* pesa za makampuni binafsi zinapelekwa nje huko. Hapa nchini tuna mashirika mawili tu ya kiserikali ambayo ni yetu, lile la Zanzibar na hili la *NIC* yetu hapa.

Kwa hiyo, kwa kweli naipongeza Serikali kwamba imetoa agizo kwamba mashirika yake na Taasisi zake zilipie Bima kule. Hii itasaidia Shirika letu la Bima au yote mawili kuimarika na kuweza kuchangia pato la Taifa kwa kupitia kodi na gawio kwa Serikali, mambo ambayo kwa sasa hayafanyiki. Kwa sababu tuna mashirika ya Bima binafsi kama 29 hivi. Ingekuwa hii kazi haina faida, pasingekuwa na mashirika binafsi mengi kabisa hapa nchini. Tunapoteza fedha, tunapunguza nguvu ya uchumi wetu, kwa kuruhusu au kwa kutokuwa na mpangilio mzuri wa hata sisi wenyewe kutumia mashirika yetu ya Bima kufanya kazi na biashara iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa, *NIC* ilikuwa na matatizo, lakini kwa sasa hivi kwa kupitia Kamati yetu, tumeelezwa kabisa na tumepata Mkurugenzi ambaye kwakweli ana maono, anajitoa, mzalendo na anajitahidi kuliimarisha na kulifufua hili.

Kwa hiyo, naomba kabisa na nitoe rai hapa, jamani kama tulikuwa na *Phonex* sijui wapi, hebu turudi tukikuze chetu! Tunalalamika hapa kwamba tunategemea sana nje, vyetu

tunavidharau, ni pamoja na Shirika la letu la *National Insurance Company*. Tuikuze, tupeleke huko biashara ili kwa kweli pesa zile ziweze kubaki humu ndani kwa ajili ya faida ya wote ambao tupo na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naendelea tu kwakweli kuipongeza Serikali na Wizara. Mungu akiwajalia kurudi waendeleze kazi hii kabisa ya kuweza kutusaidia katika masuala ya fedha na ukusanyaji wake; lakini pia waendelee kushiriki au kuhangaika kuziba mianya ya pesa hizi tunazokusanya ziweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Margareth Mkanga. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Sabreena Sungura. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia katika bajeti ya Serikali na mpango wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya kwa kuweza kutumikia wananchi wangu kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwakuwa tumeanza Mfungo Mtukufu wa Mwezi wa Ramadhani, napenda kuwatakia Watanzania wote kwa ujumla hususan wananchi wa Mkoa wa Kigoma, Ramadhan Karim na *Swaum Maqbul! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, Marehemu Mheshimiwa Eugine Mwaiposa. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi na aipe subira familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuchukua fursa hii kukishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo hususan Katibu wangu Mkuu Dkt. Wilbrod Peter Slaa na Mwenyekiti wangu wa Chama Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa ukarimu wao wa kunipa nafasi ya kuwakilisha wanawake, lakini pia kuchagulia kama Naibu Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nashukuru sana na ninaamini sikuwaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa ni mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wanawake wa Mkoa wa Kigoma kwa fursa adhimu walionipa. Nawashukuru sana, Mwenyezi Mungu awajalie heri nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukurani za dhati kwa familia yangu, baba yangu mzazi Mzee Hamza Sungura na mama yangu Rehema Rubibi, kwa ushirikiano na ushauri ambao wamekuwa wakinipa kwa takriban miaka mitano; bila ya kumsahau Katibu wangu wa Ubunge Mheshimiwa Omary Gindi, lakini na dada yangu mpendwa, Mariamu Sungura ambaye amekuwa kwa hali na mali akihangaika katika kunisaidia katika majukumu yangu. Mwenyezi Mungu amjaze heri nyingi sana hususan katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Serikali, kuna mambo ya msingi ambayo ningependa kuzungumzia. Suala la kwanza ni suala la maji. Ukiangalia bajeti ya maji kwa

mwaka tuliomaliza, fedha ya ndani ilitolewa kwa asilimia 27 tu na fedha ya nje ilitolewa kwa asilimia 33 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mwanamke na Naibu Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, suala la maji linatuumiza sana. Vijana wetu wamekuwa wakibakwa, wakienda kutafuta maji usiku na akina mama wengi wamekuwa wakivunja ndoa zao kwa suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati yako imefanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, tulikuta pale fedha za maji Shilingi milioni 300 zimeenda kutumika kwenye matumizi ya kawaida, wakati fedha hizi zilikuwa ni fedha za maombi maalum. Suala hili lilileta utata na ukizingatia Wilaya ya Kasulu ina shida kubwa sana ya maji. Kwa hiyo, tungependa Serikali iwe inachukua hatua madhubuti kwa Watendaji ambao wanatumia fedha za maji kwenye matumizi mengine na kusababisha adha kwa wananchi wetu, hususan wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba ukiangalia bajeti hii, kwenye Sekta ya Uchukuzi, fedha za ndani zilizotolewa ni sawa na asilimia 30 tu, lakini fedha ya nje hakuna hata kiasi kidogo cha fedha ambacho kimetolewa. Ukiangalia bajeti ya Uwanja wa Ndege wa Kigoma, fedha ya ndani imetengwa Shilingi milioni 400 tu, lakini fedha ya nje imetengwa Shilingi bilioni 10 na *point*. Kwa hiyo, ukiangalia kiuhalisia na kwa mwaka uliopita, fedha ya nje haikutoka hata shilingi kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kama Shilingi milioni 400, itaweza kutengeneza maegesho ya ndege, magari, banda la abiria, mitambo ya kuongozea ndege na ukarabati mwingine kwenye uwanja ule. Kiwango hiki ni kidogo sana.

Kwa mfano, uki-*compare* na uwanja wa Arusha, umetengewa fedha za ndani nyingi sana takribani Shilingi bilioni 10, lakini ukiangalia Arusha na *KIA*, *almost* zipo karibu sana! Kwa nini Serikali inakuwa haina vipaumbele? Kuna watu ambao wanakuwa wanahitaji zaidi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tunagawana *National Cake,* ni lazima tugawane katika hali ya usawa. Kwa hiyo, napenda kabla bajeti hii haijapita, muanze kutufikiria watu ambao tupo mipakani na maeneo yetu yana fursa za kiuchumi kama Serikali itatuwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye kitabu cha Kamati, Sera ya Matumizi; kwakweli eneo hili linashangaza sana. Mapato yetu ya ndani yote yanaingia kwenye matumizi na bado inabakia Shilingi trilioni tatu, inabidi tukope ili matumizi ya kawaida yaweze kwisha. Hapo hatujagusa miradi ya maendeleo! Kwa maana hiyo sasa, tumekuwa na bajeti ya kutumia bila ya kuwa na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linasababishwa na ukubwa wa Serikali. Serikali imekuwa ni kubwa. Kila siku tunasikia Wilaya mpya, Mikoa mipya, wengine ni Wabunge wapo humu ndani, Wakuu wa Wilaya ni hao hao, Wakuu wa Mikoa ni hao hao. Serikali imekuwa ni kubwa sana. *(Makofi)*

Ukarabati wa majengo ya Wakuu wa Mikoa; kwa mfano, mimi naweza nikatoa jengo langu la Mkuu wa Mkoa wangu wa Mkoa wa Kigoma, linahitaji ukarabati wa Shilingi bilioni 1.1. Ukarabati! Kwa mwaka huu wamefanya punguzo kutoka Shilingi bilioni moja mpaka Shilingi

milioni 700, ukarabati wa jengo! Sasa tukisema nchi nzima ikarabatiwe, inakuwaje? Bado Ofisi za Wakuu wa Mikoa hazijakarabatiwa, haujaja nyumba za Ma-*RAS*, Ma-*DAS*, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi. Kwa hiyo, *size* ya Serikali imekuwa ni kubwa sana kiasi kwamba ndiyo maana kila tunachokusanya tunatumia kwa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo yanakuwa bado hayajaafikiwa.

Kwa hiyo, napenda kutoa ushauri kwamba ni lazima Serikali ijitathmini. Kama kweli tunataka kuleta maendeleo katika nchi yetu, ukubwa wa Serikali ni lazima upunguzwe ili tuweze kuwa na unafuu. Kama itawezekana, badala ya kila mtu kuwa na nyumba yake, watu ambao wapo Serikalini mnaweza kuwajengea *flat* kama *apartment,* kama Mawaziri wanavyokaa Kijitonyama kule Dar es Salaam. Wawekeeni *flat*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweza mkawawekea magari machache ambayo asubuhi yatawachukua, yatawapeleka kazini, baadaye yatawarudisha; kuliko kila mtu kuwa na nyumba yake, kila mtu ahitaji Shilingi bilioni moja ya kutengeneza nyumba, kila mtu ahitaji V8 ya Shilingi milioni 500. Kwakweli mzigo ni mkubwa sana! Hii Serikali kama ni sikivu, ni lazima isikilize. Kama imeshindwa, basi Watanzania watupe fursa UKAWA ili angalau haya tunayoyasema tukayatekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kugusia ni deni la Taifa. Deni la Taifa limefikia takriban trilioni 35. Ukiangalia, miradi mingi ambayo imekuwa ikitekelezwa mingine haitekelezeki, mingine inakuwa kama miradi vivuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Serikali ilienda kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *Machinga Complex*, lakini jengo lile mpaka leo hii halijaanza kurudisha deni lile ambalo Serikali ilikopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingo lile limejengwa chini ya kiwango; hakuna lifti, halizalishi, vyumba kama vya panzi, wafanyabiashara wanashindwa kufanya biashara zao! Kwa hiyo sasa, Serikali inakopa na kuwekeza katika miradi ambayo haiwezi kurudisha madeni. Kwa hiyo, kadri siku zinavyozidi kwenda mbele deni la Taifa linazidi kukua na hakuna chochote kinachoweza kufanyika kususan maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gesi; Kambi rasmi ya upinzani Bungeni ilishauri kwamba badala ya Serikali kuendelea kusubiri kujenga miundombinu ya gesi, *process* ambayo inaweza ikachukua miaka mingi, tulishauri kwamba kwa kuwa Watanzania sasa hivi wananunua gesi kwa bei ghali sana ya kutumia majumbani, ni vyema sasa gesi ambayo tunaivuna nchini kwetu ingeweza kuchakatwa, ikapakiwa kwenye mitungi na kuwapelekea Watanzania watumie ili nishati ya kuni ambayo inaathiri miti yetu iweze kuendelea kuwa salama. Hii ilikuwa ni mpango mzuri ambao Kambi tulishauri badala ya kusubiri kutandaza mabomba nchi nzima jambo ambalo litagharamu fedha nyingi na kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni mfano wa nchi ya Ukraine. Ukraine ipo karibu na Urusi. Urusi inachimba gesi nyingi sana. Takriban asilimia 80 ya nchi za Ulaya, gesi yake inayotumia inatoka nchini Urusi, lakini mabomba yake yote yametandazwa kupitia nchi ya Ukraine. Sasa mgogoro uliosababisha Urusi na Ukraine, ni baada ya watu wa Ukraine kuwa wanachimba yale mabomba na wanajionganishia ile gesi kiholela.

Kwa hiyo, sasa kwa nchi yetu, kama hili zoezi litaendelea, liendelee lakini lazima tuangalie hizo *pre-caution* kwamba kuna uwezekano mkubwa baadhi ya watu wakaja kuhujumu baadaye hiyo miundombinu. Ndiyo maana Kambi Rasmi na Upinzani ilipendekeza

kwamba kuna haja sasa ya kuanza kupakia gesi yetu kwenye mitungi ili Watanzania waanze kutumia wakati tukisubiri huo mtandao wa mabomba uweze kuenea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti. Suala lingine ambalo napenda kuchangia kuhusu wafanyabiashara, uchumi wa Mkoa wa Kigoma umekuwa ukiathirika sana na vita ya Burundi na Congo. Pia hata safari za meli ambapo zamani tulikuwa tunapata safari nne kwa mwezi, sasa hivi zimepungua sana. Vile vile kuna uvamizi katika Ziwa Tanganyika na majangili katika mipaka yetu, lakini kodi ambazo Kigoma wanalipa, hususan pale Kigoma Mjini, zimekuwa juu sana. Faini za ucheleweshaji wa kodi zilikuwa Sh. 10,000/= lakini sasa imefika mpaka Sh. 100,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tungependa kabla hujamaliza muda wako, kipindi kilichobakia, uweze kutuma timu ikaangalie malalamiko ya wafanyabiashara wa Kigoma Mjini, wamekuwa wanalalamika muda mrefu bila msaada. Ni vyema sasa uchukue fursa hii kwenda kuwasaidia watu hawa na kuwasikiliza hasa ni kwanini kodi ya Kigoma ukilinganisha na Mikoa mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma tumekuwa tunapata shida sana kwenye ujenzi. Nyumba moja ya Kigoma ni sawasawa na nyumba mbili za Dar es Salaam. Mfuko mmoja wa *cement* tunanunua takribani Sh. 25,000/=. Kwa hiyo, kuwatoza wafanyabiashara hawa kodi kubwa kwakweli inakuwa ni mzigo mkubwa tena sana na wananchi wetu wamekuwa wakiathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nigusie viwanja vya mipira. Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza kwamba viwanja vya mpira viweze kurudishwa Serikalini, vitoke mikononi mwa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu viwanja vingi ukiviangalia hadhi yake ni dhaifulhali. Chama cha Mapinduzi walihodhi hivi viwanja lakini wameshindwa kuvihudimia. Tumekuwa tukishauri hapa kwamba Sekta ya Michezo ni lazima iwe ni sekta ambayo itarudishwa kwenye mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani Mashirika ya Umma yalikuwa yanafanya vizuri. Tulikuwa tuna timu za mipira; *CDA*, Tumbaku, Morogoro, Reli, Mtibwa, Kagera Sugar, Chumvi Uvinza; watu wote hawa kwa sababu walikuwa chini ya Mashirika ya Umma waliweza kufanya vizuri kwa sababu tu, Mashirika haya yana fedha kuweza kuendesha mpira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mkoa wa Kigoma ulikuwa unatoa wachezaji wengi sana na Mkoa ulikuwa unapata sifa na nchi kwa ujumla, lakini mpaka leo hii hatuna hata timu ya kucheza ligi kuu.

Kwa hiyo, tungependa Serikali kama tunavyoshauri, kwakuwa mmeshindwa kukusanya fedha sehemu nyingine, basi leteni nguvu katika Sekta ya Michezo ili wananchi wetu waweze kufanya vizuri. Naamini kama tutawekeza vizuri kwenye michezo, Taifa litapata fedha na hii bajeti ambayo imekuwa inasuasua itakaa vizuri kama tutawekeza katika Sekta ya Mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala la *Vocational Skills*. Tanzania tumekuwa tukijikita sana katika kuwekeza kwenye elimu ya juu, lakini tukiangalia kazi ambazo ni *white collar jobs* zinazotokana na elimu ni kazi ambazo zimekuwa kwa kiasi kikubwa kwanza ajira ni chache na wanafunzi ni wengi. Lakini kama tutawapa hawa watu *Vocational Skills*, wawe na ujuzi, watasaidia sana nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii vijana wana *degree* mbili, tatu, nne mpaka tano, lakini hata mtu kuchimba mfereji wa majitaka kutoka chooni kwenda uwani hawezi; kutundika tungi ya taa juu, hawezi! Kila kitu hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kukupa ushuhuda. Kuna mtu mmoja alikuwa anajaribu kutengeneza miundombinu ya majitaka kwenda baharini; walikuja watu na *degree* zao, ni ma-*engineer* walishindwa. Aliletwa Babu wa zamani aliyesoma zamani Darasa la Saba, alifanya ile kazi kwa muda wa siku moja tu. Tukajiuliza, kwa nini huyu mtu wa zamani ambaye hana elimu, ameweza kutengeneza mfumo mzuri na *slope* ikapatikana? Lakini walikuja ma-*engineer* na wasomi kutoka Chuo Kikuu, lile zoezi liliwashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inaonesha kwamba Vocational Skills ni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijasitisha shughuli za Bunge, naomba nitambue wageni waliopo hapa Bungeni ambao walikosa nafasi asubuhi. Ni Wanachuo 15 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na wanafunzi 60 ambao ni Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Naomba hao niliowataja wasimame! Karibuni sana.

Sasa kama tulivyotengua kanuni zetu juzi, kufuatana na Mfungo Mtukufu wa Ramadhani, kikao chetu kitaendelea saa 10.00 alasiri na kitahairishwa saa 12.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha, naomba niwataje watakaochangia jioni. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Kheri Ameir; wa pili Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Josephine Gezabuke, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Anastazia Wambura. Naomba hao wawahi kuja. Sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Josephine Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Nundu na Mheshimiwa Anastazia Wambura ajiandae. Mheshimiwa Josephine!

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba radhi, sauti yangu leo siyo nzuri, itabidi mnivumilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kunijalia afya na kuweza kunipa kibali kuweza kuzungumza jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kupongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya, Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanasemwa maneno mengi kuhusu Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Naomba nichukue nafasi hii kuendelea kuishukuru Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo imekuwa ikiendelea kuifanya kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Tanzania na hususan katika Mkoa wetu wa Kigoma. Naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuja na wazo la kuongeza tozo ya mafuta. Tozo hii ikiongezeka kupitia kwenye mafuta na pesa ile ikakusanywa vizuri ikapelekwa kwenye *REA* itaweza kutusaidia sana wananchi wa Tanzania, lakini itaweza kuwasaidia wananchi wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana tumekuwa tukilalamika nchi kuwa gizani, nchi kutokuwa na umeme, lakini kupitia chanzo hicho ambacho Serikali wameweka, naamini kabisa pesa hiyo ikikusanywa na ikapelekwa *REA,* Vijiji vingi vitafikiwa na wananchi wengi wataweza kupata umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatofautiana na watu wanaokataa chanzo hiki cha fedha kupitia mafuta kisikusanywe. Ni lazima tuwe na utaratibu sasa, sisi Watanzania wenyewe kuzoea kujifunga mkanda kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema hivyo? Zamani walipokuwepo wa-*missionary* walikuwa wakitujengea shule, wakajenga Hospitali, wakajenga Makanisa, lakini walipoondoka kazi ya ujenzi wa Makanisa, ujenzi wa nyumba za Waganga katika Hospitali, zile zilizokuwa zikiendeshwa na wa-*missionary* sasa yamekuwa zimekuwa zikifanywa na waumini wa maeneo yale na wanaenda vizuri. Ukienda vijijini wamejenga Makanisa makubwa, wamejenga shule na nyumba za Wachungaji, waumini wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata huku Serikalini naomba wananchi nao wazoee kufanya kazi wao wenyewe, kwa sababu hawa jamaa walikuwa wanatupa masharti kila wakati, wanatupangia ni jinsi gani watuchangie pesa. Wakati mwingine wanaahidi kutoa hela, halafu haziji kwa wakati, zinachelewa, matokeo yake baadhi ya miradi kule vijijini kwenye Halmashauri inakwama.

Sasa tukiamua wenyewe kuanza kujifunga mkanda, ninaamini wananchi tutaweza kupitia Serikali yetu. Isipokuwa zile pesa zitakapokusanywa ziende zikafanye kazi iliyokusudiwa. Naamini tutaweza na wananchi wakielimishwa wakahamasishwa, wataweza wao wenyewe kuchangia maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizo zikienda *REA*, Vijiji vikapata umeme, viwanda vidogo vitaanzishwa, Saluni ndogo ndogo zitakuwepo, vijana watajiajiri kupitia Saluni za kike na kiume, laini mashine za kusaga na kukoboa katika vijiji vyetu zitakuwepo. Mashine za kusindika mazao mbalimbali zitakuwepo na mashine za kuweza kukamua mafuta kwa mfano mawese na mafuta mengine haya ambayo tunayaona hata tukiwa tunapita njia ya Singida wataweza kupata viwanda vidogo vidogo kupitia umeme huo na wataweza kuzalisha wenyewe, matokeo yake wananchi wataweza kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wa *TRA*, Kamishna Mkuu, kaka yangu Ndugu Bade na Watendaji wengine wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wanafanyakazi kubwa na nzuri!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa *TRA* wapo wachache kabisa, hawatoshi. Kwa sababu gani nasema hivyo? Kama wangekuwa wanatosha, wangeshuka maeneo mbalimbali wakaenda kukusanya kodi sehemu mbalimbali na kupitia kodi ya hawa watu ambao ni wajasiriamali wadogo wadogo tungeweza kukusanya kodi ya kutosha na kodi hiyo ingeweza kuja kusaidia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile pesa ile ambayo imekusanywa na *TRA* ikishakusanywa, Serikali waipangie shughuli zile ambazo zimepangwa kuliko kubadili tena matumizi. Pesa zinapatikana halafu matumizi ya zile pesa yanabadilishwa yanapelekwa kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pesa zile zikipatikana zigawanywe sawasawa, zipelekwe kufanya kazi zile ambazo zimelengwa kuliko kuzitoa pesa hizi tena na kuzipeleka sehemu nyingine ambako hazikuwa zimekusudiwa. Tukifanya hivyo, tutaweza kuinua uchumi wa nchi yetu na tutaweza kupiga hatua na wananchi wetu wataweza kunufaika kupitia pesa zinazokusanywa kupitia *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuja na vipaumbele vya maji, umeme, na kadhalika na kutokuongeza vipaumbele vingine. Naona hiki ni kitu kizuri. Vipaumbele hivi ambavyo tumejipangia sasa ni wakati muafaka kuweza kuhakikisha maji yanapatikana, umeme unapatikana, lakini afya nayo kwa wananchi wetu inaimarika. Tukifanya hivyo, naamini kabisa kwa sababu hakuna vipaumbele vingine ambavyo vitakuwa vimeongezwa, itakuwa ni kukamilisha vile ambavyo tumejipangia, tutaweza kumaliza tatizo, japokuwa hatutamaliza kabisa, lakini tutawapunguzia makali wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kilio kikubwa cha madeni. Watu wanaidai Serikali; Wakandarasi, Wazabuni na wazee waliostaafu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, wajipange sasa kuhakikisha wanalipa madeni ili kuwaondolea matatizo wananchi hawa ambao wamejitolea kwa kufanya kazi bila kulipwa pesa. Sasa muda wa kulipwa pesa unapofika, basi wapewe stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo Vyuo vingi ambavyo vimekuwa vikipelekewa vyakula na Wazabuni na hawa Wazabuni wamekopa pesa kwenye mabenki; wanauziwa nyumba zao, wanafilisiwa kwa sababu wamekopa na hawajaweza kurejesha pesa. Sasa naiomba Serikali ilipe madeni kwa Wakandarasi, Wazabuni, Wafanyakazi wakiwemo na Walimu na watu wote wale wanaoidai Serikali ili kuweza kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu mapato ya Serikali kuhusu miundombinu ile ambayo haijaweza kukamilika. Naomba pesa zinapopatikana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Saada upeleke pesa kwenda kukamilisha miradi ile ya barabara ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimerudi leo kutoka Kigoma. Kuna barabara ile ya Kigoma - Nyakanazi, tunaomba pesa zile ambazo Waziri wa Ujenzi ameahidi, zipelekwe ili kuweza kukamilisha barabara ile ya Kigoma - Nyakanazi. Kwa sasa hivi barabara ile haipitiki kabisa, kabisa! *TANROAD* Mkoa hawaishughulikii kwa sababu tayari ilishawekwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Wananchi wa Kigoma wanaipenda CCM, wanaomba mwatengenezee barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipande cha Uvinza - Malagarasi, nacho kinahitaji pesa kusudi kuweza kukamilisha ujenzi ule wa barabara ya pale kwenye daraja la Mto Malagarasi maarufu kama Daraja la Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikia watu wanasema wanaiondoa Serikali ya CCM madaraki, haitoki! Huu ni wasiwasi wao kwa sababu wanaamini tumejipanga vizuri. Niwaase tu wana-CCM wenzangu, tutoke ndani tukiwa wamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa jamaa wanatutegeshea waone tunavuruganaje, lakini tukitoka tukiwa ni wamoja, hawakatishi! Wanatutegeshea tu waone tunafanyaje mambo yetu! Hivyo, tukitoka wamoja, wao wenyewe wanajua ngoma mdundo, ndiyo maana wengine wameshaanza kuhama Vyama mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wameshaanza kuhama Vyama mapema; huko wao wenyewe hawaelewani; hiki hakiendi huku! Kuna Vyama vingine vidogo tu, walishaanza kugombana. Hii ni dalili ya kwamba sasa tayari CCM mwendo mdundo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Kigoma. Wananchi wa Kigoma kilio chao ni reli. Naomba pesa zipelekwe kwenda kujenga Reli ya Kati. Reli ni kichocheo kikubwa cha uchumi. Reli ile ikikamilika, mizigo itaweza kusafirishwa kiurahisi, barabara zetu hazitaharibika na wananchi watanufaika kusafirisha mizigo yao kupitia reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi walihamasishwa kuanzisha vikundi vya ujasiriamali vikiwemo *VICOBA,* lakini wananchi hao bado hawajapata elimu ya kutosha, hawana Walimu! Wameanzisha vikundi lakini hawana Walimu, wanashindwa kukopesheka kwa sababu hawajapata elimu ya kutosha wakajifunza, wakaelewa, wakajua ni jinsi gani sasa wanatakiwa waende kukopeshwa na mabenki. Kwa hiyo, naomba kabisa elimu ipelekwe kwa wananchi ili waweze kujua ni jinsi gani wanaweza kukopa kupitia vikundi vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini hatutungi sheria inayosimamia uendeshaji wa *VICOBA*? Naomba sasa kupitia Bunge lako, tutunge sheria ambayo itasimamia uendeshaji wa *VICOBA,* hatimaye wananchi waweze kujua wanakopeshwa vipi kwa sababu tayari kutakuwa na sheria inayowalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Benki ya Posta pamoja na Twiga. Benki hizi zimekuwa mkombozi kwa Wajasiriamali wadogo wadogo. Naomba Benki nyingine zijifunze kupitia Benki hizo ili ziweze kuwasaidia wananchi wale wajasiriamali, wenye *VICOBA* na watu wengine wengi waliounda *VICOBA* hasa wanawake na vijana ambao ndiyo wanaohitaji kukopa kupitia Benki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba niseme naunga mkono bajeti hii ipite ili vipaumbele vyote vilivyowekwa viweze kukamilika. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephine. Sasa namwita Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Anastazia na Mheshimiwa Kheri Wajiandae.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kunipatia nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya bajeti ya Serikali. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema zake zote ambazo anatupatia sisi binadamu, hususan kwa kuniwezesha mimi kuwepo Bungeni hapa nikiwa na afya nzuri, nikiwa na furaha, nikiwa niko katika hali nzuri ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwezi wa Ramadhani na leo ni Ramadhani Mosi. Niseme kwa Waislamu wote na binadamu wote wanaomwamini Mwenyezi Mungu, Ramadhani Karim! Ni mwezi wa kuomba, tuna mambo mengi sana ya kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Waislamu, Mufti ametangulia mbele ya haki, tunasema *Innalilah Wa-Inna Ilayhi Rajiun,* lakini pia wajitayarishe kuweza kupata Mufti mwingine ambaye ana sifa kama siyo zaidi lakini kama za Mufti ambaye ameondoka.

Hali kadhalika mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi ndiyo maana tunaona Bungeni hapa saa nyingine badala ya kuchangia bajeti, watu wanaingia kwenye kampeni. Tuzidi kumwomba Mwenyezi Mungu atupatie Viongozi imara, viongozi wenye maadili, viongozi ambao wana uchungu na nchi yao na wananchi wenzao, waweze kutupeleka mbele kwenye nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru sana ndugu zangu wa Tanga kwa kunipa Ubunge wao niufanyie kazi; na ninaamini kabisa nimeufanyia kazi vizuri, matokeo yameonekana; na vile wanavyoniambia wanapenda niendelee, nawaambia nitaendelea. Ripoti wanazonipa za mtu anayepita na kusema uwongo na vile ambavyo wanamweka kando huko, hana lolote jipya, waendelee kufanya hivyo. Tumesema Tanga siyo mgumba na wana Tanga siyo wakiwa na watu wa magauni wameliona hilo baada ya kupata mafuriko juzi tu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuwa anamaliza muda wake na kwa nafasi ambayo alinipatia nikawa Waziri wa Uchukuzi kwa takribani mwaka mmoja na nusu. Ni mwaka ambao ulikuwa ni muhimu sana kwangu. Nilijifunza mengi, nimejua watu wengi, imenitayarisha katika hali ya kujua nitaiendeleza vipi na kuitumikia nchi yangu. Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Saada, pongezi sana ndugu yangu! Umekuja na bajeti hii ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Kuna ambao hawaoni yanayotokea na hawawezi kuangalia takwimu zinaonesha nini. Nikiangalia kwa kipindi cha miaka saba katika kitabu chako hiki, umeonesha wazi kabisa kuwa mapato yote yamekuwa yanakua. Ukichukulia tu mwaka 2008/2009 mapato yetu yalikuwa Shilingi trilioni 6.84, lakini baada ya miaka saba, kwa mwaka 2014/2015 yaliongezeka mpaka Shilingi trilioni 18.145. Hili ni ongezeko kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapoongezeka kila mwaka, inaonesha dhahiri, ongezeko la mwaka mmoja kwenda mwingine ukifananisha na mwaka wa nyuma, hili la mwaka huu wa mbele ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, hii ni kasi ambayo tayari imeshika mwendo na ni kasi ambayo ikiendelezwa hivyo, tutazidi kupata mapato ya kutosha, kuja kutatua matatizo ambayo sasa hivi kidogo yanasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwelekeo huu, nilitegemea bajeti ya mwaka 2015/2016 isiwe Shilingi trilioni 22.5. Nikiangalia mwelekeo ule ukiweka kimahesabu, nadhani tumekuwa tunaongelea Shilingi trilioni 24. Sijui kwa nini mmeogopa kwenda huko! Labda mna sababu, lakini mimi ningefarijika zaidi kuona kweli *trend* tungeiendeleza tukienda kwenye Shilingi trilioni 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, papo hapo mapato ya ndani katika hizo Shilingi trilioni 22.5 ni Shilingi trilioni 13.5, wakati matumizi ya kawaida ni Shilingi trilioni 16.6. Sasa hapa kuna mambo mawili ambayo yako wazi; aidha, matumizi yetu ya kawaida ni makubwa, inabidi tuyapunguze.

Waingereza wanasema kwa tafsiri, "ushone koti lako kufuatana na ukubwa wa kitambaa ulichonacho."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama makusanyo yetu ni Shilingi trilioni 13.5 lakini matumizi ni trilioni 16.6 kama ilivyooneshwa, nadhani kwa hiyo hoja niliyoitoa kwanza, tungejaribu tuone tunapunguzaje matumizi ili ifikie hiyo Shilingi trilioni 13.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kule kutokukusanya mapato inavyotakiwa. Jitihada mmezionesha, lakini nadhani jitihada hizi itabidi tuziboreshe, kwa sababu kwanza lazima wananchi wote tuelewe kuwa sote tunatakiwa tulipe kodi. Ndiyo maana zile mashine za *EFD* itabidi mwaelimishe wananchi na wafanyabiashara ziwe zinatumika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mashine kama zile, kwa wenzetu kwingine, labda nitoe mfano wa Canada; Canada ukienda ukanywa kikombe cha chai, labda uko Montreal unalipia kodi ya Quebec, unalipia na kodi ya Canada, unalipa *7.5* na *7.0;* unalipa *14.5* kwa kikombe cha chai unachokinywa. Watanzania lazima twende huko, kwa kila tunachokifanya tujue tunatakiwa tulipe kodi. Hiyo ni ya kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi hizi za nyenzo za uzalishaji ambazo hapa tumekuwa tunaendelea na mmeweka tena na mikakati ya kupata watu kuja kuwekeza. Tupate faida za kuwekeza, achia mbali ile faida ya kukusanya mapato. Tunaruhusu kuwa tunawapa fursa ya kuwasamehe kodi kwa kipindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili naomba tuliangalie tena. Katika kuangalia mikakati isiwe ni kwa kila kitu. Ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola alisema juzi pale, mpaka *toothpicks* tunatengeneza China tunaletewa hapa. Hawa ambao wanataka kuja kuwekeza; na tusiangalie pesa tu, tuangalie wanakuja kuwekeza kwenye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania vibajaji vimeenea chungu nzima na *demand* ya vibajaji na bodaboda (pikipiki) ni kubwa, lakini bado hivi vitu havitengenezwi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea kuwapa fursa hii watu wanaokuja kuanzisha viwanda ambavyo vitakuwa vinajenga vitu vikubwa na ardhi tunayo, wakija Tanga kule *fertilizer* kuna ekari 165, wanaweza kuja kuweka kiwanda cha kutengeneza *television* pale; wakaweka kiwanda cha kutengeneza simu, wakaweka kiwanda cha kutengeneza *computer;* vikawa vinatengenezwa hapa tunauza nje. Bahati nzuri kuna mwekezaji pale ameshaanza kutengeneza *voucher* hizi za simu, badala ya kuwa zinatoka nje. Kwa hiyo, vitu kama hivyo tungepata wawekezaji ambao watakuja kujikita kwenye viwanda vikubwa kama hivyo ingetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawa wa ndani wawezeshwe, nimesema mara nyingi sana mtu asianzishe leo biashara yake ya kufanya, halafu moja kwa moja anaanza kulipa kodi, hapana! Lazima ile *tax holiday* ya miaka mitano wapewe hawa katika kujenga uwezo wa kesho na keshokutwa kupata watu ambao watakuja kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ukimfanya alipe kodi akafa kampuni yake ile, haisaidii kitu kwa sababu haikuwepo. Sasa ipo, usione kile ndiyo chanzo cha kupatia pesa, kione ni chanzo cha kuendeleza uwekezaji wa kuwafanya watu waweze kuchangia kodi huko mbele. Kwa hiyo, wapewe *tax holiday.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongelea ndugu yangu aliyemaliza kuhusu Benki ya Posta, namshukuru sana Ndugu yangu Sabasaba, Mkurugenzi kule. Amekuja Tanga pale, sasa hivi tunapeleka vikundi chungu nzima kukopa kwenye Benki ya Posta na riba yao ni ndogo tu. Kwa hiyo, wananchi wenyewe wawezeshwe kufanya hivyo, waweze kujijenga kiutendaji. Ukifanya hivyo, wengi hizi *handkerchiefs*, *colgate*, *toothpicks* zitatengenezwa na wao hapa. Lakini kama anataka kutengeneza *toothpick* halafu anachajiwa kodi siku ya kwanza kabla hajauza chochote, umeshammaliza huyo, hawezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongelea wawekezaji kutoka nje na nimesema wao wapate msamaha kwa yale mambo makubwa, waje wajenge magari hapa, lakini kwa vitu kama mahoteli na masuala ya utalii, mimi sioni sababu kabisa kwa sababu, ukienda kwenye hoteli na utalii, ukimaliza hoteli tu unaanza kupata faida na huu ni ukweli. Mambo ya utalii wanapata faida toka siku ya kwanza. Sasa wanaposamehewa kodi ya magari yanayoingia hapo, inakuwa siyo sawasawa. Kwa hiyo, mnapoangalia nani wa kumsamehe na nani wa kumwambia kuwa aanze kulipa tangu mwanzo, naomba mwangalie kwenye mantiki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapa pongezi pia Wizara kwa kuliingiza lile la maji na umeme. Nilisema hapa wakati nachangia Wizara ya Maji na nilikuwa wazi kabisa na mpaka nikataja *figure* kwa *calculations* nilizokuwa nimezifanya, lakini nitaweza kufanya zaidi. Kwa hiyo, kitengwe kima cha kutosha kumaliza tatizo la maji, siyo kupunguza. Kama bajeti ya Shilingi trilioni 22, ikibidi tutenge Shilingi trilioni moja na nusu ishughulikie maji, iwe *ring fenced* kwa ajili ya maji, tulimalize tatizo la maji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kwenye umeme, pamoja na tozo tunazotoa, lakini tuazimie kabisa kuwa safari hii tatizo la umeme linamalizika. Vitu viwili hivyo viwe vimekwisha. Sasa haya mambo mengine ambayo tunayafanya, tuwaachie watu wengine wafanye. Tuwaachie watu wengine wajenge bandari, wajenge reli, lakini mikataba iwe inayoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo tunaongelea Bandari ya Mwambani, Bandari ya Mwambani, mara tunaambiwa kuna Mwapoc, mara Bandari ya Tanga palepale, hakuna kinachofanyika na uchumi unaduwaa, siyo wa Tanga tu, lakini wa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mewenyekiti, tunaongelea reli, tumekwenda mpaka tukasaini mikataba na Waganda na Wachina, hakuna kinachoendelea! Tutafute watu waje wajenge hivyo vitu. Tumeweka hapa Sheria ya *PPP* ilikuwa na matatizo yake na mlolongo mrefu, lakini nadhani ndiyo Mheshimjwa Mary Nagu alilitatua hilo kuweza kuharakisha kuwa watu wakija tuone wanawezeshwa vipi upesi upesi kuweza kuingia na kuendeleza vitu ambavyo tunataka tuvifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vimekufa. Viwanda inabidi vifufuliwe na inabidi watu wavutiwe kuja kuanzisha viwanda. Hatuwezi kwenda popote bila ya viwanda. Lakini viwanda vilivyokufa mpaka leo kwa nini watu wameachiwa wamevishika tu! *Steel Rolling Mill* pale Tanga, *Sikh Sawmills* pale Tanga, imekaa tu kila siku tunaambiwa anatafuta hati. Hati ya kufanyia nini? Mtu ana kila kitu na ana nyenzo ya kufanyia kazi, hataki kufanya kazi, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakisuasua hivyo, naomba kabisa mlichukue *seriously* kuwa hawa watu ambao wamechukua viwanda hawaviendelezi, basi viwanda hivyo vichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu nilitegemea ziende sehemu ambazo zinajitegemea kifedha, hazifanyi hivyo. Mwangalie mtaziwezeshaje Halmashauri hizi. Mmefanya

jambo jema Wizara ya Vijana, Wizara ya akina mama wanatenga pesa za kuanzishia *SACCOS,* pesa hizo sijaona *SACCOS* hata moja imeanzoshwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepigana pia hapa 5% za vijana ambazo miaka yote hazitolewi, sasa zinatolewa. Mliangalie! Kuna wajanja kule wanaanzisha *SACCOS* kwa asilimia hizi tano za vijana. Serikali lazima mwaambie wazi 5% zinazotokana na mapato ya Halmashauri siyo za kuanzishia *SACCOS!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema *SACCOS* ni za ujanja ujanja tu, kwa sababu Tanga pale *SACCOS* iliyoanzishwa vijana wakatozwa Sh. 1,980,000/= kama mchango wao na Halmashauri ikatoa Sh. 20,000,000/= majuzi hapa pesa zote hizo zimeliwa na Viongozi waliowekwa wa *SACCOS,* imebaki Sh. 186,000/= tu. Sasa kwa nini waanzishe *SACCOS* kwa kitu ambacho hakihitaji kuanzisha *SACCOS?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko katika Kamati ya *LAAC,* kote tunakotembea huko hakuna kitu kama hicho. Kwa hiyo, kule ambapo wajanja wajanja bado wanafikiria watafanya watafanya matatizo hayo, naomba Serikali iwe kidedea kueleza wazi kuwa 5% ya akinamama na 5% ya vijana siyo ya kuanzishia *SACCOS. SACCOS* inaanzishwa na pesa zinazotoka kwenye Wizara hizo mbili zinazohusuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pale na wakishakula hela hizo, huwezi kwenda Halmashauri kuingilia kwa sababu *SACCOS* ina mipango yake. Kwa hiyo, hayo mambo yashughulikiwe. Unaposhughulikia, wanadanganya vijana huko kuwaambia fulani kazuia hela zenu, kitu ambacho sicho kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *EPZA* na *EPZ* baadhi wamelipwa baadhi hawajalipwa. Wanalalamika, wameingia umaskini. Hizi pesa zipatikane, walipwe. Hizo sehemu kama bado tuna nia ya kuzifanyia kazi kuendeleza viwanda zifanyiwe. Halmashauri zinapoanzisha viwanda zifaidike na viwanda hivi. Kila kitu kama tunakitia kwenye *EPZ,* Halmashauri ndiyo hapo zinakuwa hazina pesa za kufanyia kazi. Tanga Hospitali ya Wilaya naomba muipatie pesa imalizike kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kheri atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Kafulila ajiandae.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namshukuru Mwenyezi Mungu *Sub-hanah-wataallah* kwa kutufikisha hapa, lakini vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuletea Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Tumo katika wakati ambao kwa Waislamu ni mwezi Mtukufu, ni mwezi mkubwa na *inshallah* atusaidie kwa baraka zake na baraka za Ramadhani Watanzania wote tutoke hapa tulipokuwa tumekwama. Tunamwombea vilevile Marehemu Mufti wa Tanzania Mungu amlaze mahali pema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wapigakura wangu wa Jimbo la Matemwe Zanzibar; na kwa kiasi tumeshirikiana, nimewatumikia kiasi cha kuwatumikia na Mwenyezi Mungu akipenda nadhani safari hii nawaaga. Nawaaga wao na nawaaga vilevile wenzangu katika Bunge la Tanzania. *Inshallah* tumeshirikiana, tumejuana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru CCM kwamba imenifunua na kunipa upeo mpana licha ya upeo wa kujua mambo, lakini vilevile kujuana na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo, nakuja hapa na kilichokuwa kimetukusanya na kuchangia. Kwanza nasema naunga mkono bajeti ya Serikali na namwambia Mheshimiwa Mama Saada kaza kamba, nawaambia CCM kaza kamba, nawaambia Watanzania tufunge mkanda, hatuna Wajomba sisi. Kama tutaendelea kuogopa au kutokujaribu, basi hiyo miaka tunaambiwa 50 tuliyokuwa hatujafanya jambo, tutarudi nyuma ya hapo zaidi. Mheshimiwa Mama Saada uko katika *right path* au *right track,* twende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonipa wasiwasi, sijui kama kweli sote hasa katika upande wa Kambi ya pili ya Upinzani, hivi katika muda wote tuliokaa hakuna jema lililofanywa hata moja? Wako wale wanaosema kwamba Tanzania hii hakuna kilichofanywa miaka 50 iliyopita, lakini kati yao miaka 50 iliyopita hawakuwepo, wamesomeshwa, wamekuzwa, wamelelewa mpaka wamefika hapa walipokuwa wamefika. Nafasi walizonazo, kuna wengine hawana kabisa, lakini ndiyo safari, tumshukuru Mwenyezi Mungu. Nawatanabahisha na wao kwamba hii kazi siyo ndogo, ni kubwa na hatutawapa CCM hata siku moja, hatujaribu kuwapa, ikiwa bado mawazo yao ni mawazo ya kuvutana na kusukumana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa niko mahali fulani; mimi sio mtu wa maneno, wala sio mtu wa mivutano. Lakini nilikwenda Hospitali ya *Private* nikakuta watu wanazozana, wanavutana, wanasema aah, hivi Bunge vijana wanabishana kama vile! Wanabishana kama wako sokoni! Wanasema, (mtanisamehe) wakafika mahali wakasema hivi kweli CHADEMA kama tutafika mahali pa kuwapa nchi, tutakwenda wapi? Kuna mmoja akasema katika wale kuna Waziri gani hasa aliyekuwemo? Mimi nawaona kama watoto wanacheza tu! Mtanisamehe! Nadhani mtanilinda, lakini hilo nililisikia!

Baada ya kusema hayo, sasa nijielekeze katika mada iliyopo mbele yetu. Nimemsifu sana Mheshimiwa Mama Saada na *Institute* ya Wizara ya Elimu, lakini pana jambo muhimu sana tunapaswa tulizingatie na tuweze kuliona.

Kama hatukutoka hapa anapotuelekeza Mheshimiwa Saada au Mheshimiwa Waziri na timu yake, basi hatutatoka tena. Kwa sababu, tatizo la Tanzania siyo watu, tatizo la Tanzania siyo mali tuliyonayo, tatizo la Tanzania kubwa linalotusonga ni ajira. Ajira ambayo inadai ina watu wengi, nadhani ni kilimo. Vijana wanaoranda na maduka migongoni, hawatatufikisha mahali. Ajira zile wanazofanya tunawafanyia watu waliokuwa na viwanda vilivyoko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwamba ajira isiwe biashara, ajira iwe ni kilimo. Tukifika mahali tukaweza kujielekeza kwenye kilimo na tukalima, hapo tutakuwa tuna nguvu ya kuweka viwanda vidogo vidogo. Tukitegemea misaada, tukitegemea ajira za mifukoni hizi, tukitegemea ajira kwamba kila mmoja aajiriwe Serikalini au kwenye viwanda ambavyo hatunavyo, basi hatutafika mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natoa wazo kwamba tujielekeze zaidi katika kilimo na tujielekeze zaidi katika uvuvi kwa sababu, ni sehemu ambazo ndizo zilizokuwa zimetuzunguka. Tuna bahari ambayo haina mwisho, tuna ardhi ambayo haina mwisho, tuna maziwa makubwa ambayo sisi tukijielekeza vizuri tutakuwa hatuna matatizo ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa *Sychelles. Sychelles* wana watu kama 80,000 wakazi wa pale; 120,000 ni wageni wamehamia pale. Watu wote walioko pale ni karibu 200,000

lakini walivyojielekeza katika bahari, wale jamaa wanasafirisha kontena 350 kwa siku, *20 feet container!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia wa Sychelles walivyo, angalia Watanzania tulivyo, angalia ardhi tuliyonayo Watanzania, angalia bahari tuliyonayo, angalia mito tuliyokuwa nayo, hatuna sababu kama tunajipanga vizuri na kama tuna *determine* kweli kweli basi tutatoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda uliobaki tunaomba Serikali kwamba ijizatiti kuona tunayatekeleza haya. Lawama zisizokwisha, kila siku lawama zipo, lakini hivyo kweli Vyama vya Upinzani kila jambo linalofanywa hakuna jema hata moja? Hebu na ninyi kaeni tuchangieni badala ya kuvutana. Wewe ukifanya jema lolote lile watakwambia kwamba hilo siyo, basi hata hili suala la kuondosha vibatari Tanzania nalo siyo vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao ndiyo wanakuja, wanasema kwamba hatuendelei, vibatari vimejaa mitaani, sasa njooni basi tuendeleze nchi yetu tuweze kuchangia kwa maana moja ama nyingine kuliondosha suala hili, hata hili nalo wanalipinga, lakini wao wakija huku wanalaumu kwamba hakuna umeme, hakuna maji. Sasa hizi nchi tunazozitegemea wameshachoka, wao wanachokifanya sasa hivi wanasema kwamba, sisi tupo na tujitegemee wenyewe, wamechoka kutubeba, sisi bado tunajing'ang'aniza tunasema kwamba aah! Tusaidieni, sasa hawatoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya safari hii kama tulivyokuwa tumeelezwa wamekataa kutoa misaada ya maendeleo, matokeo yake sisi tunazozana. Sasa jamani hebu tukae kama Watanzania, tuwe kitu kimoja, tusahau mvutano uliokuwepo baina yetu wa kivyama, tukaeni kama Watanzania, tukae kama watu wazima, tuseme tunataka nini na tunaelekea wapi. Kama tutaendelea kuvutana hivi hivi, hatuna tutakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naunga tena mkono hoja na nawaambia Serikali tuko katika *right track,* tuendeleeni, haya mavuvuzela tuachane nayo, yatakwisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kheri.

Kabla hatujaendelea, naomba nitambue wageni walioko Bungeni jioni hii ambao ni wageni kutoka *(EANNASO - Eastern Africa National Networks of AIDS Service Organizations)* yenye Makao Makuu yake Jijini Arusha. Yupo ndugu Olive Mumba, ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, naomba asimame. Karibu sana na tunatambua kazi kubwa inayofanywa na taasisi hizi mtandao wa Mashirika ya Kitaifa yanayopamba na UKIMWI Afrika ya Mashariki.

Yupo ndugu Amani Galugwa ni *Finance and Administrative Manager,* asimame. Karibu sana. Pia yupo ndugu Junior William ambaye ni *Team Leader Advocacy and Policy* asimame, yuko ndugu Esther Mzaba ambaye ni *Program Officer.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja mchangiaji atakayefuata, kwa bahati mbaya nilimruka Mheshimiwa Anastazia Wambura, naomba sasa nimwite achangie, halafu afuatie Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na Mheshimiwa Kafulila atafuatia. Mheshimiwa Anastazia Wambura!

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii jioni hii. Nianze kwa kuunga mkono bajeti ya hii ya Serikali kwa

asilimia mia moja. Kabla sijaendelea niseme tu kidogo kuhusu wanafalsafa wanavyotuambia, naomba ninukuu kwamba: "*It doesn't matter if the glass is half empty or half full, be gratefully that you have a glass and there is something in it*.

Kwa tafsiri yake, tunasema: "Asiyeshukuru kwa kidogo na hata kwa kikubwa hawezi kushukuru." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niendelee kufafanua tu kwamba, nchi yetu ina vitu vingi lakini haina vitu vyote, tumshukuru Mungu na tuseme pia Serikali yetu imetekeleza malengo mengi, lakini haijatekeleza malengo yote na hivyo tuishukuru Serikali. Hata Waheshimiwa Wabunge wenyewe bila kujali Wabunge wa CCM, Wabunge wa Vyama vya Upinzani pia tumefanya kazi nyingi Majimboni kwetu, lakini hatujafanya kazi zote. Vile vile hata kwa upande wa Serikali Mawaziri wetu wamefanya kazi nyingi, lakini hawakufanya kazi zote. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kujipongeza na kupeana shukrani kwa kile ambacho tumefanya katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee tujipongeze kwa kushika nafasi ya pili katika *East Africa* kwa ukuaji wa uchumi baada ya nchi ya Rwanda. Ni jambo kubwa na la kujivunia na nina imani kabisa *next time* tutakuwa wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Saada Mkuya, Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake wawili pamoja pia na timu yake nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambazo wanafanya, lakini pia kwa uthubutu na kwa kufanya maamuzi magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maamuzi hayo niseme ni hili suala la kuongeza kodi ya mafuta. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake na nitakuwa kinyume na wenzangu ambao wamekuwa wakipinga suala hili. Sina nia ya kutotaka mafanikio ya wananchi, lakini nitoe maelezo kidogo tu ni kwa nini naona hili ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetuambia kabisa kwamba nia ya kuongeza kodi ya mafuta ya petroli na dizeli ni kuongeza fedha ili kusudi tuweze kutekeleza upande wa *REA*. Kwa upande wa mafuta ya taa siyo kukusanya kodi, ni kwa ajili ya kuzuia uchakachuaji. Kwa mtazamo wangu nadhani kwamba hata tutakapopunguza kodi ya mafuta ya taa kwa mfano, hatutasaidia chochote sana sana tutakuwa tumepunguza kiasi cha mapato yanayokwenda Serikalini ambayo yangeweza yakasaidia utekelezaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano tu kwamba, kama mtumiaji wa gari anataka kununua mafuta petroli lita 20, tukiruhusu uchakachuaji atanunua petroli lita kumi na mafuta ya taa lita kumi. Kwa maana hiyo ina maana ile kodi ambayo inakusanywa itapungua, lakini si kwamba huyu mtumiaji hatailipa, hii kodi italipwa kwa mfanyabiashara wa mafuta, lakini haitakwenda Serikalini. Kwa hiyo, kwa maneno mengine hatutakuwa tumemsaidia sana mwananchi ila tutakuwa tumemdidimiza kwa sababu tutashindwa kumpatia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuliunge hili mkono, lakini niwaombe vyombo vya udhibiti *SUMATRA* pamoja na *EWURA* ifanye kazi yake ipasavyo ili kuweza kudhibiti nauli. Kwa sababu ukiangalia sana kama mtu atanunua petroli labda lita kumi, ongezeko au lita 20 ongezeko litakuwa ni sh. 1,000 tu na wala siyo zaidi katika hizi lita 20. Kwa hiyo, tuone kwamba Serikali inatusaidia lakini kwa kutufanya sisi tuchangie kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa nimpongeze Mheshimiwa Saada Mkuya, ni kuwaondoa Wabunge au kusitisha ujumbe wa Bodi katika taasisi na mashirika. Katika hili niombe tu sasa Serikali baada ya kuwaondoa Waheshimiwa Wabunge katika Bodi hizi, baada ya muda fulani pengine mwaka mmoja au miwili, ije sasa hapa Bungeni ituambie mafanikio yaliyopatikana katika Bodi hizi kwa kuondoa Waheshimiwa Wabunge na iige mfano wa Ofisi ya Rais, Mazingira wakati ilipowaondoa wafugaji Ihefu, baadaye wataalam walikuja na wakatueleza mafanikio ambayo yalipatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, yeye ni Mbunge lakini ni Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho. Mama yetu huyu amefanya kazi nzuri sana katika Bodi ya Korosho, nadhani sote ni mashahidi ameiendesha vizuri Bodi ile na migogoro imepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, naomba aendelee kuwa Mwenyekiti wa Bodi hii ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa kifupi sana, mikopo ya akinamama na vijana, kwa kutenga asilimia 10 ya pato la Halmashauri. Nadhani tumekuwa mashahidi kila Mbunge aliposimama mara nyingi hili lilitajwa sana kwamba hii asilimia 10 haipatikani katika Halmashauri nyingi. Labda nimpongeze Mheshimiwa Mangungu ambaye niliwahi kuongea naye, akasema katika eneo lake wanaweza kulitoa na wanafikia hadi shilingi milioni 600 kuwainua akinamama kwa kuwapa hii mikopo. Kwa hiyo, naomba tuige mfano wa Halmashauri hii, ahaa, ni Mbunge wa Kigamboni kwa hiyo, Halmashauri hii inafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu nilichojifunza ni kwamba, mikopo hii haitoki kwa sababu hatujajipanga vizuri na ukitaka kujua kwamba hatujajipanga vizuri utakuta kwamba, hata kule Halmashauri hakuna utunzaji mzuri wa kumbukumbu. Akinamama wanakopa, wanajitahidi kulipa, lakini baada ya miaka miwili wanafuatwa wanadaiwa tena upya, ni kitu ambacho kinawadhalilisha wanakuwa hata na woga wa kukopa tena fedha hizi. Kwa hiyo, naomba tuwasaidie akinamama wetu na vijana waweze kupata fedha za kutosha ili wajikomboe katika umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuinge mfano wa Halmashauri nyingine kwa mfano Tandahimba wao wameamua sasa kutumia benki ya *TACOBA* kupitishia mikopo hii na Manispaa ya Mtwara-Mikindani pia imeamua kupitisha mikopo hii *NMB*. Kwa hiyo, itatusaidia sana katika utunzaji wa kumbukumbu na kuwezesha mzunguko mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naamini kabisa tukiwa na dhamira ya dhati ya kutoa hii mikopo asilimia kumi tutaweza kwa sababu hebu tuangalie ujenzi wa maabara tumeweza, tumefanya nini hadi tumeweza. Kwa hiyo, tutumie nguvu hizi hizi ambazo tumeziweka kwenye ujenzi wa maabara, ili tuweze kuwapatia akinamama na vijana wetu mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo nimelikuta katika Wilaya ya Nanyumbu, ni ombi maalum kwamba wananchi huwa wanachangia fedha zao kwa kukatwa mazao na zinaingia katika akaunti ya Halmashauri ili kusudi kuhakikisha usalama wa hizi fedha. Sasa wao wanahesabiwa kwamba hili ni kati ya ile asilimia 10 ya mapato ya ndani. Kwa hiyo, wanaomba hizi zisihesabiwe kama ndiyo mapato ya ndani. Kwa hiyo, zihesabiwe tu zile za mapato ya ndani halisi, lakini michango ya wananchi iwekwe kando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu katika malengo ya maendeleo endelevu ambayo nadhani Serikali inashiriki katika Umoja wa Mataifa kuyapanga malengo haya. Niombe Serikali sasa katika moja ya mikakati, ihakikishe kwamba, fedha zinazotengwa katika sekta ya afya na maji inaendana na ongezeko la watu. Napendekeza hili ili kuondoa kule kuyumbayumba kwa

utekelezaji wa malengo, kwa sababu ukiangalia katika sekta hizi utaona kwamba utekelezaji hauendi *uniform*, inapanda inapungua, inapanda, inashuka. Kwa hiyo, tukiweka bajeti kulingana na ongezeko la idadi ya watu nina imani kabisa hata maendeleo yatakuwa *uniform* na yatakwenda katika hali ya kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo ukwepaji wa kodi kwa njia ya kutotoa *receipt*. Hili ni tatizo kubwa, limezungumzwa sana na nimelizungumza tangu mwaka 2005 nilipoingia Bungeni na mapendekezo yangu sijaona kama yamefanyiwa kazi kwa sababu tatizo liko pale pale. Ukienda nchi za wenzetu, huna haja ya kuuliza bei, ukiuliza bei atakwambia angalia *sticker* hana sababu ya kukujibu kwa sababu *sticker* zipo ni tofauti unapokwenda Kariakoo, kitu chenye thamani ya shilingi milioni tatu, milioni moja, milioni mbili hakijabandikwa *sticker*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ndipo wizi unapotokea kwa sababu yeye atakwambia milioni mbili na nusu wakati ni milioni mbili. Utakapodai *receipt* anakwambia ongeza hela ya *VAT* anaipigia *percent* 20 utakuta ni hela nyingi na wengi hawapewi *receipt*. Kwa hiyo, niombe tufanye kama wanavyofanya *shopping mall*, kama wanavyofanya *supermarket*, kila *item* dukani inakuwa na *receipt* yake. Tukifanya hivi nina imani tutaongeza mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hata katika nchi za wenzetu siyo rahisi sana kukuta mashine za *EFD* zimeharibika, ni kwa nini kwetu kila unapokwenda unakuta mbovu, ni kwa nini zetu zinakuwa mbovu, sijawahi kukuta tatizo hili katika nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niongelee kidogo kwa kifupi kuhusiana na kushuka kwa thamani ya shilingi, kwamba sababu mojawapo ni kushuka kwa bei ya dhahabu. Hebu tuangalie nchi kama South Africa, ni nchi ya kwanza katika Afrika kwa kuuza dhahabu lakini je, thamani ya shilingi yake au ya *rand* yake imeshuka kama ilivyoshuka ya kwetu? Jibu ni kwamba uwepo wa viwanda wana viwanda vingi, lakini hata nchi ya Morocco pia haikukumbwa na mtikisiko wa uchumi kwa sababu ya viwanda na nchi peke katika Afrika ambayo haikukumbwa na mtikisiko wa uchumi. Kwa hiyo, niiombe Serikali tufanye mjadala wa Kitaifa, kuhusiana na viwanda ili kusudi tuone ni jinsi gani tunaweza tukaiinua nchi yetu kwa njia ya uanzishaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kufanya kazi ya leo, lakini niwashukuru pia wanawake wa Mkoa wa Mtwara kwa kuniunga mkono na niwataarifu tu kwamba Mungu akitujalia nitarudi tena kwao kuomba ridhaa ya kuwatumikia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote pamoja na Serikali kwa ujumla. Vile vile nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, mchakamchaka anaotupa ni mkali kweli kweli na naomba wapiga kura wa Peramiho waturudishie jembe letu katika uchaguzi mkuu ujao. Niwatakie mfungo mwema wa Ramadhani Waislam wote na Wabunge wote niwatakie kila heri katika uchaguzi mkuu. Basi niombe tena Mwenyezi Mungu aturudishe hapa katika Bunge lijalo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Kombo khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kafulila!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Watallah* na kumtakia Rehema na Amani Mtume wetu Muhammad *Swallallah alayh wasalaam*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mgogoni ambao nimewatumikia kwa kipindi cha miaka minne na nusu sasa bila mikwaruzano, tumekwenda vizuri, tumeingia kwenye mchakato wa uchaguzi na aliyeshinda nitamsimamia ili nihakikishe kwamba kiti alichokuja kukikali ni kiti cha *CUF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niushukuru pia uongozi wangu wa Taifa, maamuzi yaliyotolewa ni maamuzi sahihi, nayaheshimu, nitaendelea kuyaheshimu na nitayasimamia mpaka tuhakikishe kwamba UKAWA imechukua hatamu za dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, jana kulitoka lugha ya kwamba kwenye Vyama vya Upinzani kuna viongozi waliofukuzwa, mimi sitaki nikumbushe mengi kwa sababu nakumbuka kuwa Maalim Seif Sharif Hamad, Shaban Khamis Mloo, Ali Haji Pandu, Machano Hamis Ali, Khatib Hassan, Hamad Rashid ambaye leo mnamng'ang'ania, Maulid Makame, Suleiman Seif Hamad, Sudi Yusuph Mgeni, Juma Ngwali Kombo, Masoud Omar Said, wote walikuwemo ndani ya CCM na CCM ikawafukuza na juzi amefukuzwa Mansour Yusufu Himid na Mzee Hassan Nassoro Moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kwamba, kama ni kufukuza, iliyoanza kwanza ni CCM. Kwa hiyo, mtu yeyote akionekana kwamba ana kosa, upande wenu, hata kama anaitetea Zanzibar, maana yake makosa yao hawa ni kuitetea Zanzibar, si lingine lolote. Kosa lao no kuitetea Zanzibar, hili ndilo kosa lao na kama kosa lao si kuitetea Zanzibar, nitajieni viongozi wawili, watatu kutoka Tanganyika ambao wamefukuzwa ndani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba,

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa utulivu!

**MBUNGE FULANI:** Kabwagwa huyo.

**MBUNGE FULANI:** Changia kuhusu bajeti.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Hata wewe vile vile, jana ulichangia, wala ilikuwa halihusiani na bajeti, kwa hiyo, achia nichangie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ongea na Kiti.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaendelea kuongea na Kiti.

**MBUNGE FULANI:** Ana uchungu kafukuzwa huyo.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Sijafukuzwa ndani ya chama changu na nakiheshimu sana.

**MBUNGE FULANI:** Umekataliwa Jimboni! Umebwagwa Jimboni.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaloliulizia na ambalo Wanzanzibari mpaka leo wanalihoji, ni kuhusiana na wafuatao:-

Huyu Abdallah Kassim Hanga, Abdul-Aziz Twala, Ubwa Jaha, Othman Sharif, Mdungi Ussi, Hamis Masoud, Suleiman Amour na Twaha, wako wapi? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** *Izbu* wenzio hao.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Kama wamefungwa, basi tuonyeshwe gereza walilofungwa.

**WABUNGE FULANI:** Wamenyongwa hao.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Kama wamenyongwa basi tuonyeshwe ni wapi walipozikwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ongea hoja inayojadiliwa.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja sasa.

**MBUNGE FULANI:** *Shame*.

**MBUNGE FULANI:** Haina mantiki.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** *Shame* mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya kodi ambayo Watanzania wanatakiwa wakusanye, Serikali inatakiwa ikusanye mapato ambayo yanatokana na Watanzania zaidi ya milioni 11 wanaotakiwa kulipa kodi, zaidi ya Watanzania milioni 11 wanatakiwa walipe kodi, lakini wanaolipa kodi si zaidi ya milioni mbili na kidogo.

**MBUNGE FULANI:** Wapemba wangapi!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Hivyo, Serikali hii, inayosema kwamba itajitegemea katika kuendesha bajeti ya Serikali, itajitegemea vipi, ikiwa kuna watu karibu milioni tisa hawalipi kodi, lakini *formal sector,* sekta iliyorasmi, ndiyo pekee ambayo Serikali inakusanya kodi kutoka sekta hiyo. Sekta isiyo rasmi, hakuna makusanyo ambayo Serikali inayapata. Sasa Serikali hii itakwenda vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo karibu miaka yote minne na nusu ambayo leo naingia hii ni bajeti ya tano, kila makusanyo au kila bajeti inayopitishwa, basi bajeti inayokwenda katika matumizi ya maendeleo ni ndogo, kuliko bajeti inayopangwa. Karibu asilimia 40, haifiki, sasa sijui Serikali imekusudia iendeshe nchi hii vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hilo halitoshi, mwenzangu pale kaligusia, wenzetu wa Afrika Kusini, wenzetu Afrika Kusini, unapoingia pale kutaka kubadilisha fedha, yaani dola, ni lazima uwe na *passport*. Leo dola Tanzania inabadilishwa kama njugu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu twambieni ni mapato gani ambayo yanapatikana katika hizi *Bureau De Change*s zilizopo Tanzania, maana yake Tanzania zimeenea *Bureau De Changes* kila pembe na hili ndilo linalosababisha kushuka kwa shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mrahaba, Rais Kikwete alipoingia madarakani, alisema kama yeye atafanya *review*, ili madini yaweze kuleta pato la Taifa, lakini, pato la Taifa linalotokana na madini ni asilimia tatu. Wawekezaji kutoka nje, wanachukua asilimia 25, 30, hivyo Tanzania inafaidika vipi na madini yanayotoka Tanzania? Kwa nini hatuzuii utafutaji wa madini mpaka pale Tanzania itakapoona kama sasa inajiweza ili iweze kusimamia madini yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasema, kwamba, chini ya utawala wa CCM, basi Tanzania haiwezi kufika mahali popote. Ila mkubali zamu hii, mkabidhi madaraka kwa UKAWA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayoyasema, siyasemi kimasihara, kabisa kabisa, mmeshindwa! Mmeshindwa kuiendesha nchi, CCM mmeshindwa kuiendesha nchi na sasa umefika wakati Watanzania mjue kama madini yenu yanapotezwa, yanachukuliwa ovyo, wageni ndiyo wanaofaidika na nyie Watanzania mnazidi kudidimia, siku hadi siku.

**MBUNGE FULANI:** Na wauzaji madini ni nyie.

**MBUNGE FULANI:** Hakusikika.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Nyamaza mwenyewe na kama ni Mabodi namwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea, wewe usiwajibu wale, wewe unaongea na kiti, una wajibu kazi yako wewe kuwajibu? Ongea na kiti.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa. Baada ya kusema hayo niliyoyasema, lakini nirudi kusema kidogo kuhusiana na suala la mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna mwenzangu alizungumzia kama anayegombea nafasi ya Urais Zanzibar amewadanganya wananchi kwa kusema kuwa ataachia kodi ya mchele. Namshangaa sana, ndugu yangu, mwenzangu, nakumbuka kuwa Rais Karume aliwahi kuachia kodi ya mchele, mchele ulikuwa haulipiwi kodi Zanzibar. Si hilo tu, Zanzibar ulikuwa unatoka mchele pale, Unguja kwenda Pemba, pia ulikuwa haulipiwi.

**MBUNGE FULANI:** Aaa, kwenda nchi moja utalipiwaje!

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Kwa sababu bei ya Unguja iweze kulingana na bei ya Pemba!

**MBUNGE FULANI:** *What is this!*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Sasa mtu akisema kwamba Maalim Seif anadanganya, namwona huyo kachanganyikiwa.

**MBUNGE FULANI:** Umechanganyikiwa wewe.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, niseme kwamba Zanzibar inajiweza, wale wanadai kama Zanzibar haijiwezi, wasijidanganye, Zanzibar inajiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar imeshaisaidia hata Tanganyika, Zanzibar imeisaidia *Vietnam* ambao ni wazalishaji wakubwa wa mchele, imewasaidia katika vita vyao. Sasa mtu akisema kwamba Zanzibar hajiwezi, basi huyo anajindanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niseme kwamba hakuna Mzanzibari au kiongozi yeyote kutoka Zanzibar, aliyesimama akasema kama yeye anapingana na Muungano, hakuna. Hao wanaosema hivyo ni waongo, ni wanafiki na hakuna. *(Makofi)*

Sisi tunalosema, Muungano tunaoutaka ni Muungano wa Serikali tatu na hilo si kosa!

**WABUNGE FULANI:** Mmesema mkataba.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tunasema kwamba, Muungano uwe na makubaliano ya pande mbili za Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar! Siyo Muungano huu tulio nao. Muungano wa watu mia kwa mtu mmoja, si Muungano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo ahsante sana. Sasa …

**MBUNGE FULANI:** Wewe nini wewe.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Wewe nyamaza kimya wewe.

**MWENYEKITI:** Naomba nimwite Mheshimiwa David Kafulila! Waheshimiwa naomba utulivu.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya mwisho katika utawala wa Awamu ya Nne ambao ulianza mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida ilikuwa ni matarajio ya kwamba bajeti hii iweze kutoa tathmini ya namna gani ambavyo Serikali ya Awamu ya Nne ime-*perform*, kwa misingi ya bajeti, kuanzia mwaka 2005 mpaka mwaka 2015. Kwa hiyo, kwa kuwa bajeti haikuweka mambo hayo, pengine nichukue nafasi hii ya kwanza kabisa, kuweza kueleza kwamba ni kwa nini tunasema kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tatu wakati inaingia madarakani, Awamu ya Tatu, wakati inaingia madarakani, ilikuta riba, kwa mfano, ya mabenki, ilikuwa asilimia 30, lakini mpaka inamaliza muda wake mwaka 2005, riba za mabenki zilishuka mpaka asilimia 14. Awamu ya Nne imeingia kutokea hapo, mpaka sasa miaka 10 riba za mabenki zimepanda asilimia 18 mpaka 20, hilo ni tatizo la kwanza ambalo liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tatu, mwaka 2005 imeacha deni la Taifa ni trillioni 10, Awamu ya Nne kwa miaka 10, imekuza deni la Taifa mpaka trillioni 35, kiasi ambacho ni kikubwa mno na ni kiasi ambacho ni kikubwa ilhali hatuoni kitu ambacho kimefanyika kwa mujibu wa deni hilo. Kwa sababu deni siyo tatizo, kuna nchi mbalimbali tu, Japan, Marekani, China, wana madeni makubwa, lakini ni lazima ile thamani ya deni ionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni yangu, kwamba deni la nyongeza la trillioni 25, ilitosha kabisa tuoneshwe kwamba kuna reli ya kati imejengwa, tuoneshwe kwamba kuna bandari ya

Mtwara, kuna bandari ya Tanga, Kigoma, Mwanza, lakini tuna deni kubwa la matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwaka 2005, uchumi wa Tanzania ulikuwa unakua kwa asilimia 6.7, mpaka leo, mwaka jana uchumi ulikuwa unakua kwa asilimia 6.4. Kwa maneno mengine, Serikali ya Awamu ya Tatu iliweza kujenga msingi wa kutosha wa uchumi. Mfumko wa bei mwaka 2005, wakati Mkapa anaingia, mfumko wa bei ulikuwa unafika asilimia 30, Mkapa kwa miaka 10 alishusha mfumko wa bei mpaka asilimia nne, leo mfumko wa bei ni asilimia 5.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda mbele, tunarudi nyuma, ilipaswa kutokea Awamu ya Tatu, tujenge msingi wa uchumi mkubwa kutafsiri uchumi wa kawaida. Ilikuwa ni kazi ya Serikali ya Awamu ya Nne, kubadilisha *macroeconomics* iweze kutafsri zile *micro indicators,* ilikuwa ni uchumi mkubwa uanze kutafsiriwa kwenye maisha ya watu ili watu waanze kuona thamani ya ukuaji wa uchumi wao. Leo tunazungumza kwamba uchumi wa Tanzania ni mkubwa, ni miongoni mwa nchi 10 katika Afrika, ni miongoni mwa nchi 20 duniani. Ni kweli, lakini kiasi hiki cha ukuaji wa uchumi hakijaanza leo, tangu wakati wa Mkapa, Mkapa ameacha uchumi unakua kwa kasi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokisema hapa ni kwamba, miaka 10 hii tumebomoa misingi iliyokuwa imeachwa ya uchumi mkubwa uliokuwa umejengwa, badala ya kufanya kazi ya kufanya uchumi mkubwa utafsiri uchumi mdogo ambao ni wa watu wa kawaida, tunafanya kazi ya kubomoa hata huo uchumi mkubwa uliojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa leo, Mheshimiwa Mkapa wakati anaondoka madarakani, akiba ya fedha za kigeni, Mkapa ameingia madarakani, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ya miezi miwili, anaondoka akiba ya fedha za kigeni mwaka 2005, miezi minane, Kikwete anaondoka leo akiba ya kigeni miezi minne, tunatoka nane, tunakuja nne. Kwa hiyo, ni wazi kwamba tumevunja misingi ya uchumi mkubwa uliojengwa na Mkapa kwa miaka 10, sasa tunaanza kutetereka tena kujenga upya uchumi huu huu. Ni mazingira kama haya, yanaweka wazi kwamba, hiki chama hakina namna ya kutufikisha mahala ambapo Watanzania tunahitaji! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo ambayo katika hali ya kawaida hayavumiliki, nchi kama hii ambayo ina misitu mikubwa ya mbao katika Afrika, watoto kubaki wanakalia mawe kujifunza, ni aibu! Haina itikadi ya chama hii! Kwa mujibu wa taarifa ya Haki Elimu ya mwaka huu, upungufu wa madawati ni 1,170,000. Kama kila dawati moja wanakaa watoto watatu, maana yake tuna takribani zaidi ya watoto milioni tatu wanakalia mawe kusoma, hii haivumiliki! Lazima tukubaliane kwamba kuna tatizo, haiwezekani, wakati wenzetu Wakenya, wanaweka mpango wa kuhakikisha kwamba kila mtoto kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari, anakuwa na *laptop* na kompyuta, sisi bado tunahangaika pa kukalia, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mapato katika nchi hii, vipo, lakini tunaua nchi tu na tunaiua hii nchi kwa *materials*, hata kwa *philosophy*. Leo hii taarifa ya *USAID*, kwenye utafiti wao ambao wameutoa mwezi wa Tano, wanaonesha kwamba asilimia 34 ya Watanzania, wako chini ya mstari wa umaskini, lakini taarifa ya *USAID* hiyo hiyo, ya mwezi Desemba, 2014, inaonesha kwamba watoto wanaohitimu shule ya msingi, asilimia 70 hawajui kusoma vizuri Kiswahili na asilimia 90 hawajui kusoma vizuri Kiingereza. Tunajenga Taifa jipya kabisa la watu ambao hawana maarifa, matokeo yake wanakosa juhudi, wanakosa uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia hii ni dunia ya ushindani, Rais anapoingia madarakani, lazima aangalie anatengeneza binadamu wa namna gani, Mungu anafanya kazi ya kuumba, lakini Serikali inapaswa kuangalia, inamtengenezaje huyu binadamu ili aweze kuishi katika mazingira haya. Tunahitaji kutengeneza binadamu ambao hata nchi hii isipokuwa na gesi isipokuwa na madini, ikiwa jangwa, bado wataishi, ndiyo tofauti yetu kubwa kati ya sisi na hao walioendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zinazoongezwa kila siku ni za mazoea, mnaongeza kodi kwenye mafuta, *multiply effect* yake na bahati nzuri, Wizara ya Fedha imejaa Wachumi, ni wazi kwamba *effect* ya kodi ya kwenye mafuta ni kubwa kwenye maeneo mengine, ni kweli kwamba mna dhamira ya kutaka mapato kwa ajili ya umeme kwangu nahitaji umeme. Nguruka wanataka umeme, Kigoma Kusini yote inataka umeme, lakini siyo kweli kwamba Serikali hii haina vyanzo vingine vya fedha za kupeleka huo umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukua mfano, tangu mwaka 2007 sijawa Mbunge, mpaka leo, tunapiga kelele Bungeni, kutaka Kampuni za Simu zilipe kodi sahihi! Tukataka mtambo wa kurekodi matumizi ya simu, kila atakayepiga simu, ili kusudu Serikali ijue kwamba ni kiasi gani ambacho kimeingzwa na *Tigo* na *Airtel* na *Vodacom*, lakini mpaka leo, pale *TCRA* wamenunua mtambo tu wa kurekodi simu za kuingia nje na kutoa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatuchukua miaka mingapi, Rwanda wana mtambo kama huo. Tunapoteza mapato mengi, Kampuni za Simu zinatengeneza *trillions of shillings* kwa mwaka, lakini hakuna menejimenti, hakuna udhibiti ili mapato haya yaweza kusaidia nchi yetu, hakuna. Sasa mpaka leo, tangu mwaka 2007, mpaka leo mmeshindwa kununua mtambo wa kurekodi *transactions* za simu, matokeo yake mnapata kodi kiduchu, matokeo yake mnahamisha hasiraz enu kwenda kwenye mafuta kuumiza akinamama, kuumiza wazee, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo ya kimsingi, leo hii wafanyakazi wa Tanzania kwa takriban nusu karne bado hawajaona tija ya chama hiki ambacho ni asili ya harakati zao. Wafanyakazi wa Tanzania ndiyo ambao waliasisi chama hiki na ndiyo asili ya jembe na nyundo pale, nyundo ni wafanyakazi. Kodi ambayo wafanyakazi wa Tanzania wanatozwa ni kubwa kuliko nchi yoyote Afrika Mashariki na hizi ni *facts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya mwaka wa jana mwezi wa Kwanza, ambayo ni utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Taasisi ya ukaguzi ya *PricewaterhouseCoopers* ya Januari 2014, inaitwa *the Global Tax Comparison* (Ulinganishi wa Kodi Duniani), unaonesha kwamba wastani wa kodi ya mfanyakazi Tanzania ni asilimia 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hii wakati fulani wakasema ni asilimia 12, asilimia 11. Ile 12 au 11 ni *minimum*, ni kodi ya kiwango cha chini, lakini wastani, leo Wabunge na wafanyakazi wengine wanatozwa kodi mpaka asilimia 30, wastani wa kodi ya mfanyakazi wa Tanzania ni asilimia 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini ya Kenya Chama cha Wafanyabiashara ambacho kinaongoza Kenya, kodi ni wastani wa asilimia 6.8, Uganda wastani ni asilimia 11, Burundi asilimia 10.3, Tanzania asilimia 18, Rwanda ni asilimia 5.6. Hawa wafanyakazi mnawaaminishaje kwamba hii nchi ni nchi yao. Mnawatoza kodi kubwa mno, lakini mnawatoza kodi kubwa kwa sababu vile vyanzo vikubwa vya kodi hamtozi. Nimezungumza tangu 2012, migodi hamtozi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna sheria zilitungwa hapa kutaka migodi na kampuni za simu zilipe kodi, hiyo ya simu nimeshaizungumza. Tulizungumza migodi ilipe kodi na ndiyo matokeo ya Tume ya Rais, Mwenyekiti wake akiwa Bomani. Ile ni sheria ya 2010. Leo Serikali tangu 2010 mpaka leo wanasema kwamba si rahisi kumlazimisha mtu a-*list share* zake kwenye *stock market*. Ni kweli, inawezekana si rahisi, lakini sheria tulipitisha hivyo, *otherwise* mseme kwamba ile sheria haifai, mlete Bungeni hapa tuifute, lakini wote huu uoga, Serikali hii ni dhaifu kuweza kukabili mashirika makubwa, inashindwa kukabili migodi mikubwa kwa sababu udhaifu huu wa kifisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Afrika ni Serikali ndogo ndogo, mnapoingia kwenye uchumi wa soko huria mnakabiliana na makampuni makubwa. Kwa mfano *Stateoil revenue collection* yake ya mwaka bilioni mia moja na nane, 2012. *Revenue collection* ya Tanzania bilioni nane kwa mwaka, hizo ni Dola. Katika hali ya kawaida Serikali dhaifu ya kiasi hiki kukaa na makampuni kama hayo inahitaji uadilifu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji Serikali ikusanye kodi. Kwa mfano, mmewadanganya wazee, Sera ya Wazee tangu mwaka 2006; mwaka 2006 ilipitishwa Sera ya Wazee wakati Kikwete ana mwaka mmoja, miaka kumi baadaye, yaani leo ndipo Serikali inazungumza kutengeneza sheria ya kutekeleza sera hiyo. Hii ni aibu, mnawadanganya wazee, mtapata laana! Sera ikishatungwa kinachofuata ni sheria. Sasa sera mmeitunga 2006, miaka yote mmeuchapa usingizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya tunazungumza hapa hata Mawaziri wenyewe hawapo, wote wako wanagombea, kila mmoja anahisi anaweza akawa Rais, *this is shame*. Tunazungumza hapa na Waziri wa Fedha na Naibu wake na mama Nagu tu, wengine wote hawapo hapa, Serikali iko wapi hii? Kuna masuala yanahusu maji hapa, kuna masuala yanahusu mifugo, Waziri wa Fedha hawezi kujibu kila kitu. Kuna masuala ambayo Serikali inapaswa kuwepo, mmechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Wazee ipo tangu 2006, sheria hamjaitengeneza, mnataka sheria itungwe sasa, ni wazi huu ni utapeli kwa wazee, wazee 2,600,000 walioko Tanzania mnawatapeli mchana kweupe. Ni jambo la aibu, waambieni tu kwamba hamuwezi na UKAWA tukiingia tuwakumbuke kwa sababu ndilo jukumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya fedha nchi hii vipo. Ukiangalia kule kwenye *deep sea*, ukanda wa bahari wa Tanzania na Namibia ni kama unalingana, Namibia ni Kilometa 1,500, Tanzania kilometa 1,424, ni kama tunalingana, lakini kwenye vyanzo vya mapato Namibia ukiacha madini, ya pili ni *fishing*, ni uvuvi. Sisi tumeshindwa kutoza kodi kwenye maeneo ya *deep sea*, meli zinavua hakuna kodi kwa miaka yote hiyo, mnataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi kama ya Mwadui, kila siku narudia, tangu uhuru mpaka leo wanasema wanapata hasara, hamtozi kodi mnang'ang'ania kutoza kodi kwenye mafuta, mnang'ang'ania kutoza kodi wafanyakazi, *this is shame!* Haiwezekani! Hii nchi inahitaji apatikane kiongozi ambaye anaweza akatoza kodi makampuni na migodi mikubwa, tofauti na hapo mnanyonya watu, huu ni unyonyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalia kilio cha maji hapa kila siku, ni aibu. Tunalia maji, tunalia umeme, tunalia wafanyakazi, mimi nina wafanyakazi wangu, kule wazee wangu nusu wameshafariki, wanadai mafao yao, pesa kiduchu, milioni mia tatu arobaini, lakini kwa sababu Serikali haikusanyi kodi inashindwa namna gani ya kuwalipa, kila siku ni kushoto, kulia, kushoto,

kulia. Hii si nchi ya kuishi hivi, hii si nchi ya kuishi kidhalili kiasi hiki, haiwezekani. Tunahitaji Serikali ambayo inaweza ikafanyaba haya yatokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyazungumza haya na tunaendelea kuyazungumza na muda umekwisha wa miaka 10, tunakwenda mwaka 2015. Niseme tu kwamba ni wito kwa Watanzania tukubaliane kwamba haya maisha tunayoishi si halali yetu, si halali yetu, haya ni maisha ambayo tunaishi kwa kushinikizwa. Tupo kwenye nchi yenye kila sababu ya kuishi vizuri; tuna maji ya kutosha, tuna dhahabu za kutosha, tuna *tanzanite* ya kutosha. Dunia nzima nchi pekee yenye madini ya *tanzanite* ni Tanzania lakini muuzaji mkubwa wa *tanzanite* ni Thailand, yaani kama itokee kwamba wakati Kigoma ndio wenye michikichi peke yao muuzaji wa maweze awe Mkoa wa Iringa. Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dola kwa mfano, Hotuba ya Wizara ya Fedha imeshindwa kutoa majibu kwamba inawezaje kudhibiti tatizo la sarafu yetu. Sarafu yetu hii inaporomoka kwa sababu tunatumia dola nyingi kuagiza vitu nje, hata vingine ambavyo si vya lazima. Mheshimiwa Mary Nagu anafahamu kama mchumi. Leo Tanzania tunapoteza zaidi bilioni mia nne hamsini kuagiza mafuta ya kula. Hivi inawezekanaje?

Nchi ya Malaysia, moja ya nchi ambazo walijifunza kuhusu mawese ni Kigoma, Tanzania. Leo Tanzania katika uagizaji wa bidhaa, ukiacha mafuta ya mitambo, mafuta ya kula ndiyo namba mbili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kafulila. Sasa namwita Mheshimiwa Mussa Haji Kombo! Hayupo, basi msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Selamani Zedi!

**MHE. SELEMANI SAID ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema ambayo imeniwezesha leo kusimama hapa na kuchangia bajeti hii ambayo ni bajeti ya mwisho katika muda wetu wa Bunge hili tulilo nalo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila utulivu, Mheshimiwa utulivu.

**MHE. SELEMANI SAID ZEDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kwa dhati kabisa niwashukuru wananchi, wapiga kura wote wa Jimbo la Bukene kwa namna ambavyo katika kipindi chote cha miaka mitano ambacho wamenipa heshima ya kuwatumikia, wamekuwa wakiniunga mkono kwa dhati kabisa na kwa kweli wamenitendea haki kwa namna ambavyo wamekuwa wakini-*support*, nawashukuru sana na nadhani kwamba nimetimiza matarajio yao na inshallah Mwenyekiti Mungu akipenda mwaka huu tena nitawaomba ridhaa ya kuwatumikia na *Inshallah* watanipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika kuelezea mafanikio na changamoto ambazo katika kipindi hiki cha miaka mitano zimepatikana na hasa ndani ya Jimbo langu la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni umeme. Kwa mara ya kwanza ndani ya miaka hii mitano Jimbo la Bukene limefanikiwa kupata umeme katika vijiji zaidi ya 20. Jambo ambalo linanifurahisha kama mwakilishi wao ni mwitikio mkubwa wa wananchi wa kuhitaji huduma hii muhimu ya umeme. Mwitikio ni mkubwa mno kiasi ambacho pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini na *TANESCO,* lakini bado mahitaji ni makubwa sana. Mimi kama mwakilishi wao naomba nichukue fursa hii, pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na meneja wa *TANESCO* pale Nzega, bwana Mashauri lakini bado mahitaji ni makubwa; nguzo hakuna, waya hakuna na mahitaji bado makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bukene Mjini peke yake, pamoja na kwamba sasa hivi zaidi ya wananchi 500 wa pale mjini tu wananufaika na huduma hii, lakini utakuta kwamba maeneo ya Mwenge kule bado mahitaji ni makubwa, nguzo hakuna, maeneo ya Mwantoba, maeneo ya Iluluma, maeneo ya Nyenze bado mahitaji ni makubwa mno, katika taasisi, katika nyumba binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu, juzi nilikuwa kule, maeneo ya Nyenze pale baba Mchungaji Njige kuna nyumba yake ya ibada pale wamefanya *wiring* zaidi ya miaka miwili sasa, lakini tunapambana kupata nguzo na waya bado hatujafanikiwa. Kwa hiyo napenda nitumie nafasi hii niwaombe viongozi wa *TANESCO* wa Mkoa wa Tabora na kanda ya Nyanda za Juu kwa ujumla waweze kumsaidia Meneja wa *TANESCO* wa Nzega ili aweze kupata nguzo za kutosha, apate waya za kutosha ili maeneo hayo niliyoyataja mahitaji yao yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumefanikiwa kupata mradi mwingine ambao utapeleka umeme Kata ya Mambali, ni *line* ya kilometa 44, kwa hiyo itapita vijiji vingine na Kata nyingine kama Mbutu, Mogwa, lakini vile vile tuna *line* ya umeme ambayo itapeleka Kata ya Mwangoye na huyu Mkandarasi *CHICO* atakapomaliza miradi hii miwili atahamia kwenye Kata nyingine ya Mwamala na Igusule ambako pia mahitaji ni makubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba, pamoja na mafanikio ya nishati hii ya umeme ambayo tumeyapata lakini bado wananchi wa Bukene wana kiu kubwa, wana mwitikio mkubwa na bado wanahitaji sana. kwa hiyo niitake Serikali sasa kupitia Wizara ya Nishati na Madini, kupitia Shirika la *TANESCO* na hasa *TANESCO* Tabora na Wilaya ya Nzega kujitahidi kadiri inavyowezekana kupata nguzo, kupata waya, kupata mita na vifaa vyote ili mahitaji yaweze kutimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo kama mwakilishi wa wananchi lazima nishukuru ni upatikanaji wa maji ndani ya miaka hii mitano. Katika Jimbo langu la Bukene ndani ya miaka mitano zaidi ya wananchi 20,000 ambao hawakuwa na maji sasa tumewapatia maji. Kuna miradi sita ya visima virefu imekamilika ndani ya miaka hii mitano. Sasa wanachi wa Itobo ambao hawakuwa na uhakika wa maji safi na salama sasa wananufaika na huduma hiyo, wananchi wa Mahene, Buhondo, Nawa, Sigili na Ikindwa. Maeneo yote hayo ndani ya miaka hii mitano wameweza kufanikiwa kupata huduma ya visima virefu ambavyo sasa vimewawezesha kupata maji ya uhakika, maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo dogo kuwezesha wananchi zaidi ya 20,000 ambao hawakuwa na maji sasa kupata maji. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile kama mwakilishi wa wananchi nachukua fursa hii kuipongeza Serikali pamoja na kwamba bado maeneo mengine yanahitaji huduma hii ya maji. Kuna Kata za Ikindwa, Isagenhe, Mogwa, Semembela, bado zinahitaji maji, lakini ni lazima nishukuru kwamba wananchi 20,000 kuwapatia maji ni jambo ambalo ni la jitihada kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bukene Mjini, Mji ambao unakua na una wananchi wengi, Halmashauri ya Nzega ina milioni arobaini na tano ambazo tayari mchakato wa kuboresha mfumo wa maji uliopo, umeshaanza, kwa maana ya kukamilisha taratibu za Mkandarasi ambapo tunakwenda kuongeza magati sita ambayo yatawezesha maeneo ya Ikena, Mwantoba na maeneo ya Migombani ambayo hayakuwa na magati sasa yatapata magati ya maji ili wanachi waweze kunufaika na huduma muhimu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo kama Mwakilishi ndani ya miaka mitano inabidi nishukuru mafanikio ambayo yamepatikana ni eneo la barabara. Ndani ya Bunge la Bukene kulikuwa na Kata mbili ambazo hakuwa zikifikika kabisa, zilikuwa hazina barabara kabisa. Sasa hivi Kata ya Semembela ambayo iko zaidi ya kilometa 40 kutoka Makao Makuu ya Jimbo sasa inafikika, imepata barabara na juzi nilikuwa kule, Mkandarasi anamalizia kukata miti na kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mara ya kwanza sasa, Kata hii ya Semembela sasa inaweza kufikika kwa barabara ya uhakika. Hata hivyo, tunakamilisha kutoboa barabara kwa ajili ya Isagenhe mpaka maeneo ya Buhulyu kule ambako pia changamoto yao kubwa ni upatikanaji wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni mafanikio dhahiri, ya wazi ndani ya Jimbo la Bukene ndani ya miaka hii mitano ni kukamilika kwa vyumba viwili vya huduma ya upasuaji. Chumba cha kwanza ni katika Kituo cha Afya cha Bukene, Makao Makuu ya Jimbo, lakini chumba kingine ni katika Kituo cha Afya cha Itobo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza sasa huduma za upasuaji za kisasa zitaanza kupatikana. Nilifanya mazungumzo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kebwe muda wowote kuanzia sasa tunakwenda kuzindua huduma za upasuaji katika vituo vya afya hivi viwili. Kituo cha Afya Bukene na Kituo cha Afya cha Itobo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana kwa sababu uwepo wa huduma ya upasuaji maana yake ni kuokoa maisha ya akinamama na watoto. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa vigezo vyovyote vile ni jambo ambalo kama mwakilishi nastahili kulipongeza, kwa sababu kwa mtazamo wangu sioni kama kuna jambo kubwa lolote kushinda jambo la kuokoa maisha ya watu. Kwa hiyo, huduma za upasuaji kwangu naona ni kuokoa maisha ya watu, hasa akinamama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kukamilisha na nichukue fursa hii kuwaambia wananchi wa Jimbo la Bukene kwamba wakae mkao wa kujiandaa muda wowote kuanzia sasa kwa sababu jengo limekamilika, vifaa vya upasuaji vya kisasa vimeshafungwa, vimeshafanyiwa majaribio, Madaktari wa upasuaji wameshaandaliwa, kwa hiyo, sasa ni kwenda kuzindua ili upasuaji uanze. Kwa hiyo ni jambo la kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililozungumzwa hapa ni suala la mafao ya wazee. Wote tunafahamu umuhimu wa wazee katika nchi hii, wazee ni watu ambao wametoka jasho na ndiyo hasa wametufikisha hapa tulipo. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile kuna kila haja ya kuweka mazingira mazuri ili wazee waweze kunufaika. Kwa hiyo, mtu yeyote makini ambaye yuko katika nafasi ya kufanya maamuzi wakati akiwa na nguvu za kufanya kazi hawezi kupuuza suala la maandalizi ya mafao ya wazee, kwa sababu leo uko kijana, una nguvu unaweza kufanya kazi, lakini kesho wewe pia utakuwa mzee. Kwa hiyo, unapoweka maandalizi mazuri kwa ajili ya mafao ya wazee maana yake hata wewe unajiwekea. Kwa hiyo, niipongeze Serikali kwa kuliona hilo. Rai yangu hapa kwa Serikali ni kuongeza *speed* (uharaka).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza zoezi la kuwatambua wazee wote nchi nzima na kuanza kupanga namna ambavyo watalipwa na taratibu zingine, ambalo ni jambo jema.

Mheshmiwa Mwenyeiti, kwa hiyo hapa mimi rai yangu tu ni kwamba zoezi hili liende haraka, lakini naunga mkono asilimia mia moja kwamba, ni lazima tutengeneze mazingira yatakayowezesha wazee kujulikana na hatimaye kupata mafao kwa sababu sisi wote hatimaye tutakuwa wazee, hakuna mtu ambaye ana ujanja wa kukwepa uzee, wakati wowote tutakuwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa mantiki yoyote ile ni jambo la busara kujiandalia mazingira kabla hujazeeka kwa sababu mwisho wa siku na wewe utakuwa mzee halafu mazingira hayo na wewe pia yatakunufaisha. Kwa hiyo, naunga mkono hilo lakini rai yangu kwa Serikali ni kwamba, jambo hilo liende haraka ili wazee waanze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema mafanikio na changamoto kwenye maeneo ya umeme, maji, barabara, afya, kwa maana ya upatikanaji wa upasuaji katika kituo cha afya cha Bukene na cha Itobo na suala la mafao ya wazee, nitumie tena fursa hii, kwa sababu ni Bunge la mwisho sasa hili, kwa mujibu wa kanuni zetu na taratibu zetu, kuwashukuru tena kwa mara nyingine wapigakura na wananchi wote wa Jimbo la Bukene heshima kubwa ambayo wamenipa ya kuwatumikia.

Kama nilivyosema mwanzoni *Inshallah* Mwenyezi Mungu akipenda na tukiwa wazima nitakuja kuwaomba tena ridhaa ya kuendelea kuwatumikia. Nina imani kwamba nimekidhi matarajio ambayo wananchi wa Bukene walikuwa wanayataraji na kwa maana hiyo wananchi wa Bukene kwa moyo mmoja, naamini kabisa wataungana nami kunipa tena ridhaa ili niweze kuwatumikia kwa miaka mingine mitano na *Inshallah* Mwenyezi Mungu ajalie hilo liwezekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zedi. Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu kwa leo wamemalizika. Nawashukuruni sana kwa ushirikiano mkubwa tuliokuwa nao kwa siku hii ya leo. Sasa naomba niahirishe kikao hiki mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.40 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 19 Juni, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*